Hii ni Nakala ya Mtandao (Online Document)

# BUNGE LA TANZANIA

---

## MAJADILIANO YA BUNGE

---

## MKUTANO WA KUMI NA NNE

**Kikao cha Kwanza - Tarehe 3 Februari, 2004**

*(Mkutano Ulianza Saa Tatu Asubuhi)*

## D U A

*Spika (Mhe. Pius Msekwa) Alisoma Dua*

## KIAPO CHA UAMINIFU

Mjumbe afuataye aliapa kiapo cha uaminifu na kukaa katika nafasi yake ndani ya Bunge:-

Mheshimiwa Charles Makongoro Nyerere.

## TAARIFA YA SPIKA

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, kama kawaida taarifa inahusu Miswada iliyopitishwa na Bunge hili katika Mkutano wake wa Kumi na Tatu, nayo ni kwamba, Miswada ya Sheria iliyopitishwa katika Mkutano huo ilikuwa ni minane. Miswada saba kati ya hiyo imekwishapata kibali cha Mheshimiwa Rais na sasa ni Sheria za nchi. Muswada wa nane ambao haujapata kibali ni ule unaoitwa *The Merchant Shipping* haujapata kibali kwa vile kazi ya kuuchapa upya baada ya kupitishwa na Bunge imechukua muda mrefu, kwa sababu ya mabadiliko yaliyofanywa. Kwa hiyo, bado haujapelekwa kwa Mheshimiwa Rais, itakapokuwa kazi hiyo imekamilika nitaliarifu Bunge. Tunaendelea na *Order Paper,* Katibu.

## HATI ZILIZOWASILISHWA MEZANI

Hati ifuatayo iliwasilishwa Mezani na:-

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU (MHE. WILLIAM V. LUKUVI):**

Nakala za Matoleo yote ya Gazeti la Serikali pamoja na nyongeza zake zilizochapishwa tangu Kikao cha Mwisho cha Mkutano wa Bunge uliopita.

## MASWALI NA MAJIBU

Na. 1

**Mgombea Binafsi wa Ngazi ya Uongozi wa Taifa**

**MHE. DR. AMANI W. A. KABOUROU** aliuliza:-

Je, Serikali inaweza kutoa kauli kuelezea sababu za msingi zinazoifanya isipitishe sheria inayoruhusu kuwepo kwa mgombea binafsi katika nafasi za Uongozi wa ngazi za Taifa na Serikali za Mitaa?

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU (MHE. MOHAMMED SEIF KHATIB)** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Dr. Amani Walid Kabourou, Mbunge wa Kigoma Mjini, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, Sheria ya Uchaguzi Na. 1 ya mwaka 1985, katika Fungu la 30, kama ilivyofanyiwa marekebisho na Sheria Na. 32 ya mwaka 1994, kuhusu nafasi ya Rais, Fungu 36 la sheria hiyo hiyo kuhusu nafasi za Ubunge na Sheria ya Uchaguzi wa Serikali za Mitaa Na. 4 ya mwaka 1979 Fungu 39(2)(g) kuhusu nafasi za Udiwani, zinatamka wazi kuwa wagombea wa nafasi hizo ni lazima wawe wanachama wa Chama cha Siasa na wawe wamedhaminiwa na chama ambacho kina usajili wa kudumu na kwa nafasi ya Urais, jina la aliyeteuliwa kwa nafasi hiyo ni lazima liwasilishwe kwenye Tume ya Uchaguzi na Chama cha Siasa chenye usajili wa kudumu. Aidha, dhana hii inabainishwa katika Katiba ya Nchi yetu ya mwaka 1977, fungu 39(2) kwa nafasi ya Rais, Fungu 67(1) (b) na Fungu 77(3)(a)(b) vya Sheria ya Uchaguzi wa Serikali za Mitaa Na. 4 ya mwaka 1979. Hivyo wagombea binafsi wanazuiwa Kikatiba na Kisheria kugombea.

Mheshimiwa Spika, kama wagombea binafsi wangeruhusiwa, kungekuwepo na utitiri wa wagombea binafsi ambao hawana sera wala itikadi. Aidha, mfumo huo ungeweza kuchochea udini, ukabila au ubaguzi wa rangi, ujinsia na umajimbo. Pia nafasi za uongozi zingeweza kushikwa na matajiri tu wa nchi hii. Nia yetu ni kuendeleza umoja na mshikamano wa Tanzania. Bado nchi yetu ni changa hivyo mfumo wa wagombea kudhaminiwa na vyama ni mzuri katika ujenzi wa demokrasia. Tuvipe nafasi vyama vyetu vikomae kwanza kwa sasa. *(Makofi)*

Na. 2

**Fedha za Mfuko wa *TACAIDS***

**MHE. DR. BATILDA S. BURIAN** aliuliza:-

Je, ni Wilaya ngapi zimeshapata mgao wa fedha na kwa kiasi gani kutoka katika Mfuko wa *TACAIDS* kwa ajili ya utekelezaji wa programu za UKIMWI katika Wilaya hizo?

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU (MHE. WILLIAM V. LUKUVI)** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kabla ya kujibu swali la Mheshimiwa Dr. Batilda Burian, Mbunge wa Viti Maalum, napenda kutoa maelezo yafuatayo:-

Mheshimiwa Spika, kwanza nampongeza Mheshimiwa Dr. Batilda Burian, kwa namna anavyotoa msukumo na kuhimiza utekelezaji wa programu za kupambana na UKIMWI.

Mheshimiwa Spika, Serikali kupitia Ofisi ya Rais, TAMISEMI, imetoa Mwongozo kwa Mujibu wa Sheria ya Tume ya Kudhibiti UKIMWI Tanzania Na. 23 ya mwaka 2001. Hivi sasa TAMISEMI kwa kushirikiana na *TACAIDS,* wametoa mafunzo kwa Wajumbe wa Sekretarieti za Mikoa na wanaendelea kutoa mafunzo hayo hadi kwenye Halmashauri zote za Wilaya/Miji/Manispaa na Majiji.

Mheshimiwa Spika, baada ya maelezo hayo sasa naomba kujibu swali la Mheshimiwa Dr. Batilda Burian, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, Halmashauri 57 zimepatiwa jumla ya shilingi 1,425,679,747/= kutoka Mfuko wa *TACAIDS* kwa ajili ya utekelezaji wa programu za UKIMWI.

Mheshimiwa Spika, napenda kutoa wito kwa Halmashauri na Mikoa yote nchini, kutoa kipaumbele kwenye suala zima la utekelezaji wa Mwongozo na Programu za UKIMWI katika Wilaya ili kampeni dhini ya UKIMWI iweze kufanikiwa.

**MHE. DR. BATILDA S. BURIAN:** Mheshimiwa Spika, nashukuru kwa kupata nafasi ya kuuliza swali la nyongeza. Kwa kuwa katika swali langu la msingi nilizungumzia kiasi cha mgao wa fedha pamoja na maeneo zilikotumika hizo fedha katika Programu. Ningeomba Mheshimiwa Waziri pamoja na majibu yake mazuri anielezee tu kwa kifupi ni maeneo gani yaliyotumika katika miradi hiyo?

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU (MHE. WILLIAM V. LUKUVI):** Mheshimiwa Spika, ninayo taarifa ya nyongeza ambayo nilipanga nimpe Mheshimiwa Dr. Batilda Burian, kwa sababu ni ndefu. Orodha ya Wilaya zote na shughuli ambazo kila Wilaya waliomba kufanya kwa ajili ya fedha hizo, nitampa. Lakini hata hivyo kwa nyongeza nataka kumkumbusha kwamba, Jumamosi tumeandaa semina maalum, *TACAIDS* itakuja hapa kutoa semina maalum juu ya Mwongozo huo wa TAMISEMI na Programu mbalimbali zinazotekelezwa na *TACAIDS* ili Waheshimiwa Wabunge muweze kufahamu na kutoa mchango zaidi wa kuimarisha shughuli zao.

Mheshimiwa Dr. Batilda Burian nitampa taarifa, lakini naomba na Jumamosi atumie fursa hiyo kupata ufafanuzi mwingi zaidi kwa sababu wahusika wote watakuwa hapa.

**MHE. RUTH B. MSAFIRI:** Mheshimiwa Spika, ahsante sana kwa kunipa nafasi ya kuuliza swali dogo la nyongeza. Kwa kuwa Wilaya ya Muleba ni moja kati ya Wilaya zilizopata mgao wa kwanza kabisa na tayari fedha hizo zilikwishatumika kwa kadri ya makubaliano na tukaweka mipango inayofuata. Je, Serikali itakuwa tayari sasa kuipatia Wilaya ya Muleba fedha za kuendeleza utekelezaji wa ile mipango iliyokuwa inafuata?

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU (MHE. WILLIAM V. LUKUVI):** Mheshimiwa Spika, kwa sasa utoaji wa fedha hizo tumesimamisha kidogo. Kazi inayoendelea sasa ni kutoa mafunzo kwa waendeshaji wa zile Kamati za Kupambana na UKIMWI za Wilaya, namna ya kufahamu kwa pamoja Mwongozo uliotolewa na TAMISEMI na Programu zote, kazi hiyo imeanza, Sekretariet za Mikoa tumemaliza, wanaingia kwenye Halmashauri zote za Wilaya. Baada ya hapo sasa tutaanza kutoa fedha za awamu ya pili.

Na. 3

**Mpango Shirikishi Jamii**

**MHE. DIANA M. CHILOLO** aliuliza:-

Kwa kuwa Mpango Shirikishi Jamii ni mpango ambao umewapa wananchi uwezo wa kuamua mambo yao wenyewe ya kuwaletea maendeleo na unawahamasisha kuibua fikra za kuchangia mawazo juu ya utekelezaji wa kuondoa umaskini:-

(a) Je, tangu mpango huo uanze hadi sasa ni Mikoa mingapi imefanikiwa na kwa kiwango gani na ni Mkoa upi unaongoza?

(b) Je, Serikali ina mikakati gani ya kuendeleza mpango huo kwa nchi nzima?

**NAIBU WAZIRI WA MAENDELEO YA JAMII, JINSIA NA WATOTO** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Diana Mkumbo Chilolo, Mbunge wa Viti Maalum, lenye sehemu (a) na (b) kama ifuatavyo:-

(a) Napenda kukubaliana na Mheshimiwa Mbunge kwamba, ushiriki wa wananchi katika kutayarisha Mpango Shirikishi Jamii unawapa wananchi uwezo wa kuamua mambo yao wenyewe na kuibua fikra za kushiriki katika utekelezaji wa mpango huo kwa madhumuni ya kujiletea maendeleo na hatimaye kuondoa umaskini. Aidha, utaratibu wa Mpango Shirikishi unawapa wananchi umiliki wa matokeo ya ushiriki wao. Kila Wizara na Mkoa au Mkoa husika huwa inafanya tathmini ya programu zake kwa wakati tofauti. Kwa mfano, Wizara ya Elimu na Utamaduni imefanya tathmini ya Mpango wa Maendeleo wa Elimu ya Msingi *(PEDP)* kufikia Desemba, 2003. Hali kadhalika Wizara yangu imefanya tathmini ya mradi wa *HESAWA.*

Katika Mkoa wa Singida ambako Mheshimiwa Mbunge anatoka, utaratibu wa Mpango Shirikishi umeleta manufaa makubwa katika ujenzi wa madarasa, nyumba za walimu, vyoo vya shule, Zahanati, kilimo na hifadhi ya mazingira kwa misaada ya mashirika mbalimbali. Mkoa huo ni miongoni mwa Mikoa inayoongoza katika kutathmini na kutekeleza Mipango Shirikishi Jamii. Ndiyo maana wafadhili na Mashirika yasiyo ya Kiserikali, pamoja na ya Kimataifa yamekuwa yakisaidia utekelezaji wa miradi katika sekta mbalimbali kwa mafanikio, kwa kuwashirikisha wananchi. Baadhi ya Mashirika hayo ni *IFAD, TASAF, UNICEF, World Vision, TCRS* na *SIDA.* Mashirika haya huwashirikisha kikamilifu wananchi katika kubuni, kupanga na kutekeleza miradi hiyo. Aidha, miradi hiyo ina nafasi nzuri ya kuwa endelevu kwa kuwa wananchi wanaiona kuwa ni yao.

(b) Mheshimiwa Spika, Serikali wakati wote imekuwa ikiandaa sera, mikakati na programu zinazozingatia ushiriki wa watu katika utekelezaji wake. Azma hii ya Serikali imezingatiwa kwenye Dira ya Taifa ya Maendeleo hadi mwaka 2025, Mkakati wa Kupunguza Umaskini,pamoja na Sera. Ofisi ya Rais Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa, inaendelea kuzijengea uwezo Halmashauri za Wilaya, Miji, Manispaa na Jiji, kwa kutumia mbinu shirikishi mahsusi iitwayo Fursa na Vikwazo vilivyopo katika jamii. Tayari Halmashauri 27 zimekwisha fundishwa matumizi ya mbinu hii.

Aidha, Wizara yangu hutoa mafunzo ya Stashahada na Mafunzo ngazi ya Cheti ya Wataalam wa Maendeleo ya Jamii katika vyuo vyake vya Tengeru, Buhare, Rungemba na Misungwi. Wataalam hao wanazo stadi za kuwezesha jamii kutumia mbinu shirikishi katika uandaaji na utekelezaji wa mipango yao ya maendeleo.

**MHE. DIANA M. CHILOLO:** Mheshimiwa Spika, nashukuru kwa majibu mazuri ya Mheshimiwa Naibu Waziri. Kwa kuwa Mheshimiwa Naibu Waziri ametaja Mpango wa Maendeleo wa Elimu ya Msingi yaani *PEDP:-*

(a) Je, anaweza akanitajia baadhi ya Mikoa na Wilaya ambazo zimevuka lengo katika ujenzi wa madarasa, nyumba za walimu pamoja na kununua madawati?

(b) Kwa kuwa Mikoa ambayo imeendesha mpango huo imeonyesha mafanikio makubwa. Je, Serikali haioni kwamba kuna umuhimu wa kuhakikisha kwamba Mpango huu unaendeshwa nchi nzima na katika Mikoa ambayo imefika mahali imeanza kuacha kuuendeleza mpango huu bila kukoma?

**NAIBU WAZIRI WA MAENDELEO YA JAMII, JINSIA NA WATOTO:** Mheshimiwa Spika, swali lake la kwanza angependa kufahamu maendeleo ya mradi wa *PEDP* Mikoani. Naomba tu niseme kwamba, kwa upande wa utengenezaji wa madawati Wilaya ya Rombo Mkoani Kilimanjaro matarajio yao yalikuwa kutengeneza madawati 1,167, lakini wametengeneza madawati 1,431. Kwa upande wa Shinyanga hususan Bukombe matarajio ni madawati ...

**SPIKA:** Labda ungefanya kama alivyofanya Waziri mwenzako kwamba utampa hiyo orodha baadaye.

**NAIBU WAZIRI WA MAENDELEO YA JAMII, JINSIA NA WATOTO:** Mheshimiwa Spika, sawa. Nashukuru kwamba nitakupatia hiyo orodha. La pili, kwa upande wa programu hizi kuenea nchi nzima. Naafikiana na Mheshimiwa Diana Chilolo kwamba, wazo lake ni zuri. Kwa mfano, Programu hii ya Elimu *(PEDP),* ipo nchi nzima. Kwa upande wa *TASAF*, Tanzania Zanzibar Wilaya zote

10 zinanufaika na mpango huu na uwezo ukiwepo ni kweli kabisa tunaweza kufikisha programu hizi zote katika nchi nzima. Ahsanteni sana.

**MHE. MGANA I. MSINDAI:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi niulize swali moja la nyongeza. Kwa kuwa dhana hii imepokelewa vizuri sana na wananchi wa Mkoa wa Singida na Mikoa mingine; na kwa kuwa dhana hii kuanzia mwaka 2002 imeanza kufifia Mkoani Singida; je, Serikali itaendelea kutilia mkazo kwa sababu wananchi wameshakubali kusaidiana nao katika kuwaletea maendeleo kwa kupanga miradi yao kufuatana na uzito wanaoupendekeza wao?

**NAIBU WAZIRI WA MAENDELEO YA JAMII, JINSIA NA WATOTO:** Mheshimiwa Spika, Serikali inakubali kufanya kazi kwa karibu sana na wakazi au wananchi wa Mkoa wa Singida maana imefanya hivyo na itaendelea kufanya hivyo siyo tu kwa Mkoa wa Singida bali kwa nchi nzima. Ahsanteni.

Na. 4

**Utengenezaji wa Noti Bandia**

**MHE. PAUL P. KIMITI** aliuliza:-

Kwa kuwa umezuka mtindo kwa watu wasio waaminifu, kugushi na kuiga utengenezaji wa noti bandia mara zinapotolewa na Benki Kuu:-

(a) Je, Serikali inasema nini juu ya ukweli kwamba hata kabla ya noti hizo hazijatolewa, wanakuwa wamekwishapata aina ya noti zenyewe zinazokusudiwa kutengenezwa ili waziige na kuzisambaza kwa wakati mmoja na zile halisi?

(b) Je, kwa nini panakuwepo na malumbano kati ya Benki Kuu na uongozi wa Polisi mara wanapotangaza kuwepo kwa noti hizo bandia za fedha?

(c) Je, Serikali ina mpango gani wa kuendelea kuwafundisha wananchi ili wasidanganywe na fedha hizo bandia?

**NAIBU WAZIRI WA FEDHA (MHE. DR. FESTUS B. LIMBU)** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Paul P. Kimiti, Mbunge wa Sumbawanga Mjini, lenye sehemu (a), (b) na (c) kama ifuatavyo:-

(a) Mheshimiwa Spika, ukweli kwamba wahalifu huwa wamekwishapata aina ya noti zinazokusudiwa kutengenezwa ili wazigushi na kuziingiza wakati mmoja na noti mpya halali bado haujaifikia Serikali. Kama kuna mtu aliye na taarifa hizo basi tunamwomba aishirikishe Serikali. Lakini napenda tu niseme kwamba, hakuna ukweli katika usemi huo. Utengenezaji wa noti halali hufanywa kwa siri na tahadhari kubwa ili kuhakikisha usalama wa noti hizo. Noti nyingi zilizogushiwa zikichunguzwa vizuri huonekana kuwa hazitengenezwi kwa utaalamu mkubwa. Nyingi zinagushiwa kwa *photocopy* za rangi za kisasa na pia wahalifu wengi hugushi kwa kutumia *Scanning Machines* za kisasa.

Mtu yeyote aliye maskini katika kuzitazama noti bandia, atagundua kuwa ni hafifu na pia hazina alama zote za usalama zinazoonekana katika noti halali.

(b) Mheshimiwa Spika, Benki Kuu imenihakikishia kuwa hakukuwa na malumbano kati ya Polisi na Benki Kuu kuhusu noti bandia. Benki Kuu na Polisi wamekuwa na uhusiano mzuri na wa karibu kwa miaka mingi katika kudhibiti noti bandia. Polisi na Benki Kuu wana utaratibu maalum ambao wameutumia kwa miaka mingi katika kulikabili na kudhibiti tatizo la noti bandia. Ukweli ni kwamba, wakati Polisi ilipokutana na Waandishi wa Habari kuhusu noti bandia walizokuwa wamezikamata, baadhi ya magazeti yaliandika kuwa kulikuwa na malumbano kati ya Benki Kuu na Polisi. Lakini ukweli ni

kwamba wakati ule wote Benki Kuu haikutoa taarifa yoyote ile kuhusu noti bandia au kuhusu usemi wa Polisi. Benki Kuu haikutoa taarifa yoyote kukanusha au kukubaliana na taarifa ya Polisi.

(c) Mheshimiwa Spika, Serikali inanuia kuendelea kuwafundisha wananchi ili wasidanganywe na fedha hizo bandia. Lakini kinga kubwa kabisa ya kutokudanganywa ni kila mwananchi kuwa makini kuzichunguza noti kabla ya kuzipokea. Noti nyingi za bandia hujulikana kwa urahisi kwa kuwa hazifafanani na noti halali kwa kuzingatia zile alama za usalama na pia noti bandia hutengenezwa na kukopiwa kwa kutumia karatasi ya kawaida ambayo ni nyepesi zaidi kuliko karatasi ya noti halali. Kabla noti mpya hazijatolewa, Serikali ilitoa matangazo kwa njia ya vyombo vya habari mbalimbali na kwa vipeperushi na mabango kote nchini juu ya sura na alama za usalama za noti mpya.

Matangazo hayo yalitangazwa kwa muda mrefu kwa madhumuni ya kuhakikisha kwamba, watu wote wanaelewa alama muhimu zinazowawezesha kuzitambua noti halali ili kutofautisha na noti bandia kwa urahisi. Ni dhahiri kuwa elimu iliyotolewa kwa wananchi wa Tanzania imezaa matunda kwa kuwawezesha wananchi kuwa mstari wa mbele katika kuzitambua noti bandia. Inaonekana kuwa kuzagaa kwa noti bandia kunatokana na uwezo wa wananchi kuzitambua kwa urahisi noti hizo za bandia na siyo kuwa kugushi kumeongezeka, kwani noti bandia zinazoifikia Benki Kuu hazijaongezeka.

Mheshimiwa Spika, ni muhimu kuelewa kuwa hakuna utaalamu duniani unamzuia mhalifu kutenda kosa la kihalifu ambalo amedhamiria kulitenda. Hivyo umadhubuti wa noti haumzuii mhalifu kujaribu kugushi noti hizo. Kitu ambacho kitamkatisha tamaa mhalifu ni kuona kuwa anashindwa kutumia ama kuziingiza katika mzunguko noti zake za bandia. Jambo hilo litatokea ikiwa mtu wa kwanza atakayemlenga kumpa noti hizo mara moja atazikataa kuzipokea kwa kuwa ametambua kuwa ni noti za bandia. Basi Mhalifu huyo akiona anashindwa kuziingiza noti zake za bandia kwenye mzunguko hatimaye ataacha kuendelea kujaribu kugushi noti hizo kwani ataona kuwa zinampa hasara.

**MHE. PAUL P. KIMITI:** Mheshimiwa Spika, nashukuru kwa majibu mazuri ya Mheshimiwa Naibu Waziri wa Fedha. Kwa kuwa suala zima ambalo nilikuwa nimeliuliza ni suala ambalo lilijitokeza katika Vyombo vya Habari na wote ni mashahidi waliona malumbano yaliyokuwa yamejitokeza. Sasa maswali mawili ya nyongeza:-

(a) Kwa kuwa moja ya sifa kubwa za Utawala Bora ni pamoja na uongozi wa pamoja; na kwa kuwa kumeendelea kujitokeza baadhi ya vitendo ambavyo baadhi ya Wizara wamekuwa wakitupiana mpira, ukichukua mfano wa *Tanzania Elimu Suppliers,* wafanyakazi wamekuwa na matatizo mara waende Wizara ya Afya na mara waende Wizara ya Elimu na Utamaduni; sasa hivi isingekuwa vizuri kama kungekuwa na utaratibu wa *One Stop Center* ili matatizo ya wafanyakazi yajulikane yanakwenda kwa nani?

(b) Je, Serikali ina mpango gani kuhakikisha kwamba mambo ambayo yanajitokeza katika Wizara moja yanashughulikiwa na Serikali kwa wakati mmoja badala ya kuonekana kila Wizara inafanya mambo yake peke yake?

**NAIBU WAZIRI WA FEDHA (MHE. DR. FESTUS B. LIMBU):** Mheshimiwa Spika, Serikali ni moja na utendaji wa kazi ni mmoja na kila Idara ama kila Kitengo cha Serikali kinafanya kazi kulingana na majukumu yake na hivyo Polisi wanafanya kazi yao ya kuzuia uhalifu na Benki Kuu wanafanya kazi yao ya kuhakikisha kwamba Sekta ya Fedha inafanya kazi nzuri.

Mheshimiwa Spika, kwa kweli utakubaliana na mimi kwamba, Benki Kuu imejitahidi sana kuhakikisha kwamba Sekta ya Fedha inaimarika na hatimaye mfumuko wa bei unashuka hadi kufikia *digit* moja kutoka *digits* mbili. Kwa hiyo, malumbano yalikuwepo mimi naweza kusema kwamba hayakuwa halisi kwa sababu Benki Kuu wana majukumu yao na Polisi wana majukumu yao.

**SPIKA:** Mheshimiwa Hamad Rashid Mohamed, samahani ngoja kidogo kuna majibu ya nyongeza kutoka kwa Mheshimiwa Waziri Mkuu.

**WAZIRI MKUU:** Mheshimiwa Spika, napenda niongezee tu majibu ya nyongeza kwa majibu mazuri ya Mheshimiwa Naibu Waziri. Mwuliza swali Mheshimiwa Paul Kimiti, amezungumzia pia suala la wafanyakazi wa *Tanzania Elimu Suppliers* ingawa kwa hakika halihusiani kabisa na noti bandia. Lakini napenda tu nimjibu kwamba, wafanyakazi hao wamekuwa wakifuata taratibu za kawaida na wamefika kwenye Wizara zinazohusika na ukitaka kujua *One Stop Centre* ya Serikali ni kwa Waziri Mkuu na hao wafanyakazi wamekwishafika. *(Makofi)*

**MHE. HAMAD RASHID MOHAMED:** Mheshimiwa Spika, pamoja na majibu mazuri ya Mheshimiwa Naibu Waziri, nina swali la nyongeza.

Kwa kuwa hizi noti za bandia ambazo zinagushiwa zinazunguka katika vyombo vya fedha; na kwa kuwa katika hivyo vyombo vya fedha wakati mwingine unalipwa na unazipata hizo noti bandia. Kwa mfano, mimi mwenyewe nililipwa *Barclays Bank* imepita kwenye *system* na halafu ikaonekana ni ya bandia. Je, Mheshimiwa Naibu Waziri, atakubaliana nami kwamba udhaifu huo unaweza uka-*penetrate* katika *system* za benki na mtu akalipwa fedha za bandia kama nilivyolipwa mimi?

**NAIBU WAZIRI WA FEDHA (MHE. DR. FESTUS B. LIMBU):** Mheshimiwa Spika, siyo rahisi Sekta ya Fedha ama Benki kutoa fedha bandia na kama hilo lilitokea kwa Mheshimiwa Mbunge, basi Wizara ya Fedha haikuwa na taarifa, angetutaarifu tungelifuatilia hilo suala kwa ukaribu na kama itatokea kwa mwananchi yeyote akalipwa fedha za bandia kutoka Benki, basi aitaarifu Serikali mara moja na sheria zitachukuliwa dhidi ya Benki hiyo.

Na. 5

**Marekebisho katika Sekta ya Fedha**

**MHE. HENRY D. SHEKIFFU (k.n.y. MHE. WILLIAM H. SHELLUKINDO)** aliuliza:-

Kwa kuwa Serikali imekamilisha azma yake ya kurekebisha Sekta ya Fedha na kujitoa katika Uendeshaji wa Benki na Taasisi nyingine za Fedha:-

(a) Je, hadi kufikia Juni, 2003 ni Benki na Taasisi ngapi za shughuli za Kifedha zimekuwepo hapa nchini zikitajwa kwa majina, Mji/Wilaya ambamo zimo na matawi yake?

(b) Je, ni Benki ngapi zenye hisa kiasi gani za Serikali na au za Watanzania Wazalendo na ni zipi zina utaratibu wa kutoa mikopo ya shughuli za Kilimo na uzalishaji mali mwingine?

(c) Je, tangu marekebisho hayo yafanyike ni Benki na Taasisi ngapi za fedha zimefilisika?

**NAIBU WAZIRI WA FEDHA (MHE. DR. FESTUS B. LIMBU)** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, napenda kujibu swali la Mheshimiwa William H. Shellukindo, Mbunge wa Bumbuli, lenye sehemu (a), (b) na (c) kama ifuatavyo:-

(a) Hadi kufikia Juni, 2003 kulikuwa na jumla ya Mabenki ya Biashara 23 na taasisi nyingine za fedha 8, yakitoa huduma za kibenki katika maeneo mbalimbali hapa nchini. Kati ya Mabenki ya Biashara 23, *National Micro-Finance Bank*, ndio yenye mtandao mpana zaidi ikiwa na jumla ya matawi 105 ikifuatiwa na *NBC Limited* matawi 31 na *CRDB Bank* matawi 25. Benki inayofuatia ni *Standard Chartered Bank* yenye matawi 6, Benki zingine zina matawi pungufu ya matano. Kati ya taasisi nyingine za fedha yenye mtandao mpana kuliko zote ni *Tanzania Postal Bank,* ambayo ina matawi 20 na zinazofuatia ni *National Bureau De Change Limited* na *Savings and Finance* zenye matawi 2 kila moja na zingine zilizobaki zina tawi moja moja.

(b) Mheshimiwa Spika, Serikali ina hisa katika Benki na taasisi za fedha zifuatazo:-

| JINA LA BENKI | HISA |
|---|---|
| *National Micro-finance Bank Limited* | 100% |
| *Tanzania Postal Bank* | 89.5% |
| *Tanzania Investment Bank Limited* | 100% |
| *National Bureau De Change* | 100% |
| *People's Bank of Zanzibar* (Serikali ya Zanzibar) | 100% |
| *NBC Limited* | 30% |

Watanzania Wazalendo ama Makampuni ya Wazalendo yana hisa katika Benki na taasisi za fedha zifuatazo:-

| | |
|---|---|
| *CRDB Bank (T) Limited* | 70% |
| *Exim Bank Limited* | 80% |
| *Akiba Commercial Bank Limited* | 60% |
| *CF Union Bank Limited* | 74% |
| *Azania Bankcorp Limited* | 90% |
| *Mufindi Community Bank Limited* | 100% |
| *Mwanga Rural Community Bank* | 100% |
| *Mbinga Community Bank* | 100% |
| *Kagera Farmers Co-operative Bank* | 100% |
| *Dar es Salaam Community Bank* | 100% |

Mheshimiwa Spika, Mabenki yote 23 isipokuwa 5 tu yalitoa mikopo ya shughuli za kilimo. Mabenki ambayo hayakutoa mikopo hadi kipindi hicho ni *United Bank of Africa, National Microfinance Bank, Federal Bank of the Middle East Limited, Mbinga Community Bank* na *Dar es Salaam Community Bank.* Taasisi za fedha zote 8 zilitoa mikopo ya shughuli za kilimo isipokuwa *Savings and Finance.* Kuhusu mikopo kwa ajili ya uzalishaji mali mwingine, mabenki na taasisi zote za fedha zilitoa mikopo hiyo.

(c) Mheshimiwa Spika, tangu marekebisho ya Sekta ya Fedha yaanze, jumla ya Mabenki matatu yamefilisika. Mabenki hayo ni *Tanzania Housing Bank (THB), Greenland Bank (T) Limited na Meridian Biao (T) Limited.*

(b) Mheshimiwa Spika, Serikali ina hisa katika Benki na taasisi za fedha zifuatazo:-

| JINA LA BENKI | HISA |
|---|---|
| *National Micro-finance Bank Limited* | 100% |
| *Tanzania Postal Bank* | 89.5% |
| *Tanzania Investment Bank Limited* | 100% |
| *National Bureau De Change* | 100% |
| *People's Bank of Zanzibar* (Serikali ya Zanzibar) | 100% |
| *NBC Limited* | 30% |

Watanzania Wazalendo ama Makampuni ya Wazalendo yana hisa katika Benki na taasisi za fedha zifuatazo:-

| | |
|---|---|
| *CRDB Bank (T) Limited* | 70% |
| *Exim Bank Limited* | 80% |
| *Akiba Commercial Bank Limited* | 60% |
| *CF Union Bank Limited* | 74% |

| | |
|---|---|
| *Azania Bankcorp Limited* | 90% |
| *Mufindi Community Bank Limited* | 100% |
| *Mwanga Rural Community Bank* | 100% |
| *Mbinga Community Bank* | 100% |
| *Kagera Farmers Co-operative Bank* | 100% |
| *Dar es Salaam Community Bank* | 100% |

Mheshimiwa Spika, Mabenki yote 23 isipokuwa 5 tu yalitoa mikopo ya shughuli za kilimo. Mabenki ambayo hayakutoa mikopo hadi kipindi hicho ni *United Bank of Africa, National Microfinance Bank, Federal Bank of the Middle East Limited, Mbinga Community Bank* na *Dar es Salaam Community Bank.* Taasisi za fedha zote 8 zilitoa mikopo ya shughuli za kilimo isipokuwa *Savings and Finance.* Kuhusu mikopo kwa ajili ya uzalishaji mali mwingine, mabenki na taasisi zote za fedha zilitoa mikopo hiyo.

( c) Mheshimiwa Spika, tangu marekebisho ya Sekta ya Fedha yaanze, jumla ya Mabenki matatu yamefilisika. Mabenki hayo ni *Tanzania Housing Bank (THB), Greenland Bank (T) Limited na Meridian Biao (T) Limited.*

**MHE. HENRY D. SHEKIFFU:** Mheshimiwa Spika, nafurahi kwa majibu mazuri kutoka kwa Naibu Waziri.

Kwa kuwa kwa kipindi kirefu suala la kilimo halijapewa umuhimu wa kwanza katika utoaji wa mikopo ya kilimo na zaidi ya asilimia 80 ya uchumi wetu unategemea kilimo. Je, Serikali inatamka nini katika kuhakikisha kwamba katika Benki zetu kunakuwa na chombo au taasisi maalum inayoshughulikia kilimo?

Pili, kwa kuwa mwisho wa mwaka 2003, Rais alimwalika Profesa kutoka Brazil kwa nia nzuri ya kujenga hisia za kuwawezesha Watanzania. Je, tumejifunza nini kutoka kwa Profesa huyu; je, tuna dhamira ya kweli ya kuwasaidia Watanzania ili waweze kumudu maisha yao na shughuli zao za biashara pamoja na kilimo? *(Makofi)*

**NAIBU WAZIRI WA FEDHA (MHE. DR. FESTUS B. LIMBU):** Mheshimiwa Spika, katika jibu langu la msingi nilitaja Mabenki ambayo yametoa mikopo katika shughuli za kilimo na hadi Juni, 2003 jumla ya Sh. 96.6 bilioni zilitolewa kwa ajili ya kilimo ukilinganisha na Sh.713 bilioni zilizotolewa katika uzalishaji mwingine. Pia taasisi za fedha zilitoa Sh.104 bilioni katika shughuli za kilimo ukilinganisha na Sh. 700 bilioni. Sasa napenda kusema tu kwamba, kilimo kama tunavyofahamu wote ni shughuli ambayo ni *risk* kwa hiyo taasisi za fedha nyingi hazipendi kujiingiza kwa sababu inategemea hali ya hewa na uzalishaji mwingine. Kwa hiyo, Benki zikiweka fedha zake katika kilimo kunakuwa na *risk* kubwa. Lakini ni kweli kwamba, Serikali inaandaa mikakati ya kuwa na taasisi ama chombo maalum kinachoshughulikia kilimo. Kwa hiyo, tulianzisha *Export Credit Guarantee Scheme* kwa ajili ya ku-*finance* shughuli za kilimo zaidi. Pia tulianzisha katika Bajeti ya mwaka huu ambayo inafanyiwa kazi, *guarantee scheme* kwa ajili ya shughuli ndogo ndogo *(SMAs)* katika kilimo na karibu itaanza kufanya kazi na wananchi watataarifiwa ipasavyo.

Kuhusu swali la pili la nyongeza la Mheshimiwa Shekiffu kwamba, Profesa kutoka Amerika ya Kusini, ambaye anaitwa Profesa Dissoto. Suala hilo linafanyiwa kazi kwa karibu na tunaamini kwamba, mkakati huo utakapokamilika, pamoja na mikakati mingine ya Serikali kufikia mwaka 2020, kama ambavyo *Tanzania Vision* inasema, tutakuwa tumepiga hatua kubwa. *(Makofi/Kicheko)*

**MHE. DR. CHRISANT M. MZINDAKAYA:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru naomba sasa kuuliza swali la nyongeza. Nchi nyingi ambazo zimepiga hatua katika kilimo kama vile India, Malaysia, Philippines, ni nchi ambazo sera za nchi zenyewe na kwa kusimamiwa na Benki Kuu, Benki imeweka katika sheria zake kutoa malengo na kuwalazimisha wenye Benki kutoa mikopo kwa sekta ya kilimo kwa asilimia inayokubaliwa. Benki hizo zisipotekeleza maagizo ya Benki Kuu fedha hizo huchukuliwa kama adhabu kufidia ukopeshaji, je, sisi tutafika lini huko? *(Makofi)*

**NAIBU WAZIRI WA FEDHA (MHE. DR. FESTUS B. LIMBU):** Mheshimiwa Spika, mchango wa Mheshimiwa Mbunge ni muhimu tutaufanyia kazi kutokana na uzoefu ambao ameutaja.

**SPIKA:** Napenda kuwaarifu Waheshimiwa Wabunge kwamba, *Radio Tanzania Dar es Salaam* wana matatizo ya kiufundi. Kwa kawaida maswali hutoka moja kwa moja. Sasa hivi maswali haya na majibu hayasikiki kwa sababu ya matatizo ya kiufundi. Tunaendelea. *(Makofi/Kicheko)*

Na. 6

**Mashamba ya Serikali Kugawiwa/Kumilikiwa na Wananchi**

**MHE. AGGREY D. J. MWANRI** aliuliza:-

Kwa kuwa zoezi zima la ubinafsishaji wa Mashirika ya Umma kwa sasa unafikia hatma; na kwa kuwa wananchi wa Kata ya *West Kilimanjaro* Jimboni Siha wamekuwa wakisubiri kwa hamu kubwa kupatiwa makazi ya kudumu kama ambavyo Serikali imekuwa ikiwaahidi:-

(a) Je, kwa nini zoezi hilo linaelekea kuchukua muda mrefu kiasi hicho na ni utaratibu gani ulioandaliwa na Serikali wa kuhakikisha kuwa wananchi wote waishio West Kilimanjaro watapata maeneo ya kudumu hasa ikizingatiwa kuwa Serikali inakusudia kubinafsisha mashamba ya umma kama vile *NAFCO*, kwa watu binafsi?

(b) Je, Serikali ina mpango gani wa kuhakikisha kwamba wananchi wazalendo wasio na mtaji wanawezeshwa kununua/kumiliki mashamba hayo ili waweze kupunguza umaskini?

**NAIBU WAZIRI WA KILIMO NA CHAKULA** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Kilimo na Chakula, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Aggrey Deaisile Joshua Mwanri, Mbunge wa Siha, lenye sehemu (a) na (b) kama ifuatavyo:-

(a) Zoezi la ubinafsishaji wa mashamba ya *West Kilimanjaro* limechukua muda kwa kuwa Serikali imeamua kushughulikia migogoro yote iliyopo kabla ya mashamba hayo kutangazwa na hatimaye kubinafsishwa.

Katika kubinafsisha mashamba ya *NAFCO* yaliyoko *West Kilimanjaro*, hatua zifuatazo zimefikiwa:-

(i) Shamba la Rosylin linalomilikiwa na *NAFCO*, lenye ukubwa wa ekari 2,458 limetengwa kwa ajili ya kuuzwa kwa wananchi waliovamia msitu wa hifadhi ya Mlima Kilimanjaro. Halmashauri ya Wilaya ya Hai, ikisaidiwa na *PSRC*, wanaandaa mipango ya kutekeleza uamuzi huo.

(ii) Kutokana na baadhi ya wananchi wa *West Kilimanjaro* kuvamia sehemu za mashamba ya *NAFCO* na *West Kilimanjaro* na kujenga Makazi ya Kudumu, Serikali imeamua kuyapima mashamba yote upya kwa lengo la kutenga maeneo yaliyojengwa makazi ya kudumu na kuyauza kwa wananchi wanaohusika. Aidha, baada ya kutenga maeneo hayo yaliyojengwa makazi ya kudumu, sehemu za mashamba zitakazosalia zitabinafsishwa moja kwa moja.

(iii) Kampuni ya Bia Tanzania *(Tanzania Breweries Limited),* imetoa shamba la Fresian lenye ukubwa wa ekari 2,330 kwa Halmashauri ya Wilaya ya Hai ili iwagawie wananchi wa Wilaya hiyo wenye shida ya ardhi ili wasiendelee kuvamia mashamba mengine ya *TBL* yaliyoko Wilayani Hai. Mpaka sasa Halmashauri ya Wilaya ya Hai ikishirikiana na *TBL* inaendelea kupima na kugawa maeneo kwenye shamba hilo.

Mheshimiwa Spika, mahitaji ya ardhi ya wananchi wa Hai ni makubwa na hayawezi kutoshelezwa kwa kuwagawia au kuwauzia mashamba ya Serikali peke yake. Wananchi wasiokuwa na ardhi ya kutosha wanashauriwa kuhamia kwenye mikoa yenye ardhi ya kutosha.

(b) Wananchi watakaogawiwa sehemu za mashamba yanayohusika, watapewa muda wa kuyalipia. Aidha, Serikali inakamilisha mkakati wa uwezeshaji ambao utawawezesha wananchi kupata mitaji ya kuwekeza kwenye shughuli zao za uzalishaji, kama kilimo na utoaji wa huduma.

**MHE. AGGREY D. J. MWANRI:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi ya kuuliza maswali mawili madogo ya nyongeza. Napenda pia kumshukuru Mheshimiwa Naibu Waziri, kwa majibu yake mazuri na naomba niulize kama ifuatavyo:-

Kwa kuwa *squatters* walioko *West Kilimanjaro* ni watu waliofika katika eneo lile kihistoria kufuata Wazungu ambao walikuwa wamepewa maeneo yale; na kwa kuwa wao walikuwa ni vibarua wanatumika mle na mpaka sasa hivi wamekuwepo kule kwa sababu hizi hizi za shughuli za kilimo; je, ni sahihi kuwaona kwamba hawa wananchi ni wavamizi au ni watu ambao wamekwenda pale kutokana na sababu za kihistoria?

Pili, nakubaliana na majibu mazuri kwamba, Rosylin imetengwa kwa ajili ya wananchi wa *West Kilimanjaro* na kwamba sasa hivi tunapozungumza, *PSRC* inawasiliana na uongozi wa Wilaya kwa ajili ya kuona kwamba hilo linatekelezwa. Je, nikiondoka hapa niwaambie wananchi wa *West Kilimanjaro* kwamba kazi hiyo itatekelezwa lini kabla ya mwaka 2005? *(Makofi/Kicheko)*

**NAIBU WAZIRI WA KILIMO NA CHAKULA:** Mheshimiwa Spika, kiuhakika hawa ni wavamizi kwa sababu maeneo yale hayakuwa yao walikaa kinyume cha sheria. Kwa maana hiyo walikuwa wavamizi.

Pili, mlolongo wa taratibu ni mrefu utatekelezeka tu kama watafuata kama nilivyoeleza kwenye jibu la msingi.

**MHE. ESTHERINA KILASI:** Mheshimiwa Spika, nashukuru kwa kunipa nafasi niweze kuuliza swali la nyongeza.

Kwa kuwa Wilaya ya Mbarali ina mashamba ya *NAFCO* yanayofanana na Wilaya ya Siha na zoezi la kubinafsisha limeanza tangu mwaka 2001 na wananchi wamekuwa wakipewa taarifa tu kwamba litabinafsishwa au watagaiwa wakulima wadogo wadogo na sasa ni mwaka wa tatu. Je, Wizara husika ina mpango gani kuwasiliana na *PSRC* ili wananchi hawa wa Mbarali wajue zoezi hili litakamilika lini na litaanza lini?

**NAIBU WAZIRI WA KILIMO NA CHAKULA:** Mheshimiwa Spika, mpango wa kugawiwa mashamba ya *NAFCO* bado uko pale pale. Tunachofanya ni kuandaa taratibu zote kusudi isifanywe nusu nusu. Kwa hiyo, tunachoomba ni subira. Tutafanya, tumeanza na Ruvu, Dar es Salaam tutafika huko. *(Makofi/Kicheko)*

**MHE. THOMAS NGAWAIYA:** Mheshimiwa Spika, nashukuru kwa kunipa nafasi hii, naomba nimwulize Mheshimiwa Waziri. Kwa kuwa kuna njaa kali sana Tanzania sasa hivi; na kwa kuwa kuna mashamba makubwa yenye rutuba yaliyoko Tanga na Morogoro; Serikali ina mikakati gani ya kuwagawia wananchi mashamba hayo ili walime maana kuna malalamiko kwamba yamekaa bure kwa muda mrefu, Serikali ina mpango gani?

**SPIKA:** Waziri kama una majibu, unaweza kuyatoa lakini halitokani na swali la msingi. *(Makofi/Kicheko)*

**NAIBU WAZIRI WA KILIMO NA CHAKULA:** Mheshimiwa Spika, ardhi ni nyingi sana hapa nchini si lazima kungoja haya mashamba. Hata hivyo anakaribishwa kupata jibu lenye kina na pana. *(Makofi/Kicheko)*

Na. 7

**Teknolojia Mpya na Mitaji kwa Kilimo Kikubwa**

**MHE. ALHAJ SHAWEJI ABDALLAH** aliuliza:-

Kwa kuwa Kilimo kikubwa kinahitaji zana bora za kilimo kama vile mbolea, madawa, mbegu bora na kadhalika na kwa kuwa teknolojia ya kilimo hicho inahitaji njia bora za kupata taarifa mpya ya masoko, uwezo wa kifedha na mitaji, hali ambayo inakuwa vigumu kwa wakulima wadogo wadogo kuwa nazo.

Je, Serikali itakubaliana nami kwamba, teknolojia hiyo mpya, uwezo wa kifedha na mitaji kwa ajili ya kilimo hicho, inawapa uwezo wakulima wawekezaji wakubwa wa nje kuhodhi kilimo hicho na kwamba hali ya uchumi inapoyumba, wawekezaji hao huwa na tabia ya kutoa mitaji yao, hali ambayo inahitajika sasa kuwa na *Asian Tigers* kulinda wawekezaji hao na kuwa na mipango ya kuwawezesha wakulima wadogo wadogo kuwekeza katika kilimo hicho kikubwa?

**NAIBU WAZIRI WA KILIMO NA CHAKULA** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, kwa niaba ya Waziri wa Kilimo na Chakula, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Alhaj Shaweji Abdallah, Mbunge wa Kilosa, kama ifuatavyo:-

Nakubaliana na Mheshimiwa Mbunge kuwa kilimo kikubwa chenye tija na faida kinahitaji zana bora, mbolea, madawa, mbegu bora, njia bora za kupata taarifa za masoko na uwezo wa kifedha kwa wakulima wadogo na wakubwa.

Mheshimiwa Spika, zaidi ya asilimia 80 ya kilimo cha Tanzania hutegemea wakulima wadogo. Kwa mfano, kilimo cha pamba, korosho na pareto hutegemea wakulima wadogo wadogo kwa zaidi ya asilimia 80 wakati zao la chai hutegemea wakulima wadogo kwa zaidi ya asilimia 50. Mazao pekee ambayo yanategemea wakulima wakubwa kwa zaidi ya asilimia 80 ni mkonge na miwa kutokana na mazao hayo kuhitaji kulimwa kwenye mashamba makubwa na kwa upande wa miwa, kuhitaji viwanda vya gharama kubwa vya kuyasindika. Kwa mazao yote ya chakula hulimwa na wakulima wadogo kwa zaidi ya asilimia 90.

Kutokana na maelezo hayo ni dhahiri kwamba, wakulima wakubwa kwa sasa hawajahodhi kilimo cha Tanzania na kwa hiyo hawaathiri uchumi wa nchi. Hadi sasa wapo wawekezaji wachache sana kutoka nje katika kilimo na wanajishughulisha zaidi na kilimo cha miwa, chai, mkonge, kahawa, maua na mboga za majani za kuuzwa nje ya nchi. Tunahitaji kuwavutia wawekezaji wakubwa wengi zaidi ili wawekeze katika kilimo cha mashamba makubwa na kutumia raslimali za kilimo zilizopo kwa kiwango kikubwa zaidi.

Nakubaliana na Mheshimiwa Alhaj Shaweji Abdallah kwamba, kuna umuhimu wa kujenga mazingira ya kutuwezesha kupata maendeleo ya haraka kama yale ya *Asian Tigers,* lakini itabidi tutambue mambo yaliyoziwezesha nchi hizo kupata maendeleo ya haraka na mambo hayo yanayojumuisha uwekezaji kutoka nje ya nchi hizo, uwekezaji katika kilimo na ukuaji wa haraka wa sekta ya viwanda. Kwa upande wetu, tumeshaandaa Mkakati wa Kuendeleza Sekta ya Kilimo na kuanzia mwaka 2003, tumekuwa tukiandaa programu za kuitekeleza. Kinachohitajika ni mitaji ya kuwekeza kutoka ndani na nje ya nchi.

**MHE. PROF. JUMA M. MIKIDADI:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi hii niweze kuuliza swali dogo la nyongeza. Kutokana na jibu la msingi alilojibu Mheshimiwa Naibu Waziri kwamba, wakulima wakubwa sio ambao waliokuwa wanazuia maendeleo ya kilimo au uchumi wetu kukua kutokana na kilimo. Je, ikiwa hivyo ndivyo kwa nini Serikali haina mpango mahsusi wa kuweza kuwasaidia wakulima wadogo wadogo hasa kuwapa nyenzo ambazo zitaweza kuwapeleka mpaka kumiliki ulimaji huu wa mashamba makubwa?

**NAIBU WAZIRI WA KILIMO NA CHAKULA:** Mheshimiwa Spika, tunao mpango wa kusaidia wakulima wadogo wadogo kufikia hayo aliyoyataja Mheshimiwa Mbunge. Huo ni utaratibu tunaosema uwezeshaji. Tunachoomba Mheshimiwa Mbunge awe na subira, ukitoka tu tutaueneza. *(Makofi/Kicheko)*

Na. 8

**"Mzigo Mbebeshe Mnyamwezi"**

**MHE. JAMES P. MUSALIKA** aliuliza:-

Kwa kuwa upo usemi kwamba "Mzigo Mzito Mbebeshe Mnyamwezi"; na kwa kuwa usemi huo ni wa muda mrefu na umekuwa ukitumiwa na watu wengi hususan wa maeneo ya Pwani:-

(a) Je, ni nini maana ya usemi huo na ni lini na nani aliuanzisha na kwa malengo yapi?

(b) Je, kuna athari zozote zinazotokana na matumizi ya usemi huo kwa walengwa?

(c) Je, Serikali inasema nini kwa sehemu (a) na (b) ya swali hili?

**WAZIRI WA ELIMU NA UTAMADUNI** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, napenda kujibu swali la Mheshimiwa James Phillipo Musalika, Mbunge wa Nyang'hwale, lenye sehemu (a), (b) na (c) kama ifuatavyo:-

(a) Mheshimiwa Spika, maana ya usemi "Mzigo Mzito Mbebeshe Mnyamwezi au Mzigo Mzito Mpe Mnyamwezi ni kuwa jambo au kazi ngumu yoyote mpe mtu unayehisi kuwa ana uwezo au nguvu za kuifanya. Usemi huu ni wa siku nyingi lakini hautumiwi na watu wa Pwani peke yao. Chimbuko lake ni katika mapokeo ya utani na ulianza kutumiwa tangu enzi ya Mababu zetu na hakuna kumbukumbu ya lini usemi huu ulianza kutumika.

Hata hivyo, inaaminika kuwa usemi huu ulianza kutumika kabla ya huduma za usafiri wa kisasa wa njia ya Reli, Barabara na Ndege kutoka na kwenda Bara. Wakati huo makabila ya Bara (hasa Wanyamwezi) yalitumika kubeba mizigo na kutembea kwa miguu kutoka Bara hadi Pwani na kurudi. Katika safari hizo walibeba mizigo mbalimbali ya biashara. Baadhi yao walibaki Mwambao (kwa watani wao Wazaramo, Wadigo, Wazigua) kufanya kazi mbalimbali ikiwa ni pamoja na za kilimo. Inawezekana Mnyamwezi wa wakati huo aliona fahari kwamba anathaminiwa na watu wa Pwani kutokana na nguvu na uwezo alionao. Ndipo, ulipoibuka msemo "Mzigo Mzito Mpe Mnyamwezi". *(Makofi/Kicheko)*

(b) Mheshimiwa Spika, kwa msingi huo nilioueleza katika sehemu (a) ya swali, hakuna athari yoyote inayotokana na matumizi ya usemi huo kwa walengwa. Napenda nimfahamishe Mheshimiwa Mbunge kwamba, fasihi (nahau, methali, nyimbo, majigambo, ushairi, simulizi na kadhalika), ni mali ya jamii, huzaliwa, hulelewa na hutumiwa na jamii yote bila ya mipaka. Kwa hiyo, dhana ya "Mnyamwezi" ni kiwakilishi tu katika fasihi, ambayo inahusu jamii nzima.

(c) Mheshimiwa Spika, Serikali haina usemi wowote kuhusu vipengele (a) na (b) vya swali, hasa kwa kuzingatia kwamba, "Utani" ndio unaojenga na kuimarisha maisha ya jamii na kwa kweli huchangia kuleta amani na utulivu. Utani ni changamoto, hufariji katika sherehe na misiba. Aidha, napenda kumfahamisha Mheshimiwa Mbunge kuwa, makabila mengi ni watani kutokana na matukio fulani ya kihistoria baina yao na utani unachukua sura ya matukio haya. *(Makofi)*

**MHE. JAMES P. MUSALIKA:** Mheshimiwa Spika, nashukuru kwa kunipa nafasi niulize maswali mawili madogo ya nyongeza.

Kwa kuwa kwa upande wake Serikali nayo imekuwa ikitekeleza usemi huu kwa kisirisiri kwa kuwabebesha mizigo mizito wananchi wa Mwanza, Shinyanga, Tabora, Kigoma na Singida, kwa

kutowapelekea huduma za jamii kama vile umeme, barabara na maji, je, Serikali ni lini sasa itawatua hawa Wanyamwezi mizigo ambayo wamebeba kabla na baada ya uhuru. *(Makofi)*

Pili, je, Serikali inasema nini ikiwa wananchi wa maeneo mengine wangebeba kwa miaka kumi tu mizigo hii; wananchi wa mikoa ya Tanga, Arusha, Kilimanjaro na Dar es Salaam kungetokea nini? *(Makofi)*

**WAZIRI WA ELIMU NA UTAMADUNI:** Mheshimiwa Spika, napenda kumhakikishia kabisa kwamba, matendo ya Serikali hayana utani kwa sababu sasa hivi kwa mfano tunatekeleza elimu kwa wote. Kwa hiyo, tukisema elimu kwa wote ni pamoja na Wanyamwezi na Wasukuma.

Swali la pili kwamba je, wengine wangebeba mizigo wangepata athari gani inategemea uwezo. Mnyamwezi nasema aliaminika kwamba ana uwezo wa kubeba mizigo. Aliweza kufanya safari ndefu akiwa amebeba mizigo mizito, mchana, usiku amebeba mizigo kwa uwezo mkubwa, sasa ukiwapa wasio na uwezo wanaweza kuathirika, lazima twende kwa uwezo. *(Makofi)*

**SPIKA:** Natafuta watani wa Wanyamwezi.

**MHE. SEMINDU K. PAWA:** Mheshimiwa Spika, kwa kuwa suala la ubebaji wa mizigo kutoka mbali kwenda kwa miguu limeisha kutokana sayansi na teknolojia, sasa hivi kuna magari, ndege; na kwa kuwa utani huo bado unaendelea, kwa kuimarisha hivyo Serikali inaweza ikasema hakuna sasa zamu ya kuwapa wengine, kwa sababu suala hilo sasa limeisha, usafiri wa teknolojia upo na watu hawatembei kwa miguu, lakini utani uendelee? *(Makofi)*

**SPIKA:** Haya Mheshimiwa Waziri, naona una hamu ya kujibu.

**WAZIRI WA ELIMU NA UTAMADUNI:** Mheshimiwa Spika, labda katika kulijibu ili lieleweke jambo hili inafaa ieleweke kwamba, si utani wote uko katika msingi wa kubeba mzigo. Kwa mfano, utani wa Wahehe na Wanyamwezi ama utani wa Wahehe na Warangi, msingi wake sio kubeba mizigo ila ni kubebana kwa sababu historia yenyewe katika matukio ya kihistoria utani wa Wahehe na Wanyamwezi ulianza kutokana na mkataba wa ndoa uliofanywa na Mkwawa na Mtawala wa Wanyamwezi aliyeitwa Isike Mwanakiyungi. Waliamua waache kugombana baina yao watengeneze umoja, kwa hiyo, Isike Mwanakiyungi akamwoza Mkwawa binti yake kwa jina Gilagila. Kwa hiyo, ikawa ni mkataba wa ndoa. Kwa hiyo, utani wa Wahehe na Wanyamwezi una sura ya kubebana kuliko kubeba mizigo. *(Makofi/Kicheko)*

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo, ni muhimu kabisa kutafuta katika historia ndani ya mapokeo yetu chanzo cha utani ni tukio lipi basi utakuta na utani wenyewe utakuwa na sura hiyo.

Na. 9

**Vazi la Taifa**

**MHE. ISMAIL J. R. IWVATTA** aliuliza:-

Kwa kuwa mavazi ni kipengele kimojawapo kati ya vipengele vingi vinavyoelezea Utamaduni/Utaifa wa nchi husika:-

(a) Je, Tanzania inalo vazi la Taifa kwa ajili ya Watanzania wote?

(b) Kama vazi la aina hiyo lipo, je, ni lipi na limeanza kutumika lini?

(c ) Kama hakuna vazi la aina hiyo, je, isingefaa sasa Serikali ikabuni vazi la aina hiyo kama kielelezo cha Utamaduni/Utaifa wetu na likawa linatumika kwenye *Occasions* mbalimbali za Kitaifa na nje ya nchi?

**WAZIRI WA ELIMU NA UTAMADUNI** alijibu:-

Mheshimiwa Spika, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Ismail Iwvatta, Mbunge wa Manyoni Magharibi, lenye sehemu (a), (b) na (c) kwa pamoja kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, nchi yetu haijapata kuwa na Vazi la Taifa kwa wanaume au kwa wanawake. Ulikuwepo wakati ambapo vazi la kiume lijulikanalo kama *Nyerere Suit* au *Bunge Suit* lilitumiwa na Watanzania wengi kama utambulisho wao Kitaifa. Hiyo haikutokana na uamuzi wa chombo chochote cha Taifa, bali ilikuwa ni kumuiga mwanzilishi wa vazi hilo, Baba wa Taifa, Hayati Mwalimu Julius Kambarage Nyerere. Yeye alitumia vazi hilo kama vazi rasmi. Kwa upande wa wanawake, hakujapata kuibuka uvaaji wowote mahsusi wenye nguvu na mvuto kama ule wa *Nyerere Suit* kwa wanaume.

Mheshimiwa Spika, kwa kutambua kuwa kwa sasa hakuna vazi lililoteuliwa rasmi kuwa vazi la Taifa, Serikali imeanzisha mchakato wa kubuni na hatimaye kuteua vazi la Taifa kwa wanaume na wanawake. Kazi hii inawashirikisha wabunifu wa mavazi wa nchi nzima na utaendeshwa kwa utaratibu wa mashindano ngazi ya Mkoa na Taifa. Wizara yangu na Wizara ya Maendeleo ya Jamii, Jinsia na Watoto, zinasimamia zoezi hili kwa kushirikiana na Sekretarieti za Mikoa na Wadau wengine. Tumepanga kuikamilisha kazi hii kabla ya mwisho wa Juni, 2004.

**MHE. ISMAIL J. R. IWVATTA:** Mheshimiwa Spika, kwanza naomba nikushukuru kwa kunipatia nafasi ili niulize swali la nyongeza. Katika majibu ya Mheshimiwa Waziri anasema, Wizara yake ikishirikiana na Wizara ya Maendeleo ya Jamii, Jinsia na Watoto, wanalifanyia kazi suala hili. Kwa kuwa katika taarifa za baadhi ya magazeti inaonyesha kwamba kazi hii ambayo Mheshimiwa Waziri anafanya inaonekana kusuasua kutokana na mwitikio mdogo wa hao wabunifu kutoka katika Mikoa mingine, ni Mikoa michache tu ndiyo inayoonekana kwamba imeitikia.

(a) Je, Wizara yake imejaribu kuona tatizo la baadhi ya Mikoa ambayo ni mingi kutoitikia ni nini na kama imetafiti; je, wana mpango gani wa kutatua tatizo hilo?

(b) Je, isingekuwa vizuri basi Wizara au Serikali ikaangalia uwezekano wa kutoa motisha nzuri ili hao wabunifu waweze kujitokeza haraka?

**WAZIRI WA ELIMU NA UTAMADUNI:** Mheshimiwa Spika, napenda nikubaliane na Mheshimiwa Iwvatta kuwa, kwa taarifa tunazozipata ni kweli kwamba, kazi hii imeonyesha dalili ya kusuasua katika baadhi ya Mikoa na hii inatokana na viongozi wa maeneo hayo kutokulipa umuhimu jambo hili. Kwa hiyo, napenda kuchukua nafasi hii kutoa wito kwa viongozi wa Mikoa yote kuanzia ngazi za Wilaya na Mikoa, walipe uzito jambo hili ili tuweze kupata mashindano yaliyo mazuri. Ifahamike kwamba nchi yetu ni mjumuiko wa makabila yasiyopungua 120, tungependa kupata kitu ambacho kinachanganya sehemu zote. Kwa hiyo, kila Mkoa washiriki katika zoezi hili.

Wito wa pili napenda kuelekeza kwa Makampuni mbalimbali ya kibiashara. Mheshimiwa Iwvatta ametoa wazo zuri kwamba tuongeze motisha. Napenda kuchukua nafasi hii kutoa wito kwa Makampuni ya Kibiashara kwamba yajitokeze kusaidiana na Serikali kutoa motisha ili wajitokeze wasanii wengi kwani kinachoweza kuwavutia ni kupewa zawadi nono.

Kwa hiyo, naomba ushirikiano kati ya Makampuni na Mikoa ili mashindano haya ya kupata Vazi la Taifa yaweze kufanikiwa mapema iwezekanavyo.

Waheshimiwa Wabunge, naomba tusaidiane katika zoezi hili ili tuweze kufanikisha na tuweze kuwa na Vazi la Taifa. *(Makofi)*

Na. 10

**Mfuko wa Afya ya Jamii *(CHF)***

**MHE. DR. WILLBROD P. SLAA** aliuliza: -

Kwa kuwa Mfuko wa Afya ya Jamii *(CHF)* ni mkombozi kwa Wananchi wa kawaida wenye lengo la kutoa huduma ya afya kwa njia ya unafuu na uhakika; na kwa kuwa Wizara ya Afya kwa kutumia Wataalam wake imefanya kila jitihada kuingiza Wilaya ya Karatu kuwa miongoni mwa Wilaya chache zilizoshirikishwa kwenye mpango huo:-

(a) Je, Mfuko huo ulianza rasmi mwaka gani Wilayani Karatu na hadi sasa unao Wanachama wangapi na wamechangia jumla ya shilingi ngapi kwa kila mwaka?

(b) Je, Bodi ya Mfuko huo imeundwa katika ngazi zote kama sheria inavyotaka na umepata mafanikio yapi hadi sasa, yakitajwa kwa aina, idadi au kiasi na kama hakuna mafanikio yoyote; je, kuna matatizo yapi?

(c) Kama Mfuko umekumbwa na matatizo; je, matatizo hayo yamesababishwa na nini/nani na wahusika wamechukuliwa hatua gani za kinidhamu ili kunusuru Wananchi wengi wanaohitaji huduma za Mfuko huo na je, Serikali imechangia shilingi ngapi kwenye Mfuko huo hadi kufikia tarehe 31 Oktoba, 2003?

**NAIBU WAZIRI WA AFYA** alijibu: -

Mheshimiwa Spika, napenda kujibu swali na Mheshimiwa Dr. Willbrod P. Slaa, Mbunge wa Karatu, lenye sehemu (a), (b) na (c) kama ifuatavyo: -

(a) Mheshimiwa Spika, Mfuko wa Afya ya Jamii ulianza rasmi Wilayani Karatu tarehe 15 Machi, 2002. Hadi sasa kuna Wanachama 1,113. Mwaka 2002 walichangia kiasi cha Sh.11,020,000/=. Mwaka wa 2003 hadi hivi sasa wamechangia kiasi cha Sh.2,502,000/=. Jumla hadi sasa ni Sh.13,522,000/=.

(b) Mheshimiwa Spika, kilichotakiwa kuundwa ni Bodi ya Huduma za Afya ya Halmashauri *(Council Health Service Board)* na siyo Bodi ya Mfuko. Kazi mojawapo ya Bodi hiyo ni kusimamia uendeshaji wa Mfuko wa Afya ya Jamii Wilayani kama moja ya vyanzo vya fedha za kuendeshea huduma za afya na kushirikisha Wananchi Wilayani.

Bodi iliyoundwa Wilayani Karatu Oktoba, 2002 ilivunjwa kwa kuwa taratibu za uundaji wake zilikiukwa. Taratibu zilizokiukwa ni kama ifuatavyo:-

(i) Hakukuwepo mwakilishi toka Mashirika yasiyo ya Kiserikali;

(ii) Halmashauri haikutoa matangazo ya nafasi za Wajumbe wa Bodi na Kamati mbalimbali za Afya katika ngazi zote;

(iii) Baadhi ya Wajumbe wa Bodi walioteuliwa walikuwa na nyadhifa katika Vyama vya Siasa kinyume na mwongozo uliotolewa na Wizara yangu; na

(iv) Baadhi ya Wajumbe hawakuwa na elimu inayotakiwa yaani Elimu ya Sekondari kidato cha nne na kuendelea.

Mheshimiwa Spika, matatizo kadhaa yalijitokeza baada ya Bodi kuvunjwa ikiwa ni pamoja na haya yafuatayo: -

(i) Ucheleweshaji wa kuvilipa Vituo vya Huduma za Afya vinavyomilikiwa na Mashirika yasiyo ya Kiserikali. Hata hivyo, vituo hivi sasa vimeshalipwa jumla ya Sh.9,278,000/=; na

(ii) Kumekuwa na kasi ndogo ya wanaojiunga na Mfuko kutokana na uhamasishaji mdogo uliosababishwa na malumbano kati ya Madiwani na Watendaji hasa baada ya kuvunjwa kwa Bodi.

(c) Mheshimiwa Spika, ni kweli kwamba Mfuko umekumbwa na matatizo yaliyotokana na kukiukwa kwa mwongozo wa uanzishaji na uendelezaji wa Bodi za Huduma za Afya za Halmashauri kutokana na wahusika kutoelewa vizuri mwongozo huo.

Kwa sababu tatizo limetokana na uelewa mdogo wa wahusika, hakuna hatua za kinidhamu zilizochukuliwa, badala yake Wataalam wa Wizara yangu walikwenda Karatu mnamo tarehe 13 - 17 Januari, 2004 kwa madhumuni ya kuendesha mafunzo kuhusu taratibu za uundaji wa Bodi hiyo na uendeshaji wa Mfuko wa Afya ya Jamii. Hivi sasa maandalizi yamefanywa ili kuunda Bodi mpya. Ni matumaini ya Wizara kwamba Waheshimiwa Madiwani na Watendaji watashirikiana ili kufanikisha uendeshaji wa Mfuko huu kwa maslahi ya Wananchi wa Karatu.

Mheshimiwa Spika, hadi kufikia tarehe 31 Oktoba, 2003 Serikali Kuu ilikuwa imechangia jumla ya Sh.11,130,000/=.

**MHE. DR. WILLBROD P. SLAA:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi niulize maswali mawili madogo ya nyongeza.

Mheshimiwa Spika, awali naomba nimshukuru Mheshimiwa Waziri kwa majibu yake mazuri na ninaomba nishukuru kwa kuipongeza timu ya Wizara aliyoitaja kwa kufika Karatu na kufanya kazi nzuri vile vile.

(a) Kwa vile Waheshimiwa Madiwani pamoja na timu ya Wataalam ilizunguka Wilaya nzima na Wataalam ndiyo wanaotoa miongozo, kutokana na miongozo hiyo kama kweli Bodi ilikosea, Wananchi wameadhibiwa kwa kulipishwa Sh.1,000/= katika kila hospitali zile za papo kwa papo, lakini hawakupata huduma. Je, sasa tutarudisha imani kwa Wananchi namna gani kuhusu Mfuko huu ambao kimsingi ni makosa ya Watendaji?

(b) Kwa kuwa taarifa zilizopo zinazotolewa na Idara ya Afya zinaonyesha kwamba, kwa miaka miwili ambayo Mfuko umefanya kazi ni watu 3,075 tu kwa Wilaya nzima ndiyo waliotibiwa katika hospitali zetu na kwa kuwa kuanzia tarehe 15 Machi - 14 Aprili, 2003 katika kituo cha Karatu tu imeonyesha kwamba wagonjwa waliotibiwa walikuwa 3,200. Inaonekana kwamba, fedha zilizopotea ambazo hazikuidhinishwa ni zaidi ya Shilingi milioni 50 na watu wetu wanaonyesha kwamba fedha hizo hazitolewi risiti. Je, Serikali inachukua hatua gani ili kumdhibiti Afisa anayehusika na hujuma hiyo?

**NAIBU WAZIRI WA AFYA:** Mheshimiwa Spika, kama nilivyosema kwenye jibu la swali la msingi, ni kweli kwamba, imani kwa Wananchi inaweza kuwa imepungua kutokana na matatizo yaliyojitokeza. Lakini kama nilivyosema, kwa kuwa Wataalam wa Wizara ya Afya wameshafika katika Wilaya ya Karatu na wametoa mwongozo wa kuunda Bodi ambayo itakuwa imefuata mwongozo husika, bila shaka itakuwa ni wajibu wa Madiwani na Watendaji sasa kwenda katika Vijiji na kuhakikisha kwamba wanaeleza matatizo yaliyotokea ili kurudisha imani ya Wananchi hatimaye waendelee kuchangia Mfuko huu.

(b) Mheshimiwa Spika, Mheshimiwa Mbunge katika maelezo yake anasema kuna fedha zinazoonekana kwamba zimepotea. Wizara yangu haina taarifa hiyo, lakini nataka nimwombe Mheshimiwa Mbunge endapo ataweza kutusaidia maelezo kamili basi bila shaka Wizara itaweza kuchukua hatua. Lakini kabla ya kufika katika ngazi ya Wizara ndiyo maana kuna Bodi na ndiyo maana kuna Kamati ya Afya ya Halmashauri, tunataka suala hili lifikishwe huko na pengine wao wanaweza wakamaliza kwa kuchukua hatua. Endapo itashindikana hivyo, basi Wizara itakuwa tayari kupokea taarifa hizo.

**MHE. PROF. JUMANNE A. MAGHEMBE:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi ya kuuliza swali moja la nyongeza. Kwa kuwa Mfuko wa Afya ya Jamii ni utaratibu mzuri wa kuhakikisha kwamba Wananchi wetu wanapata huduma bora ya afya hapo baadaye, lakini unachukua muda kwa Wananchi kuelewa. Je; Serikali imeweka mkakati gani wa kuhakikisha kwamba wale ambao bado hawajajiunga na Mfuko wa Afya ya Jamii wanapata huduma ya afya?

**NAIBU WAZIRI WA AFYA:** Mheshimiwa Spika, mwongozo wa Mfuko wa Afya ya Jamii unaeleza bayana kabisa kwamba, Wananchi wote watakaojiunga na Mfuko huu watalipa mara moja kwa

mwaka kiwango kitakachokuwa kimepangwa na Halmashauri husika. Kuna baadhi ya Halmashauri wanachangia Sh.5,000/= tu kwa mwaka, kuna baadhi wanachangia Sh.10,000/= na wengine wamefika mpaka Sh.15,000/=. Madhumuni ya kuchangia zaidi ni kwamba ile tele kwa tele (kile kiwango kinachotolewa na Serikali Kuu) kiweze kuongezeka. Sasa, kuna utaratibu wa wazi kabisa uliopangwa kwamba endapo Wilaya itakuwa imeanza *Community Health Fund,* wale ambao watakuwa siyo Wanachama watalipa kila wanapokwenda kupata huduma za afya na kiwango hicho kinapangwa na Halmashauri husika. Kwa hiyo, kuna baadhi ya Halmashauri ambazo wameweka Sh.500/= mathalan kwa kila Zahanati au Kituo cha Afya. Kwa hiyo, hao watalipa kila wanapokwenda.

Ni jukumu letu kama Waheshimiwa Wabunge, kuhakikisha kwamba, tunawaelewesha Wananchi wachangie mara moja na hususan wakati ule wa mavuno kama ni Sh.5,000/= au Sh.10,000/= ili wasiweze kuchangia kila wanapokwenda kupata huduma za afya.

Na. 11

**Huduma Itolewayo na Wakunga wa Jadi**

**MHE. STEPHEN M. KAZI** aliuliza: -

Kwa kuwa Serikali inatambua wazi kwamba pamoja na huduma nzuri inayotolewa na Wakunga wa Jadi kwa akina mama wanaojifungua, bado inayo mapungufu hasa ya usalama na ubora wa huduma yenyewe. Je, Serikali kupitia Wizara ya Afya inayo malengo gani ya kuhakikisha kuwa huduma hiyo inatolewa kwa usalama na ubora kwenye Zahanati au Vituo vya Afya ili iendane na karne hii ya Sayansi na Teknolojia?

**NAIBU WAZIRI WA AFYA** alijibu: -

Mheshimiwa Spika, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Stephen Masaba Kazi, Mbunge wa Mwanza Mjini, kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Spika, ili kuboresha kiwango cha huduma za afya ya uzazi inayotolewa kwa akina mama, Wizara yangu inafanya yafuatayo: -

Kwanza, kutoa mafunzo ya rejea ya stadi muhimu za kuokoa maisha ya akina mama wakati wa uzazi *(Life Saving Skills)* kwa watoa huduma wa ngazi zote. Mafunzo haya yameanza na yamefanyika katika Mikoa ya Kagera, Tabora, Kigoma, Rukwa, Ruvuma, Singida na Shinyanga kwa msaada wa *UNFPA*. Aidha, Halmashauri zote zimehimizwa kuweka mafunzo haya katika mipango yao ili yaweze kugharamiwa na Halmashauri zenyewe.

Pili, vifaa muhimu vya huduma ya uzazi vimenunuliwa na kusambazwa kwenye Vituo vya Afya. Aidha, zoezi hili bado linaendelea kutegemea na upatikanaji wa fedha.

Tatu, ukarabati wa Vituo vya Afya unaendelea kufanyika ili kuboresha mazingira ya utolewaji wa huduma na hasa kuwa kivutio cha wanaohitaji huduma hizi.

Nne, kutoa mafunzo kwa wawezeshaji watatu kutoka kila Wilaya watakaosimamia Mkakati wa Ushirikishwaji Jamii katika Kuboresha Afya ya Wanawake katika Jamii *(Community Based Maternal Health Care)*. Aidha, Halmashauri zimeelekezwa kuweka mkakati huu katika mipango ya Halmashauri ili uweze kutekelezwa na uwe endelevu katika ngazi zote.

Tano, mafunzo kwa Wakunga wa Jadi yanaendelea kutolewa ili waboreshe kiwango cha huduma wanayotoa.

**MHE. STEPHEN M. KAZI:** Mheshimiwa Spika, nashukuru sana kwa kunipa nafasi ili niulize maswali mawili madogo ya nyongeza:-

(a) Pamoja na majibu mazuri ya Waziri napenda kufahamu kama Wizara inafahamu kiwango cha akina mama wanaojifungulia majumbani ni kiasi gani?

(b) Kufuatana na maendeleo na hali halisi tuliyonayo sasa hivi na ule ukweli kwamba tumefanya mpango kama wa MMEM na tumefanikiwa, hili tatizo la akina mama kujifungua kwa matatizo namna hii, Wizara ina mpango gani wa aina hiyo ili wote sasa waweze kupata nafasi ya kujifungua chini ya mikono ya Wizara ya Afya? *(Makofi)*

**NAIBU WAZIRI WA AFYA:** Mheshimiwa Spika, hatuna takwimu kamili za idadi ya akina mama wanaojifungulia majumbani, lakini tunafahamu kwamba kiwango ni kikubwa. Kuna sababu kadhaa zinazosababisha jambo hilo.

Kama nilivyosema katika jibu langu la msingi ni kwamba, Wizara imeanza mikakati ya kuboresha huduma zinazotolewa katika Zahanati na Vituo vyetu vya Afya ili kuwafanya akina mama waridhike kwenda kwenye vituo hivyo. Baadhi ya mikakati hiyo kama nilivyosema ni kwamba, ukarabati umeanza.

Huko nyuma kulikuwa kuna wakati ambao hali ya Vituo vya Afya ilikuwa hairidhishi, sasa hivi kwa maeneo mengi ukarabati umeanza ili kutoa mazingira mazuri kwa wale wanaokwenda kujifungua. Aidha, vifaa tiba vimeanza kusambazwa katika maeneo mengi ili akina mama hawa waweze kupata sehemu nzuri ya kujifungulia.

Kwa hiyo, ninakubaliana na Mheshimiwa Kazi kwamba, bado kuna akina mama wengi ambao wanajifungulia majumbani, lakini Wizara ya Afya kupitia mabadiliko katika Sekta ya Afya, inafanya juhudi ili kuboresha mazingira katika Vituo vyetu vya Afya hatimaye akina mama wengi waweze kujifungulia katika maeneo hayo. Vile vile, kulikuwa kuna tatizo la usafiri, kwa mfano, maeneo mengi hayana *ambulance* ya kuwapeleka akina mama katika Vituo vya Afya. Suala hilo nalo linafanyiwa kazi ili hatimaye usafiri wa kuwafikisha katika maeneo hayo upatikane.

Na. 12

**Usafi wa Barabara Kuu Nchini**

**MHE. PAUL P. KIMITI (k. n. y. MHE. MARIA D. WATONDOHA)** aliuliza: -

Kwa kuwa barabara kuu za nchi ziko chini ya Wizara ya Ujenzi na kwa kuwa nyasi zinazoota kando kando ya barabara hizo zinahitaji kufyekwa mara kwa mara ili kuzifanya barabara hizo ziwe safi kwa usalama wa raia na madreva wanaotumia barabara hizo:-

(a) Je, ni nani anayewajibika kuhakikisha kwamba nyasi kando kando ya barabara zinaondolewa?

(b) Je, Serikali inawajibika kufidia hasara kutokana na ajali zinazoweza kutokea kutokana na utoaji mkubwa wa nyasi unaozuia madreva kuona vizuri njia?

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI** alijibu: -

Mheshimiwa Spika, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Maria Watondoha, Mbunge wa Viti Maalum, lenye sehemu (a) na (b) kwa pamoja kama ifuatavyo: -

Mheshimiwa Spika, Wizara yangu kupitia Wakala wa Barabara *(TANROADS),* ina jukumu la kuhakikisha barabara kuu zote nchini zinafanyiwa matengenezo yanayotakiwa katika barabara hizo ikiwa ni pamoja na ufyekaji wa nyasi zinazoota katika maeneo ya barabara ili kuhakikisha usalama kwa watumiaji wake ikiwa ni pamoja na madreva na raia wengine.

Mheshimiwa Spika, Serikali kwa ujumla ina wajibu na imekuwa inatoa fidia kwa Wananchi kwa hasara zilizojitokeza na ambazo zimethibitika zilisababishwa na uzembe wa Watendaji wake. Hata hivyo, mpaka hivi leo matokeo ya tafiti mbalimbali za vyanzo vya ajali hapa nchini zimeonyesha kuwa ajali

nyingi zinatokea kutokana na matatizo ya kibinadamu (hasa ya madreva) kama kuendesha gari kwa mwendo wa kasi na kutoheshimu alama za barabarani na maelekezo ya matumizi ya barabara kama yanavyotolewa na vyombo husika.

Mheshimiwa Spika, hata hivyo, tokea kuanzishwa kwa Wakala wa Barabara *(TANROADS)* na kuboresha Mfuko wa Fedha za Barabara, *TANROADS* wamekuwa wakiingia mkataba na Bodi ya Mfuko wa Fedha za Barabara kila mwaka kuhakikisha matengenezo muhimu yakiwemo kufyeka nyasi, yanafanyika kwa wakati katika barabara zetu.

**MHE. PAUL P. KIMITI:** Mheshimiwa Spika, pamoja na majibu mazuri ya Mheshimiwa Naibu Waziri, nina swali moja la nyongeza.

Je, Serikali itakubaliana na ushauri ambao umekuwa ukitolewa mara kwa mara na Waheshimiwa Wabunge kwamba, ili kuhakikisha kuwa barabara kuu zote ambazo zinapita katika Vijiji mbalimbali vya nchi hii, Vijiji hivyo au Serikali za Vijiji vingepewa ukandarasi wa kufyeka nyasi katika maeneo hayo ili kupunguza gharama za watu kusafiri kutoka Makao Makuu ya Mikoa na kuja kufyeka barabara ambazo zinapita katika Vijiji hivyo na ingesaidia Vijiji kupata fedha za kusaidia miradi yao ya maendeleo? *(Makofi)*

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI:** Mheshimiwa Spika, Serikali ilikuwa na mpango huo na bado ina nia hiyo, lakini baada ya kupitisha Sheria ya Ununuzi ya Mwaka 2001 sasa yapo masharti, ni lazima yafuatwe kwenye sheria ile. Mantiki hiyo maana yake ni kwamba, lazima sasa vikundi vya akina mama ama Vijiji vijiandikishe kwenye Bodi ya Makandarasi na kwa maana hiyo vikundi hivyo ama Vijiji hivyo ni lazima viwe Kampuni.

Sasa hivi tunajaribu sana kuelimisha hasa akina mama kutoka katika Kitengo chetu cha Wanawake, Wizara ya Ujenzi, ili waweze kusaidia kufanya kazi hiyo huko waliko kwa kuwaelimisha kujiandikisha kama Kampuni ili waweze kujiandikisha kwenye Bodi za Makandarasi na wapate kazi hizo wao. *(Makofi)*

Na. 13

**Njia za Waenda kwa Miguu Kando Kando ya Barabara**

**MHE. SALOME J. MBATIA** aliuliza: -

Kwa kuwa watu wanaokwenda kwa miguu wanayo haki ya kutumia njia za waenda kwa miguu kando kando mwa barabara bila bughudha yoyote:-

(a) Je, kwa nini wenye majumba hasa ofisi kubwa za wageni hufunga kabisa njia hizo kiasi cha kuwalazimu wenye nchi kutembea barabarani jambo ambalo linahatarisha usalama wa maisha yao mfano majengo ya *European Union (Umoja House)* katika makutano ya Mirambo na *Garden Streets?*

(b) Kwa nini wageni hao ambao huko kwao sheria za barabarani zinaheshimiwa sana wanafanya vitendo hivyo bila ya Mamlaka zetu husika kuchukua hatua zozote?

(c) Je, ni lini tatizo hilo litaondolewa?

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI** alijibu: -

Mheshimiwa Spika, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Salome J. Mbatia, Mbunge wa Viti Maalum, lenye sehemu (a), (b) na (c) kama ifuatavyo: -

(a) Mheshimiwa Spika, nakubaliana na Mheshimiwa Mbunge kuwa, Wananchi wanayo haki ya kutumia njia za waenda kwa miguu kando kando ya barabara inayotumiwa na magari. Hivyo, kufunga njia hizo ni kuvunja Sheria za Barabara pamoja na zile zinazosimamia Miji, Jiji na Manispaa. Aidha,

imebainika kuwa wenye majumba hasa ofisi kubwa za wageni hufunga njia za waenda kwa miguu kwa sababu wanazoziita za kiusalama ikiwa ni pamoja na kuzuia uegeshaji ovyo wa magari katika sehemu hizo. Athari za kufanya hivyo ni kuwalazimu waenda kwa miguu kupita kwenye barabara inayotumiwa na magari, hivyo kusababisha hali inayohatarisha usalama wao. Eneo yalipo majengo ya *European Union (Umoja House)* katika makutano ya Mitaa ya Mirambo na *Garden* ni mojawapo ya maeneo yenye sura kama hiyo.

(b) Mheshimiwa Spika, sababu ya baadhi ya wageni hao kutofuata sheria za barabarani kama zilivyowekwa na Mamlaka zetu ni kukiuka kwa makusudi taratibu kama zilivyoainishwa kwenye Sheria ya Mipango Miji - Sura ya 378 zinazotaja wazi wazi kuwa sehemu ya ukanda wa barabara *(right of way)* ni mali ya umma *(Public Space)* inayomilikiwa na Halmashauri husika. Aidha, kutokana na historia kuwa udhibiti wa utaratibu wa Mamlaka mbalimbali zinazosimamia uendelezaji endelevu wa miundombinu Mijini haukutiliwa mkazo vya kutosha na jamii ya Miji haikuelimishwa ipasavyo, matokeo yake sasa uendelezaji wa ujenzi umekuwa ukifanywa bila kuzingatia Sheria kwa Wananchi na wageni. Vile vile, mabadiliko ya mara kwa mara ya Mamlaka katika uendeshaji wa Jiji la Dar es Salaam huko nyuma umechangia katika kutoa mianya inayoruhusu ukiukwaji wa kanuni na taratibu kwa mujibu wa Sura ya 101 ya Sheria ya Ujenzi Mijini.

(c) Mheshimiwa Spika, Halmashauri ya Manispaa ya Ilala ilifuatilia kwa wamiliki wa jengo hilo na kuwaagiza waondoshe uzio uliojengwa kinyume na taratibu za hifadhi za barabara Mijini. Wahusika walifanya marekebisho kama walivyoelekezwa. Aidha, hatua kama hizo zinaendelea kuchukuliwa katika sehemu mbalimbali. *(Makofi)*

**MHE. NJELU E. M. KASAKA:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi hii. Kwa kuwa inaonekana Miji yetu inajengwa kwa kweli bila kufuata sheria, lakini pia na matumizi ya hizo barabara hayazingatii sheria. Kwa mfano katika baadhi ya Miji na hasa Dar es Salaam magari huacha barabara na kwenda kuendeshwa kwenye *pavements* yaani kando kando ya barabara, kuwafuata raia ambao ni watembea kwa miguu walipo.

Je, Sheria zinasema nini na Serikali inatamka nini kuhusiana na utaratibu huu wa kuendesha nje ya barabara kuwafuata raia?

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI:** Mheshimiwa Spika, ni kweli kabisa kwamba, waendesha magari hasa daladala wanapenda sana kuvunja sheria hii kwa makusudi, lakini nawashukuru *Traffics* wanawadhibiti sana siku hizi, kila wanapofanya kitendo hicho wakiwepo Maaskari hawa wanawachukulia hatua. Tamko la Serikali liko wazi katika sheria linasema "Usivunje Sheria Makusudi Utachukuliwa Hatua."

Na. 14

**Uchakavu wa Majengo Mahakama za Mwanzo**

**MHE. HAMISI J. NGULI** aliuliza: -

Kwa kuwa majengo mengi ya Mahakama za Mwanzo ni ya zamani na mengine yamejengwa kabla ya kupata uhuru; na kwa kuwa hayafanyiwi ukarabati na Halmashauri husika au na Serikali; na kwa kuwa katika sehemu nyingine imelazimika Mahakama kuhamia na kupanga kwenye jengo la mtu binafsi hasa Mahakama ya Utemini iliyopo Singida Mjini kwa sababu ya uchakavu wa jengo la Mahakama hiyo: -

(a) Je, ni lini Serikali itakarabati au kujenga Mahakama hizo ili Wananchi waweze kupata haki katika majengo yenye hadhi na heshima ya Mahakama?

(b) Je, ni kiasi gani cha fedha kimelipwa hadi sasa kwa ajili ya kukodi jengo la mtu binafsi kuwa Mahakama ya Utemini Mjini Singida na ni nani anayelipa kodi hiyo?

(c) Je, isingekuwa busara kukarabati jengo la Mahakama ya Utemini Singida Mjini badala ya kuendelea kukodi jengo la mtu binafsi.

**WAZIRI WA SHERIA NA MAMBO YA KATIBA** alijibu: -

Mheshimiwa Spika, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Hamisi J. Nguli, Mbunge wa Singida Mjini, lenye vipengele (a), (b) na (c) kama ifuatavyo: -

(a) Katika kutambua tatizo hili la uchakavu wa majengo ya Mahakama, Serikali kupitia mpango wake mahsusi wa kuboresha huduma na miundombinu ya Idara ya Mahakama, imeanzisha mradi wa *quick start* ambao unashirikisha Serikali, Wahisani pamoja na Wananchi.

Mojawapo ya madhumuni ya mradi huo ni kujenga majengo mapya na kukarabati majengo yaliyopo ambayo ni chakavu. Kwa kuanzia, mradi huo unetekelezwa katika Mikoa ya Manyara na Arusha. Baada ya kutathmini mafanikio yake mradi huo utaendelezwa katika Mikoa mingineyo. Hivi sasa Mkandarasi anafanya tathmini ya majengo yote ya Mahakama nchini ili kubaini yapi yanatakiwa yakarabatiwe na yapi yajengwe upya.

(b) Shughuli za Mahakama ya Mwanzo Utemini - Singida zilikuwa zikifanywa kwenye jengo la mtu binafsi na Mahakama ililipa kodi ya Sh.720,000/= kwa kipindi hicho cha mwaka mmoja. Lakini kuanzia Mei, 2002 hadi leo, huduma za Mahakama za Mwanzo Utemini zinafanywa kwenye jengo linalomilikiwa na Ofisi ya Mkuu wa Mkoa wa Singida.

(c) Hali ya jengo la Mahakama ya Mwanzo Utemini ni mbaya na halifai kufanyiwa ukarabati, inapaswa kubomolewa na kujengwa upya.

**MHE. HAMISI J. NGULI:** Mheshimiwa Spika, nashukuru kwa kupata nafasi ya kuuliza swali la nyongeza.

Kwa kuwa kwa utawala wa sasa hivi Mahakama za Mwanzo hazipo moja kwa moja kwenye Halmashauri zetu kama ilivyokuwa zamani wakati wa ukoloni ambapo Mahakama hizi zilikuwa chini ya Watemi ambao ndiyo walikuwa watawala wa wakati huo na kwa hivyo walikuwa wanaweza kuzitunza na kuzifanyia matengenezo ya haraka.

Je, ni vipi sasa hivi Halmashauri hizi zinawajibika kutengeneza wakati ambapo Mahakama hizi hazipo moja kwa moja na wala hazipokei wala kupata fedha yoyote inayotokana na maduhuli ya Mahakama haya?

**WAZIRI WA SHERIA NA MAMBO YA KATIBA:** Mheshimiwa Spika, ni kweli katika miaka ya nyuma shughuli za Mahakama za Mwanzo zilikuwa zinahusisha Halmashauri zetu, lakini baada ya kupata uhuru masuala ya Mahakama yamewekwa pamoja *(Unified Post System)* kutokea Mahakama ya Mwanzo mpaka Mahakama ya Rufaa. Ushauri huo kusema tuzirudishe Mahakama za Mwanzo katika mfumo wa Halmashauri kule pia tuna matatizo makubwa ya kifedha.

Kwa hiyo, nadhani utaratibu tulionao kwamba hizi Mahakama za Mwanzo zishughulikiwe na mfumo wa Mahakama yenyewe ni mzuri zaidi.

Na. 15

**Bendera ya Serikali ya Zanzibar**

**MHE. MWADINI ABBAS JECHA** aliuliza: -

Kwa kuwa Tanzania ni nchi yenye mfumo wa Serikali mbili yaani Serikali ya Jamhuri ya Muungano na Serikali ya Mapinduzi Zanzibar; na kwa kuwa Katiba ya Jamhuri ya Muungano Ibara ya 102(1) inatambua kuwepo kwa Serikali ya Mapinduzi Zanzibar; na kwa kuwa Katiba ya Serikali ya

Mapinduzi Zanzibar inaruhusu kuwepo alama ya kuitambulisha Serikali hiyo, bendera ikiwa ni mojawapo ya alama muhimu; na kwa kuwa mpaka leo hii Serikali ya Mapinduzi Zanzibar haina bendera yake ambayo inajitambulisha kwayo: -

(a) Je, Serikali inaweza kutueleza kwamba ni tatizo gani linalokwamisha kuwepo kwa Bendera ya Serikali ya Zanzibar?

(b) Ikiwa jibu katika sehemu (a) ya swali hili ni hapana, je, ni utaratibu gani ufuatwe ili kuiwezesha Serikali ya Mapinduzi Zanzibar ili iwe na bendera yake ya Serikali itakayopepea katika majengo ya Taasisi zisizo na Muungano?

**WAZIRI WA SHERIA NA MAMBO YA KATIBA** alijibu: -

Mheshimiwa Spika, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Mwadini Abbas Jecha, Mbunge wa Utaani, lenye sehemu (a) na (b) kama ifuatavyo:-

(a) Napenda kumhakikishia Mheshimiwa Jecha kwamba, hakuna tatizo lolote la msingi linalokwamisha Zanzibar kuwa na bendera yake. Hali iliyokuwepo ni kwamba, wakati wa Muungano, pande zote mbili zilikubaliana kuwa na bendera moja tu ya Taifa, ili kujenga na kuimarisha dhana ya Utaifa.

Hata hivyo, baada ya muda mrefu wa Muungano, sasa ni dhahiri kwamba, Utaifa wa Tanzania umekwishajikita ndani ya mioyo ya Watanzania. Ndiyo sababu Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar, zimekuwa zikifanya mawasiliano kuhusu suala hili la Zanzibar kuwa na bendera yake na kuzingatia kuwa Zanzibar ina Serikali yake kamili.

(b) Kwa taarifa nilizonazo ni kwamba, Serikali ya Mapinduzi Zanzibar hivi sasa inalishughulikia suala hilo ili kukamilisha utekelezaji wa ibara ya Katiba ya Zanzibar inayohusu suala la kuwa na vielelezo vinavyotambulisha kuwepo kwa Serikali ya Zanzibar. *(Makofi)*

**MHE. NIMROD E. MKONO:** Mheshimiwa Spika, ahsante sana kwa kupewa nafasi hii. Pamoja na majibu mazuri aliyotoa Mheshimiwa Waziri mimi napenda kuuliza swali moja tu.

Je, wakati wa Muungano mwaka 1964, Bendera ya Zanzibar na Bendera ya Tanganyika wakati huo tulipoungana hazikufanyiwa mabadiliko kuonyesha kwamba Bendera ya Zanzibar pia inayo *place* kwenye bendera tuliyonayo leo na kwamba jambo la kuwa na bendera nyingine Zanzibar ni kukiuka utaratibu wa mwaka 1964? *(Makofi)*

**WAZIRI WA SHERIA NA MAMBO YA KATIBA:** Mheshimiwa Spika, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Nimrod Mkono, kama ifuatavyo:-

Baada ya Muungano Bendera ya Zanzibar kwa kweli iliendelea kupepeapepea, lakini baadaye ikafariki yenyewe. Lakini pamoja na hayo katika Katiba ya Zanzibar ya mwaka 1984 ibara 3(1) inasema kwamba, "Kutakuwa na Muhuri wa Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar ambao alama yake itakuwa kama itakavyokubaliwa na sheria itakayotungwa na Baraza la Wawakilishi. *(Makofi/Kicheko)*

Pili, Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar itakuwa na uwezo wa kuweka kitu chochote kitakachokuwa kielelezo cha Serikali kama ilivyokubaliwa na sheria iliyotungwa na Baraza la Wawakilishi. Kwa hiyo, jibu ndiyo hilo. Ninachosema tu ni kwamba, hebu tuwaachie wenzetu wa Zanzibar walishughulikie suala hili na baada ya hapo tutaweza kujadili. *(Makofi)*

**SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, muda wa maswali umekwisha kwa hiyo, tunaendelea na mambo mengine, lakini kabla hatujaendelea kuna matangazo yafuatayo: Mheshimiwa Waziri wa Maji na Maendeleo ya Mifugo, anaomba niwasomee tangazo lifuatalo kwamba saa 4.30 yaani sasa hivi baada ya maswali haya, Wizara yake itaweka saini Mkataba wa Ujenzi wa Awamu ya Kwanza ya ujenzi wa Kuta la Maji litakalotoa maji Ziwa Victoria kuelekea Miji ya Kahama na Shinyanga.

Kwa hiyo, Mheshimiwa Waziri anawaalika Wabunge wote wa Mikoa ya Ziwa na Nzega na Bukene, kushuhudia tukio hilo pale kwenye ofisi za Wizara yake, Wizara ya Maji na Maendeleo ya Mifugo. Ni mwaliko kwa Wabunge wanaotoka maeneo hayo ili kushuhudia tukio hilo. *(Makofi)*

Tangazo la pili ni la Mheshimiwa Joel Bendera, anawatangazia Wabunge wana michezo wote wakutane hapa saa 7.00 baada ya kumaliza shughuli za Bunge. *Agenda* ikiwa ni kujiandaa kwa mchezo wa mpira wa miguu dhidi ya Wabunge wa Bunge la Afrika Mashariki. *(Makofi)*

Tangazo la Tatu linatoka Redia Tanzania kwamba, kipindi kilichovurugika asubuhi hii kwa sababu za kiufundi kitatangazwa kuanzia saa 8.30 mchana na kuendelea. Lakini vile vile wanataka niwafahamishe Waheshimiwa Wabunge kwamba, kwa sababu wanatangaza mpira saa za jioni, kwa hiyo, kile kipindi ambacho huwa kinatoka saa 11.00 sasa kimehamia saa 8.30 hadi saa 10.00 jioni halafu wanaendelea na mpira. Lakini saa tatu kutoka Bungeni kitatangazwa kama kawaida. Hayo ni maelezo ya Redio Tanzania. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, la Mwisho, ni wagombea Ubunge wa Bunge la Afrika *(Pan African Parliament),* saa 10.00 jana jioni ndiyo ulikuwa mwisho wa kupokea majina ya wanaotaka kushiriki. Sasa *Returnig Officer,* Katibu wa Bunge, amepata majina yafuatayo kwa kila kundi la nafasi zilizopo kama tunavyofahamu kuna makundi 4. Sasa kwa kundi la wanawake wamejitokeza wagombea wawili Mheshimiwa Balozi Getrude Mongella na Mheshimiwa Dr. Aisha Kigoda.

Kwa kundi la Wabunge wa Tanzania Zanzibar, wamejitokeza wagombea 6 wafuataο: Mheshimiwa Balozi Ahmed Hassan Diria, Mheshimiwa Dr. Suleiman Juma Omar, Mheshimiwa Dr. Haji Mwita Haji, Mheshimiwa Remidius Kissassi, Mheshimiwa Kidawa Hamid Saleh na Mheshimiwa Omar Mjaka Ali. *(Makofi)*

Kwa kundi la Wabunge kutoka Kambi ya Upinzani wajimetokeza watatu wafuatao: Mheshimiwa Hamad Rashid Mohamed, Mheshimiwa Dr. Amani Kabourou na Mheshimiwa Benedicto Mutungirehi. *(Makofi)*

Kwa kundi la Wabunge kutoka Tanzania Bara wamejitokeza 7 wafuatao: Mheshimiwa Dr. Hassy Kitine, Mheshimiwa Dr. Makongoro Mahanga, Mheshimiwa Dr. William Kusila, Mheshimiwa Athumani Janguo, Mheshimiwa Dr. William Shija, Mheshimiwa George Francis Mlawa na Mheshimiwa Kilontsi Mporogomyi. Hao ndiyo wagombea wetu kura zitapigwa siku ya Ijumaa asubuhi mara baada ya kipindi cha maswali. Mwisho wa matangazo.

## HOJA ZA SERIKALI

## MAAZIMIO

### Azimio la Kuridhia Mkataba wa Kimataifa wa Stockholm wa Mwaka 2001 *(The Stockholm Convention on Persistent Organic Pollutants)*

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA MAKAMU WA RAIS (MHE. ARCADO D. NTAGAZWA):** Mheshimiwa Spika, kwanza kwa idhini yako na kupitia kwako, ningependa kuwatakia kwanza wewe mwenyewe binafsi na Waheshimiwa Wabunge wote...

**SPIKA:** Labda ungesubiri kidogo Mheshimiwa Waziri, kwanza tupate utulivu baada ya Waheshimiwa Wabunge wanaokwenda kunywa chai kuondoka unaweza kuendelea Mheshimiwa Waziri.

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA MAKAMU WA RAIS (MHE. ARCADO D. NTAGAZWA):** Ahsante Mheshimiwa Spika.

Nilianza kwa kusema kwa idhini na kupitia kwako Mheshimiwa Spika, niruhusu kwanza nikutakie wewe mwenyewe heri ya mwaka mpya pamoja na Waheshimiwa Wabunge wote, bila kuwasahau Maafisa

wanaofika hapa Bungeni, Wahudumu katika ukumbi huu na hata wana habari wanaosaidia kufikisha haya tunayosema kwa wananchi.

Mheshimiwa Spika, baada ya kusema hayo, naomba niseme kwamba, uchunguzi wa kisayansi uliofanywa na *UNEP* miaka ya tisini, ulibaini kuwa kiwango cha athari zitokanazo na kemikali hatari zinazochukua muda mrefu sana kuoza ni kikubwa na kinakua. Ili kukabiliana na hali hiyo, Baraza la Utendaji la Shirika la Umoja wa Mataifa linaloshughulikia masuala ya mazingira *(UNEP Governing Council),* lililipitisha uamuzi wa kuunda Mkataba wa Kimataifa dhidi ya kemikali kumi na mbili zilizoonekana kuwa na madhara makubwa zaidi. Majajdiliano ya kuunda Mkataba wa Kimataifa wa kudhibiti athari za kemikali hizi yalianza Juni, 1998 huko Mjini Montreal - Canada na yalikamilika Desemba, 2000 huko Johannesburg, Afrika ya Kusini. Tanzania ilishiriki kikamilifu katika kuandaa Mkataba huu. Wadau mbalimbali kama Wizara ya Afya, Wizara ya Kilimo na Chakula na Shirika lisilo la Kiserikali la *AGENDA* wameshirikishwa katika kutoa michango yao wakati wa majadiliano ya Mkataba huu.

Mheshimiwa Spika, Mkataba ulipitishwa na Kongamano la Kimataifa lililofanyika Mei, 2001 huko Stockholm, Sweden. Tanzania ni miongoni mwa nchi 92 za kwanza zilizotia saini Mkataba huu. Madhumuni ya Mkataba huu ni kulinda mazingira na afya ya binadamu dhidi ya athari zitokanazo na kemikali hatari zinazochukua muda mrefu sana kuoza. Kwa mujibu wa Ibara ya 25 na 26 ya Mkataba wa Stockholm, Mkataba huu ni lazima uridhiwe na nchi 50 ndipo utekelezaji wake uanze. Hadi sasa nchi 151 zimetia saini na nchi 40 zimeridhia Mkataba huu. Kati ya nchi zilizoridhia 9 ni za Afrika. Nchi hizo ni Misri, Ghana, Lesotho, Liberia, Mali, Rwanda, Senegal, Sierra Leone na Afrika Kusini.

Mheshimiwa Spika, Mkataba wa Stockholm umeorodhesha aina kumi na mbili za kemikali hatari zinazochukua muda mrefu sana kuoza. Kati ya kemikali hizo tisa zinatumika kuulia wadudu waharibifu *(pesticides),* ambazo ni *Aldrin, Chlordane, Dieldrin, DDT, Endrin, Heptachlor, Hexachlorobenzene, Mirex* na *Toxaphene*, kemikali 2 zinatumika viwandani *(Industrial Chemicals)* ambazo ni *Polychlorinated Biphenyls (PCB)* na *Hexachlorobenzene* na kemikali 2 zinajulikana kama *Dioxins* na *Furans,* ambazo hazitengenezwi kwa makusudi yoyote *(unintended by-products),* bali hutengenezwa pasipo kukusudia wakati wa uzalishaji mali viwandani hasa kama kuna malighafi zenye atomi za *chlorine* na pia kunapokuwa na uchomaji moto wa vitu vyenye aina hiyo ya atomi kwa kiasi cha nyuzi joto chini ya sentigredi 1600.

Hapa nchini kemikali/madawa ya kuulia wadudu waharibifu hutumika katika kilimo, kulinda afya, ujenzi, kuhifadhi mbao, usafirishaji na kadhalika. Kemikali za viwandani aina ya *Polychlorinated Biphenyls* hutumika katika *transformers* na *capacitors* katika shughuli za ugavi wa umeme. Kemikali zote hizi hazitengenezwi hapa nchi ila zinaagizwa kutoka nje.

Mheshimiwa Spika, kemikali zinazodhibitiwa na Mkataba wa Stockholm hudumu kwa muda mrefu, muda unaoweza kuzidi hata miaka 100 kwenye mazingira kwa vile haziozi kwa njia za kibaolojia au kikemikali. Aidha, zinayeyuka kwa kiwango kikubwa kwenye mafuta kuliko kwenye maji na hivyo hujilimbikiza katika miili ya binadamu na viumbe wengine kupitia mzunguko wa chakula. Kemikali hizi husafirishwa kwa njia ya maji na hewa kwa umbali mrefu na kuenea hadi sehemu ambazo kemikali hizo hazijawahi kutumika. Madhara yatokanayo na kemikali hizi kwa afya ya binadamu ni pamoja na saratani ya ngozi, saratani ya maini, saratani ya mapafu, saratani ya mifupa na upungufu wa uwezo wa mwili kujikinga na maradhi, madhara ya mishipa ya fahamu na matatizo ya uzazi. Aidha, kemikali hizi huathiri pia wanyamapori na viumbe wengine. Vile vile utafiti wa kisayansi umeonesha kuwa madhara ya kemikali za aina hii huathiri zaidi ya kizazi kimoja.

Mheshimiwa Spika, Mkataba wa Stockholm umeziruhusu nchi zinazohitaji kuendelea kutengeneza na kutumia kemikali aina ya *Chlordane, Mirex* na *Hexachlorobenzene* kuendelea kuzitumia katika matumizi maalum kwa muda hasa pale ambapo kemikali mbadala hazijapatikana. Utengenezaji wa kemikali aina ya *Aldrin, Dieldrin, Endrin, Heptachlor* na *Toxaphene* umepigwa marufuku japokuwa utumiaji wa kemikali hizi umeruhusiwa kwa muda kwa ajili ya matumizi maalum. Nchi zinazohitaji kuendelea kutumia kemikali hizo zitajiorodhesha kwenye kitabu maalum kinachotunzwa katika Ofisi ya Sekretarieti ya Mkataba ili matumizi hayo yaweze kudhibitiwa. Kemikali zinazotokea bila kukusudia kama

vile gesi za *Dioxins* na *Furans,* Mkataba unazitaka nchi wanachama kuondoa au kupunguza vyanzo vinavyoeneza kemikali hizi katika mazingira.

Mheshimiwa Spika, Mkataba umeruhusu kemikali aina ya *DDT* iendelee kutumika kwa muda kudhibiti wadudu waletao maradhi kwa binadamu hadi hapo njia mbadala ambazo ni rahisi na salama kwa afya ya binadamu na mazingira zitakapopatikana. Japokuwa tayari kemikali mbadala zipo, lakini baadhi zimeonekana hazifanyi kazi kwa ufanisi au zina gharama kubwa.

Kwa mfano, kemikali aina ya *pyrethroids* inayotumika kudhibiti mbu waenezao malaria ina ufanisi mkubwa, lakini ina tatizo la kusababisha mbu kuwa sugu haraka na ni ghali hivyo watu wengi katika nchi zinazoendelea kutoweza kuzimudu. Tanzania inalima zao la pareto ambalo ni mali ghafi ya kutengeneza *pyrethroids.* Hata hivyo, kutokana na ughali wa gharama na usugu wa *pyrethroids, DDT* itahitajika zaidi hapa nchini.

Mkataba unahimiza tafiti zifanyike ili kupata kemikali mbadala mapema iwezekanavyo. Mkataba unazitaka nchi ambazo zinaendelea kutengeneza na kutumia *DDT* kujiorodhesha kwenye kitabu maalum kitakachowekwa Ofisi ya Sekretarieti ya Mkataba kwa ajili ya ya udhibiti wa kemikali hii.

Mheshimiwa Spika, Mkataba umezuia utengenezaji wa kemikali aina ya *Polychlorinated Biphenyls.* Mkataba unazitaka nchi ambazo bado zinatumia vifaa vyenye *Polychlorinated Biphenyls* kama vile *transformers* na *capacitors* za umeme kuendelea kuvitumia na kuanza kupunguza taratibu matumizi haya hadi ifikapo mwaka 2025 ambapo utumiaji wake utasitishwa. Nchi nyingi zilizoendelea tayari zimepiga marufuku utengenezaji na utumiaji wa kemikali hii, lakini bado inatumika katika nchi nyingi zinazoendelea. Hapa nchini kiwanda cha *TANELEC* cha Mjini Arusha, ambacho hutengeneza vifaa aina ya *transformers* na *capacitors* kimeanza kutumia kemikali mbadala.

Mheshimiwa Spika, mkataba unazitaka nchi wanachama kuandaa mpango wa utekelezaji wa Mkataba huu. Mpango utawasilishwa kwenye mkutano wa nchi wanachama katika kipindi kisichopungua miaka miwili tangu Mkataba utakapoanza kutekelezwa.

Aidha, Mkataba unazitaka nchi zilizoendelea kuzisaidia nchi zinazoendelea ili kuweza kutekeleza majukumu yao ya Mkataba huu. Tayari Tanzania imepata msaada wa Dola za Kimarekani 500,000 kutoka Mfuko wa Dunia wa Mazingira *(Global Environmental Facilities),* kwa ajili ya kuandaa mpango wa kutekeleza Mkataba. Pia Tanzania imepata msaada wa Dola za Kimarekani milioni 9 kutoka kwa wafadhili mbalimbali kwa ajili ya kuondoa na kuteketeza kemikali na madawa yaliyokwisha muda wake ambayo nia kiasi cha tani 1,000.

Mheshimiwa Spika, kwa kuridhia Mkataba huu, Tanzania itanufaika kutokana na ushirikiano wa Kimataifa katika kusitisha/kupunguza matumizi ya kemikali hizi na hivyo kulinda afya ya binadamu na mazingira dhidi ya athari za kemikali hizi ambazo hazitambui mipaka ya nchi. Vile vile nchi yetu itanufaika kwa kujenga na kuimarisha uwezo wa taasisi husika katika kutekeleza Mkataba, kuweka mikakati ya pamoja katika kudhibiti madhara yatokanayo na kemikali hizi, kukuza weledi *(awareness)* kwa umma na kupata taarifa za kitaalamu, teknolojia mbadala na mafunzo ya kitaalamu katika kudhibiti madhara yatokanayo na kemikali hizi.

Mheshimiwa Spika, hapa nchini kuna sheria zinazosimamia kemikali na gesi mbalimbali zinazodhibitiwa na Mkataba wa Stockholm. Sheria hizo ni *Plant Protection Act No. 13 of 1997, Tropical Pesticides Research Institute Act No. 18 of 1979, Local Government Act No. 7 of 1982* na *The Industrial and Consumer Chemicals (Management and Control Act)* ya mwaka 2003. Iwapo hapana budi sheria hizi zitahuishwa ili zizingatie utekelezaji wa Mkataba huu.

Mheshimiwa Spika, Ofisi ya Makamu wa Rais kwa kushirikiana na Shirika la Umoja wa Mataifa linaloshughulikia Maendelea ya Viwanda *(UNIDO),* inatekeleza mradi wa miaka miwili wa kuandaa mpango wa Taifa wa kutekeleza Mkataba wa Stockholm. Shughuli kuu za mradi ni kukusanya taarifa za matumizi na usimamizi wa kemikali zinazodhibitiwa na Mkataba, kukuza weledi kwa umma na kuandaa mpango huo.

Matokeo ya ukusanyaji taarifa hizo yamethibitisha kuwa kemikali hizi zipo hapa nchini kwa mfano, madawa chakavu ya kilimo kiasi cha tani 179, mafuta ya mitambo tani 51,000 yenye kemikali aina ya *Polychlorinated Biphenyls* na vyanzo kadhaa vya kemikali aina ya *Dioxins* na *Furans.* Vyanzo vikuu ni uchomaji wa mafuta na taka *(burning of fossil fuel and biomass)* katika mitambo ya viwanda, mitambo ya kutengeneza umeme, vyombo vya usafirishaji na uchomaji wa taka nyinginezo za hospitali na taka maeneo ya mijini.

Wadau mbalimbali wanashirikishwa katika utekelezaji wa mradi huu. Wadau hao ni Idara za Serikali, Wakala na Mashirika ya Umma kutoka Serikali ya Muungano na Serikali ya Mapinduzi Zanzibar, Taasisi za Utafiti na Mafunzo, Mashirika yasiyokuwa ya Kiserikali na vyombo vya habari. Wadau hawa walishauri Tanzania iuridhie Mkataba huu kutokana na umuhimu wake.

Mheshimiwa Spika, kuhusu gharama Mkataba haujaonesha gharama ambazo nchi wanachama zinastahili kuchangia kwa ajili ya uendeshaji wa Mkataba huu. Mkutano wa kwanza wa nchi wanachama utakubaliana taratibu za kupata fedha. Inatarajiwa kwamba michango ya nchi wanachama itafuata viwango vya Kimataifa ambapo mchango wa nchi yetu ni chini ya asilimia 0.01 na kwa baadhi ya Mikataba ambayo nchi yetu ni mwanachama, nchi ambazo huchangia chini ya asilimia 0.01 huwa hazichangii kabisa.

Mheshimiwa Spika, baada ya maelezo haya ya utangulizi sasa nitapenda kusoma Azimio lenyewe kama ifuatavyo:-

KWA KUWA uchunguzi wa kisayansi uliofanywa na Shirika la Umoja wa Mataifa linaloshughulikia masuala ya mazingira *(UNEP)* miaka ya tisini ulibainisha kuwa kiwango cha athari zitokanazo na kemikali zinazochukua muda mrefu sana kuoza ni kikubwa na kinakua na kuongezeka;

NA KWA KUWA Baraza la Utendaji la *UNEP (UNEP Governing Council)* lilipitisha uamuzi wa kuunda Mkataba wa Kimataifa dhidi ya kemikali kumi na mbili zilizoonekana kuwa na madhara makubwa zaidi;

NA KWA KUWA mwaka 2001 Mkataba wa Kimataifa uliidhinishwa ili kudhibiti kemikali hizi ambazo kati ya hizo tisa zinatumika kuulia wadudu waharibifu, kemikali moja inatumika viwandani na kemikali mbili zinazotumika zinatokea katika uzalishaji mali yaani hazitengenezwi kwa makusudi yoyote bali hutokana na shughuli za uzalishaji mali viwandani na uchomaji wa vitu mbalimbali;

NA KWA KUWA Tanzania ni nchi mojawapo kati ya nchi 151 zilizotia saini Mkataba huu;

NA KWA KUWA hapa nchini kemikali zinazodhibitiwa na Mkataba huu hutumika katika kilimo, kulinda afya ya binadamu, ujenzi, kuhifadhi mbao na usafirishaji na kwenye mitambo ya ugavi wa umeme na nyingine hujitokeza bila kukusudiwa kutokana na shughuli za uzalishaji mali viwandani na uchomaji wa vitu mbalimbali kama vile mafuta ya mitambo na taka;

NA KWA KUWA madhara yatokanayo na kemikali hizi kwa afya ya binadamu ni pamoja na saratani ya ngozi, saratani ya maini, saratani ya mapafu, saratani ya mifupa na upungufu wa uwezo wa kujikinga na maradhi, madhara ya mishipa ya fahamu na matatizo ya uzazi;

NA KWA KUWA kemikali hizi huchukua muda mrefu kuoza, husafiri umbali mrefu kwa njia ya maji na hewa hadi sehemu ambazo hazijawahi kutengenezwa au kutumika na hujilimbikiza kwenye miiili ya binadamu na wanyama pori kupitia mzunguko wa chakula;

NA KWA KUWA Mkataba huu unazitaka nchi zilizoendelea kuzisaidia nchi zinazoendelea katika kutekeleza majukumu ya Mkataba huu;

NA KWA KUWA tayari Tanzania imepata msaada wa Dola za Kimarekani 500,000 kutoka Mfuko wa Dunia wa mazingira kwa ajili ya kuandaa mpango wa kutekeleza Mkataba huu na Dola za

Kimarekani milioni 9 kutoka kwa wafadhili mbalimbali kwa ajili ya kukusanya, kusafirisha na kutekeleza madawa chakavu ya kilimo nje ya nchi;

NA KWA KUWA utekelezaji wa Mkataba huu utakuza ushirikiano wa nchi wanachama katika kusitisha au kupunguza matumizi ya kemikali hizi na hivyo kulinda afya za binadamu na mazingira;

NA KWA KUWA nchi yetu itanufaika kutokana na kujenga na kuimarisha uwezo wa taasisi zote husika, katika kutekeleza Mkataba huu kuweka mikakati ya pamoja na kudhibiti madhara yatokanayo na kemikali hizi, kukuza weledi kwa umma na kupata taarifa za kitaalamu, teknolojia mbadala na mafunzo ya kitaalamu;

NA KWA KUWA kwa mujibu wa ibara ya 25 na 26 ya Mkataba wa Stockholm Mkataba huu lazima uridhiwe na nchi 50 ndipo utekelezaji uanze;

KWA HIYO BASI kwa mujibu wa ibara ya 63 (3) (e) ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ya Mwaka 1977, inayolipa Bunge madaraka ya kujadili na kuridhia Mikataba yote inayohusu Jamhuri ya Muungano na ambayo kwa masharti yake inahitaji kuridhiwa, hivyo basi Bunge hili katika mkutano wake wa kumi na tatu linaazimia kuridhia Mkataba wa Kimataifa wa Stockholm kuhusu udhibiti wa kemikali hatari zinazochukua muda mrefu sana kuoza ujulikanao kwa jina la *The Stockholm Convention on Persistent Organic Pollutants.*

Mheshimiwa Spika, naomba kutoa hoja.

**WAZIRI WA ARDHI NA MAENDELEO YA MAKAZI:** Mheshimiwa Spika, naafiki.

*(Hoja ilitolewa iamuliwe)*

**MHE. WILLIAM J. KUSILA (k.n.y. MHE. ANNE S. MAKINDA - MWENYEKITI WA KAMATI YA MALIASILI NA MAZINGIRA):** Mheshimiwa Spika, awali ya yote naomba kuchukua fursa hii kwa niaba ya Mwenyekiti na Wajumbe wa Kamati ya Maliasili na Mazingira kukushukuru kwa kunipa nafasi hii ili niweze kutoa maoni ya Kamati hii kuhusu Azimio la Kuridhia Mkataba wa Stockholm wa mwaka 2001 unaohusu udhibiti wa kemikali hatari zinazochukua muda mrefu sana kuoza, yaani *The Stockholm Convention on Persistent Organic Pollutants of the year 2001.*

Mheshimiwa Spika, naishukuru Serikali yetu kwa kuchukua uamuzi wa kuungana na Serikali za nchi nyingine katika kukubali kuridhia Mkataba huu wa Kimataifa kwani kwa kufanya hivyo tutaweza kuepukana na madhara mbalimbali yatokanayo na kukaa kwa muda mrefu madawa chakavu bila ya kuyateketeza. Kwa hiyo, ni vyema tuharakishe kuridhia Mkataba huu kwa manufaa ya nchi yetu na wananchi wake kwa ujumla.

Mheshimiwa Spika, kwa kuwa Tanzania ni moja ya nchi zinazoendelea ambazo zimekubalika zipewe msaada wa Dola za Marekani laki tano kwa ajili ya kuandaa mpango wa kutekeleza Mkataba huu wa Stockholm na pia kupewa Dola za Kimarekani milioni tisa kutoka wafadhili mbalimbali kwa ajili ya kukusanya na kuangamiza nje ya nchi madawa chakavu ya kilimo, Kamati inaishauri Serikali iendelee na hatua za awali za kutekeleza Mkataba huu wakati tunasubiri utekelezaji wake uanze rasmi. Aidha, tunaipongeza Ofisi ya Makamu wa Rais kwa kuandaa warsha mwaka jana ambayo ilizindua mradi wa miaka miwili wa kutayarisha mpango wa Taifa wa kutekeleza Mkataba huu. Warsha hii iliwashirikisha wataalam wa Sekta ya Mazingira, Nishati na Kilimo na vile vile wataalam kutoka Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar.

Mheshimiwa Spika, pamoja na maudhui ya Mkataba huu, tunaishauri Serikali kupiga marufuku uingizaji kutoka nchi za nje na utengenezaji wa mifuko ya *plastic* kwani madhara yake ni makubwa sana

kwa binadamu, wanyama, mimea na udongo kama yalivyo madawa chakavu na kemikali za aina mbalimbali.

Mheshimiwa Spika, kwa kuwa hakuna hata nchi moja Afrika yenye uwezo na mitambo ya kuteketeza kemikali na madawa chakavu, Kamati inaishauri Serikali kuweka mikakati ya kuwa na mitambo yake yenyewe badala ya kutegemea kupeleka taka Ulaya, kwani kwa kufanya hivyo tutakuwa tunaingia gharama kubwa sana kwa kusafirisha taka hizo ili zitateketezwe huko nchi za nje. Ni bora misaada ya wafadhili tunayoipata kwa wafadhili kwa ajili ya kuteketeza taka itumike kwa kununulia mitambo hiyo na kujenga viwanda vya kuchoma taka hizo hapa nchini. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, ili kudhibiti ubora wa madawa tunayopata kutoka nje kupitia misaada mbalimbali, ni muhimu tukawezeshwa kuwa na wataalam wetu ambao watakuwa wanakagua kila shehena ya madawa au kemikali zinazoingizwa nchini ili kwa kufanya hivyo tuweze kuepuka mlundikano wa madawa chakavu miaka ijayo ambayo yanaweza kusababisha madhara mengi kama alivyosema Mheshimiwa Waziri kwa afya ya binadamu ikiwa ni pamoja na magonjwa ya saratani ya ngozi, maini, mapavu, mifupa, upungufu wa uwezo wa kujikinga na maradhi na madhara ya mishipa ya fahamu na matatizo ya uzazi.

Aidha, elimu juu ya madhara ya mifuko ya *plastic* na madawa chakavu na vitu vingine vyenye madhara itolewe kwa wananchi ili kulinda afya zao. Kamati ilisikitishwa sana kwamba baadhi ya wananchi wanaitumia mifuko ya *plastic* kuwashia moto majumbani mwao kitendo ambacho kinaweza kusababisha athari kubwa sana kwa afya zao. *(Makofi)*

Hospitali kwa ujumla zinazalisha taka nyingi sana na za aina mbalimbali. Tunaishauri Serikali kupata ufumbuzi wa kudumu wa namna ya kuziteketeza taka hizo kwa vile kama zitaachwa kuzagaa ovyo, nazo zinaweza kusababisha madhara makubwa kwa afya ya binadamu.

Mheshimiwa Spika, mbolea na madawa ya kilimo yanayonunuliwa au kupatikana kwa msaada yaletwe kwa wakati na kuzingatia mahitaji halisi katika msimu husika, vinginevyo yatageuka kuwa sumu na kusababisha madhara makubwa.

Mheshimiwa Spika, mwisho, baada ya kusema hayo, nachukua fursa hii kuipongeza Ofisi ya Makamu wa Rais na hasa Waziri wa Nchi anayeshughulikia masuala ya mazingira Mheshimiwa Arcado Ntagazwa, wataalam wa Ofisi yake na Mwakilishi wa Mwanasheria Mkuu wa Serikali kwa kuwasilisha mbele ya Kamati ya Maliasili na Mazingira maelezo fasaha na ya kina kuhusu Mkataba huo. Wajumbe wa Kamati wameelewa vizuri faida zitakazotokana na utekelezaji wa Mkataba huu wa Stockholm na hivyo kuunga mkono na kuupitisha kwa kauli moja.

Pia naishukuru Ofisi ya Bunge, hususan Sekretarieti ya Kamati hii kwa kutupatia huduma mbalimbali zilizoiwezesha Kamati kukamilisha kazi yake kupitia Mkataba huu bila vikwazo vyovyote. Kwa ujumla sisi Wajumbe wa Kamati ya Maliasili na Mazingira, tunaomba Waheshimiwa Wabunge wenzetu wote kuuridhia Mkataba huu ili nchi yetu na wananchi wake kwa ujumla waweze kunufaika kutokana na matunda yatakayotokea baada ya utekelezaji wake.

Mheshimiwa Spika, naomba kuwasilisha. *(Makofi)*

**MHE. MHE. KARIM SAID OTHMAN (k.n.y. ALI SAID JUMA - MSEMAJI MKUU WA UPINZANI KWA OFISI YA MAKAMU WA RAIS (MAZINGIRA):** Mheshimiwa Spika, Kambi ya Upinzani inatoa pongezi kwa Mheshimiwa Waziri kwa kuleta Muswada huu ili kuridhiwa na Bunge hili kwani Tanzania ilikwishakubaliana na mambo yote yaliyomo kwenye Mkataba wenyewe.

Mheshimiwa Spika, ndani ya Mkataba huu kuna vipengele vingi ambavyo vinaangalia chanzo cha uzalishaji wa kemikali hizo hatari zinazochukua muda mrefu sana kuoza na zinaingia katika mzunguko mzima wa maisha ya binadamu kama vile uchafuzi wa udongo na baadhi ya kemikali hizo zinaathiri kuanzia kwenye mazao mpaka mtumiaji wa mwisho wa mazao hayo. Kemikali hizi huoza na kuwa sehemu

ya udongo ambapo mimea hutoa na kufyonza kemikali hizi na mazao ya mwisho huwa pia na kemikali hizo ambazo madhara yake ni makubwa kwa maisha ya binadamu.

Mheshimiwa Spika, Muswada huu unaelezea kuwa moja ya vyanzo vya hizi kemikali ni uchomaji wa wazi wa takataka, uunguaji wa mafuta ya mitambo, hivyo Kambi ya Upinzani inamwomba Mheshimiwa Waziri atafute njia mbadala ya kuteketeza taka hizo kwa wananchi wa kawaida. Sambamba na kuridhia Mkataba huu, elimu kuhusu madhara ya kemikali hizo ipelekwe kwa wananchi wa kawaida ili wafahamu madhara yake. Pia wapewe njia muafaka ya kuteketeza kemikali hizo ili zisilete madhara kwao. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, kemikali hatari aina ya *TBS,* mkusanyiko wake ni mkubwa chini ya mito midogo midogo. Maji ya mito hii hutumiwa na wafugaji na wakulima Mijini katika shughuli mbalimbali za kujiongezea kipato. Watumiaji wa maji hayo hutumia kwa umwagiliaji wa mbogamboga tunazokula kila siku ikiwa ni pamoja na matunda na mayai. Hivyo basi, kwa kuwa maji hayo yako *polluted* na madhara yake ni dhahiri, basi Wizara inayohusika na mazingira itafiti mito hiyo ambayo maji yake yamekuwa *polluted* na kuzuia matumizi ya maji hayo ili kulinda afya za wananchi wetu. Wale waliokuwa wakitumia maji hayo kwa shughuli za kawaida na za kiuchumi watafutiwe njia mbadala ya kupata maji kwa shughuli zao kama mfano kuwachimbia mabwawa, visima na kadhalika.

Mheshimiwa Spika, Sekta nzima ya Madini kwa wachimbaji wadogo wadogo wanaotegemea kutumia *mercury* katika kazi zao, hii kemikali ina matatizo makubwa kuanzia pale inapodondokea kama ni kwenye udongo au kwenye maji. Hivyo mzunguko unakwenda kupitia kwa wanyama mpaka nyama tunazokula.

Mheshimiwa Spika, suala hapa ni kwamba Mheshimiwa Waziri ni njia gani mbadala ameitayarisha kwa hawa watumiaji wakubwa wa kemikali hii? Kambi ya Upinzani inamshauri Mheshimiwa Waziri kushirikiana na Baraza la Mazingira *(NEMC)* kuona Maabara yenye ubora unaotakiwa ili aweze kugundua kutoka kwenye maeneo mengi yaliyotajwa kuwa ndio wazalishaji wakubwa wa hizo kemikali. Hii itaondoa udanganyifu na kuweka udhibiti. Sheria zitakazotungwa zitakuwa zinatoka kwenye hali halisi ya kwetu na sio kufuata viwango vya Kimataifa yaliyoendelea. Mfano, *Geita Gold Mine,* madawa ya kusafishia dhahabu pamoja na kwamba yametengewa mabwawa ya kutosha, bado madawa haya yanazama chini ya ardhi na kukutana na mtiririko wa kawaida wa maji ardhini na kuingia katika Ziwa Victoria. Madhara yake, maji na viumbe vyake vinaathirika. Leo hii hatuyaoni lakini baada ya muda mfupi, madhara hayo yataonekana kwa samaki na hata binadamu wanaotumia samaki na maji hayo. Hivyo wenye kuchimba dhahabu wapewe masharti kuwa mabwawa ya maji ya kusafishia dhahabu yapate *statement* sahihi ili yasije kuleta madhara ya Ziwa na viumbe vyake. Maabara yajengwe kwenye maeneo hayo ili kuwe na uchunguzi wa maji na udongo unaoathirika na kemikali hizo na kutoa taarifa kwa Serikali na watumiaji wengine mara kwa mara.

Mheshimiwa Spika, Kambi ya Upinzani inaunga mkono Azimio hili na kuliomba Bunge lako Tukufu kuridhia. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, naomba kuwasilisha. *(Makofi)*

**MHE. OMAR MJAKA ALI:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi hii ya kwanza na mimi kushiriki katika Azimio hili muhimu kwa Taifa letu na kwa wananchi wa Tanzania. Kwanza na mimi labda nifuate utaratibu nikupe kheri ya mwaka mpya pamoja na kwamba tulikutana Dar es Salaam. Nimpongeze Waziri, niipongeze Serikali, niwapongeze Mwenyekiti wa Kamati na Mwasilishaji kwa upande wa Upinzani. Nami nataka nitamke kwamba naunga mkono Azimio hili. *(Makofi)*

Mheshimiwa Spika, Azimio ambalo tunataka kulipitisha ni Azimio kubwa na muhimu kwa Taifa letu kwa sababu katika dunia hakuna kitu cha muhimu kama afya za wanadamu. Kwa kweli Azimio hili linalowasilishwa limejenga hofu kubwa sana kwamba sote miongoni mwetu maisha yetu yako hatarini. Kwa hiyo, labda nimtakie mafanikio Mheshimiwa Waziri, Serikali pamoja na wananchi kuweza kushiriki katika vita hivi vikubwa vya kuangalia uhai wa maisha yetu.

Mheshimiwa Spika, Azimio hili ni muhimu sana kwa Taifa letu na kwa wananchi wote wa Tanzania kama nilivyosema mwanzo na kwa kweli kuna maeneo ambayo ndiyo yaliyonishawishi na mimi kutoa mchango wangu kwa dhati juu ya suala hili zito kwa Taifa letu na nimtake Mheshimiwa Waziri kwamba tusipitishe tu, lakini kuwe na usimamizi mzuri ili kuondokana na hii hofu kwa sababu kama Azimio hili tulivyowasilishiwa na kama litafika kwa wananchi, kwa kweli litajenga hofu kubwa sana kwa wananchi. Sasa hivi katika gonjwa kubwa moja ambalo tunaambiwa halisikii dawa na ni hatari kwa maisha ya wananchi ni la Ukimwi na tukiangalia katika Azimio hili kuna maeneo katika hizi aina 12 za dawa hizi hatari na *infection* za matatizo yake ambayo yanatokea, tunaweza tukawarudishia watu wakaamini kumbe wengine madhara si Ukimwi. Wangeona hii *strong poison* ambayo inapatikana kwenye viwanda, katika mashamba ambayo wananchi wanakutana nayo kila siku, kwa kweli yatakuwa ndiyo yanawaathiri.

Mheshimiwa Spika, vile vile kilichonisimamisha hapa, Serikali na Wizara zote za Serikali zinazohusika zifanye utafiti juu ya Madaktari wetu ambao sasa hivi wanatibu wananchi wetu katika Taifa hili la Tanzania hasa wale wanaotibu maradhi ya Malaria. Kwa sababu ukiangalia katika eneo hili limeonyesha madhara makubwa ambayo ni muhimu sana ambayo matatizo hayo unayakuta kwa mtoto ambaye anapata matatizo ya tumbo, homa, Ukimwi, matatizo ya kifua na mambo mengine. Sasa kama katika mahospitali tutakuwa na Madaktari ambao watakuwa wanapokea wagonjwa wanaeleza matatizo yao kwamba mimi nimeanza kupoteza nguvu kwenye viungo vya mwili, akamwambia hiyo ni Malaria tu *positive four,* pengine kuna *infection* kubwa iliyotokana na sumu hii ya kemikali hizi. Kwa hiyo, vile vile mfumo mzima wa Wizara yetu ya Afya na Wizara nyingine ambayo inashughulika na jamii ifanye utafiti kwa kiasi gani tunaweza kupambana na majanga mazito katika Taifa letu kiasi hiki.

Mheshimiwa Spika, kwa kweli madhara yote haya yaliyotajwa humu katika Taifa letu yamo. Sasa hivi watu wengi wana matatizo ya vifua, wana matatizo ya viungo vya mwili, karibu yote haya. Tumeambiwa kwamba kuondoa hizi kemikali kwa kweli inahitajika teknolojia ya hali ya juu. Tulikuwa tunaongea hapa na Mwenyekiti wa Mazingira, Mheshimiwa anasema kwamba lazima ipatikane ile mashine ambayo itakuwa na nguvu kubwa sana. Kwa kweli kupata kiwanda hicho ambacho *temperature* yake itakuwa na *degree 200* ni kazi na mifuko mingi hii ya Rambo wananchi wa kawaida wanaichoma tu huko katika majalala ya kawaida. Kwa hiyo, hili ni suala la kuliangalia sana na si kwa wananchi wetu tu. Sasa sijui wenyewe tunamokaa, tunamotembea na kila sehemu.

Mheshimiwa Spika, tunapitisha Azimio hili ambalo ni la miaka ya 1990 na ambalo Azimio lake ni la mwaka 2001. Kwa hiyo, ningeishauri Serikali mara tu Azimio hili tunapoliunga mkono walifanyie kazi kwa haraka sana kwa sababu hizi kemikali hatuepukani nazo kwa sasa hivi kutokana na mfumo wa uchumi tuliobadilisha katika Taifa hili la Tanzania. Viwanda sasa hivi ni vingi, biashara huria - mifuko hii ni mingi na bahati mbaya sasa hivi inawezekana imetusaidia kwa sababu wakulima wengi sio wenye teknolojia ya hali ya juu, lakini huko mbele ya safari tunaamini kwamba tutawekeza wakulima wa Kimataifa ambao wataingiza zaidi kemikali kwa ajili ya mashamba yao. Kwa hiyo, vile vile kabla hatujakaribisha wale wakulima wakubwa wa Kimataifa, kuwe na mpango maalum wa Serikali wa namna gani ya kudhibiti hii.

Mheshimiwa Spika, nalisema hili kwa dhati kwa sababu kuna kiwanda hiki cha Mufindi, kuna kemikali pale na mpaka leo zimeshindwa hata kufanyiwa *process* za kuziondoa. Je, vikija kuongezeka viwanda vingine? Ikiwa kile kiwanda kimoja na vingine ambavyo hata hatuvijui wananchi wa Taifa hili wameanza kuwa na hofu, hata Serikali ilete bilioni ngapi kuhamisha ile kemikali iliyoko pale na ndio maana anatafutwa mwekezaji haraka sana ili aweze kuitumia ile kemikali. Kwa hiyo, pamoja na kuiwasilisha hii lakini lazima Serikali iweke mipango sahihi ambayo itaondoa hofu kwa umma.

Mheshimiwa Spika, maji yetu katika Taifa hili ni maji ambayo yanapita katika maeneo tofauti. Hivi karibuni mwishoni mwa mwezi uliopita Kamati yetu ya Ulinzi na Usalama tulikuwa ziarani Kagera. Tuliangalia hali ya maji inavyokwenda mle. Tuliona Ziwa Victoria pale, wavuvi waliomo na wengine wanatumia kemikali. Lakini tukiangalia Mto Kagera unavyosafiri kutoka eneo lile ambalo linapoanzia mpaka unapoingia na unakotokea, wengine wanatokea Rwanda na Burundi. Tuangalie vile vile zile athari za kemikali za zile nchi jirani ambazo tunapakana nazo na maji ya nchi zile yanaingia katika Taifa letu; Je, hakuna kemikali hizi? Tusiangalie vile vile kuziba hapa kwetu tu na hizi nchi jirani ambazo maji ya kwao bado yanaingia katika upande wetu. Hata tukiangalia hapa Rusumo tumeipita. Ule mto uliopita

pale unatokea vile vile Burundi. Kwa hiyo niitake Serikali utafiti isifanye ndani tu, lakini hata nchi jirani tunazopakana nazo ambazo vyanzo vyake vya maji vinaingia katika nchi yetu hii ya Tanzania ambavyo vinaweza kuleta athari kwa mifugo yetu na athari kwa wananchi wetu.

Mheshimiwa Spika, vile vile kuna baadhi ya mifugo ambayo inatokea Uganda, Rwanda na inawezekana ikawa kule kwao kemikali hizi ziko na ikawa imekunywa maji kule katika wakati ule inapopatiwa malisho. Lakini ukiangalia kule Kagera kuna mifugo mingi sana ambayo imeingia kutokea Uganda na Rwanda. Tunasema kama athari yake ni kubwa inachukua muda mrefu sana. Kuna ng'ombe pale zinauzwa, tuangalie afya za ng'ombe zile. Kilichotutisha ni kwamba hata zile ng'ombe za Ziwani zinazoingia mle wakati wanaporudishwa wale Wakimbizi hawaruhusiwi kuingia nazo ng'ombe zile ndani ya nchi yao. Zinauzwa huku huku ndani ya Tanzania au zinachukuliwa hatua nyingine yoyote. Kwa hiyo, kwa sababu zinaingilia mpaka kwenye masuala ya vyakula, kwa hiyo mifugo ni suala ningeiomba Serikali sana kulifanyia utafiti wa hali ya juu, tusiseme tu ili wananchi wajue kile tulichokipitisha hapa Bungeni, tulichokisimamia hapa Bungeni kinafanya kazi vizuri katika Taifa hili kwa faida ya wananchi wetu na kwa maisha yetu ya baadaye.

Mheshimiwa Spika, nilikuwa na hayo machache, nilitakie mafanikio Azimio hili na namwunga mkono Mheshimiwa Waziri na nalipitisha kwa asilimia mia kwa mia. Ahsante. *(Makofi)*

**MHE. SEMINDU K. PAWA:** Mheshimiwa Spika, nakupa kheri ya mwaka mpya pamoja na Waheshimiwa Wabunge wote na Watendaji wote pamoja na Waandishi wa Habari na wananchi kwa ujumla kuwapa kheri ya mwaka mpya mwaka 2004. Nimechelewa kutoa kheri ya mwaka mpya leo ni tarehe 03/02 lakini hata hivyo ninawapeni kheri ya mwaka mpya kwa sababu angalau mmeuonja na mkauona utamu wake. Tarehe ya papo kwa papo kutoa kheri ya mwaka mpya huwa ni nzuri zinaeleza bayana kuhusu pahima ya kujipa moyo katika nguvu yote. Lakini mara nyingi tunajiona kwamba sisi ni wateule wa Mungu, sio mabingwa wa wenzetu na kuwaombea waende mahali pema Peponi wasiouona mwaka huu.

Mheshimiwa Spika, baada ya kusema hayo Ofisi ya Makamu wa Rais imeleta mbele yako kitu ambacho kilikuwa kinahitajika sana na Watanzania ambao walikuwa wakikasirishwa na tabia ya nchi nyingi duniani ambazo zinaona bidhaa zao au kemikali za aina mbalimbali zinapokaribia kwisha muda wake, wakiona ni gharama kuziteketeza kwenye nchi yao, kuliko kwa bei rahisi kuzisafirisha katika nchi ambazo zinapenda kemikali hizo kutumika, basi hutoa kwa taratibu ya msaada au kwa bei nafuu. Kwa hiyo, nchi nyingi duniani kutoka Afghanistan mpaka Zimbabwe kwa kuzitaja zile ndogo zilizokumbwa na mfumo huo ni kwamba zilionja mtindo huu wa kupewa misaada kwa kupitia kilimo au upande wa kemikali, elimu, viwanda ambavyo tunasema kwamba bado tunaendelea kuvitumia. Zipo takwimu zilizotolewa na Wizara ya Kitengo cha Mazingira cha Ofisi ya Makamu wa Rais inayoonyesha idadi aliyoitaja Waziri ya maeneo mbalimbali na mahali yalipohifadhiwa. Azimio hili pamoja na kuliridhia litasimamisha haya, lakini baadaye tutahitaji sheria iletwe ambayo itakuwa na meno kwa Watanzania ili kuweza kuteketeza na kutekeleza wajibu wa hii.

Sasa katika hii inaendana na *International Standard* ya *WHO* ya mwaka 1998 ambapo vifaa hafifu au bidhaa hafifu na kemikali, *persistent organic* hatuzungumzii *inorganic* maana katika kemikali kuna *organic compound* na *inorganic. Organic* ndio hizi ambazo zinatokana na asili ya aina ya *Carbonize compounds* ambazo zina *carbon* tu ambazo haziungui, hazitozi wala chochote kwa utaratibu wa kuteketeza. Zipo *organic* ambazo zinaweza zikateketezwa kwa njia ya kemikali tu zikaondoka kwa utaratibu huo, lakini hizi imeshindikana kwa hilo. Sasa kinachoendelea nilitaka labda wataalam wake wangekuwa wananisaidia kidogo. Katika orodha ya hizi kemikali za *organic* nimekuta kwenye ukurasa wa 41 wametaja pale kuna, kwa mfano *motor vehicle contraction* sawa, lakini kwenye upande wa *textile,* sawa; lakini kuna *secondary copper production;* kuna *center plant of iron and steel industrial na secondary aluminum production* na *secondary production* ya *zinc.* Sasa hii *zinc* ni *metal,* sasa imeingiaje kwenye hii organic au kwenye persistent? Kwa sababu Muswada na Azimio linazungumzia *International* ya kuhusu mambo ya *organic persistent.* Sasa hivi *organic compound* kwa sababu ni *metallic* kama *zinc* na vitu vingine. Nadhani wanajua zaidi wao, watafafanua ili kusudi Watanzania wanaojua *chemistry* peke yake bila kujua *combination* ya *combustion* na vitu vingine wakaelimika vizuri ili wasije wakaviona hivyo.

Nyingine, napongeza Shirika lililotupa Watanzania fedha za kufanyia mambo ya uelewa. Sasa uelewa wenyewe kwa kweli uende kwa walengwa katika maeneo ambayo yatasaidia. Tusizigawe fedha hizi kwa ajili ya mgao tu. Kuna maeneo kadhaa ambayo wamejipanga kwa ajili ya masuala haya, nayo ni *National Environment Council, Tanzania Industrial Research Organisation, TIRDO,* watu kama wa *TBS* watatusaidia sana na maeneo mengine ambayo ni *reliable* kwa hayo na upande wa Zanzibar ambapo vile vile kwa sababu *pollutant,* nadhani mambo ya *environment* ni mambo ya Muungano. Sasa hivi kuna takataka zinaweza zikatupwa Tanzania Bara yakapelekwa kwa njia ya maji kwenda Zanzibar na wakaathirika wananchi wanaogelea kwenye bahari na kuharibiwa kwa ngozi zao.

Kwa upande wa wateketezaji nimepongeza kiwanda cha *Twiga Cement* kwa kazi nzuri waliyoifanya ya kuteketeza *day drill*, dawa ya nzige mwaka 1989 na mwaka 1992 ambayo nilikuwa kwenye Baraza la Mazingira, walijaribu kuziteketeza dawa za nzige, *the day drill* ambazo zilipitwa na wakati, zililetwa hapa nchini. Pia tunasikitika kwa tukio lile la *DDT (Dichloro Difinale)* ambazo zilimwagwa pale Vikuge kutoka Italy ambayo Italy yenyewe haikusaini kuridhia katika Mkataba ambapo wao wana viwanda lakini hawakuridhia. Wanaoridhia ni wale wanaopokea tu. Katika orodha ukiangalia *90 percent* ya watu ambao waliridhia ni nchi ambazo zinalalamika, ambazo zinaomba haki kwamba kutotupiwa matakataka katika nchi zao.

Lakini wale wenye viwanda vikubwa vya *industrial chemicals* zenyewe hasa wengine bado hawajaridhia. Kwa hiyo, ningeomba sasa dunia iweke kipaumbele kuwaambia nchi hizo zinazotengeneza kwanza, sio nchi zinazotumia. Kwa sababu *consumers* mara nyingi ni wanyonge ambao hawana uwezo wa kufanya hivyo, lakini wao walianza kutengeneza, baadaye wanatupa msaada wa kuteketeza. Hiyo ni biashara ambayo inaweza ikaleta athari katika nchi hizo. Pale mwanzo nilisema kwamba nchi nyingine zinafanya mahesabu kuona wana tani 1000 pengine za *DDT.* Kuteketeza wanatumia milioni 100 dola za Kimarekani. Sasa kuzisafirisha kupeleka nchi changa kama wakiomba pengine zina-*expire* muda wa miezi miwili tu ijayo wanaharakisha kuzisafirisha katika nchi hizo na kusafirisha wanatumia dola 50,000 tu. Sasa unakuta ni rahisi na biashara nzuri sana. Sasa tuwaambie kwamba mchezo wenu ni mauti kwetu.

Lengo ni kwamba Watanzania nadhani kwa hali hii sasa ni kutunga sheria ili kusudi kwa waagizaji, imeandikwa kabisa kwenye taarifa kwamba waagizaji kama watumiaji kwa mfano upande wa pareto na upande wa umeme wataagiza kemikali hizo zitumike kwa muda, wataomba kibali. Sasa tufuatilie kwa kina waagize kiasi ambacho kitatumika kwa muda mfupi halafu waagize tena. Wasiagize kiasi kikubwa kikazagaa kwa matumizi ambayo hayatumiki kwenye maeneo hayo. Wakifanya hivyo watakuwa wame-*pollute* nchi yetu. Hivyo hiyo kazi, changamoto kwa *NEMC,* Idara ya Mazingira, Wizara kwa ujumla ikishirikiana na Wizara nyingine na Sekta ya Mtambuko, *Cross Sectoral* ili kubainisha kufanya kazi hii pamoja ili kuweza kubainisha suala hili.

Mheshimiwa Spika, mchanganuo unasaidia lakini michanganuo mingine haisaidii. Kuna Padre mmoja aliambiwa alete mchanganuo ili apandishwe madaraka, kumbe somo la saikolojia sio somo la kuandika mambo ya kweli yaliyomo ndani ya kitabu kitakatifu. Aliambiwa andika michanganuo ifuatavyo:-

Mheshimiwa Spika, akaambiwa tutajie Miji miwili mikubwa kama wewe Padre mwenyewe unaijua; tutajie vitabu viwili vitakatifu; taja nyimbo mbili nzuri; taja nchi mbili unazozijua; mwisho wakamwambia andika matusi mawili makubwa. Ulikuwa mtego mkubwa kweli! Kwenye kitabu kitakatifu kama kile Padre huwa anaijua Miji akaandika Miji Mikuu akaandika Istanbul na Mji mwingine akaja akataja milima mikuu akataja Kilimanjaro akataja na Everist. Sasa kuna msamaria mwema akamwambia Padre huko mbele utatukana tu. Kwa sababu unakuja kwa mchanganuo, lazima matusi makubwa utayataja kwa hiyo acha hapo. Sasa utaratibu huu ni mzuri wa kuleta Muswada huu lakini kule mbele tuje tuangalie kwamba sheria zetu zinakidhi Muswada huu. Ahsante. Naunga mkono hoja hii. *(Makofi)*

**MHE. PAUL P. KIMITI:** Mheshimiwa Spika, na mimi nakushukuru kunipa nafasi ili na mimi nichangie Azimio hili ambalo ni muhimu kwa maendeleo ya watu wetu na Taifa kwa ujumla. Kabla ya yote napenda kusema wazi ya kwamba na mimi naliunga mkono mia kwa mia Azimio zuri sana hili. *(Makofi)*

Nataka niwashukuru wenzangu ambao wametangulia kuzungumzia kuanzia Mwenyekiti wa Kamati yetu ambaye anashughulikia na Maliasili na Mazingira. Lakini pia Ndugu Ali Juma ambaye kwa kweli Msemaji wa upande wa Upinzani. Napenda kumshukuru kwa sababu ameonyesha umahiri kuhusiana na suala hili ambalo ni athari komesha watu wetu na wasemaji wezangu waliotangulia wamezungumzia mambo ambayo na mimi nitayagusia kwa ufupi tu.

Ndugu Spika, nataka niseme machache yafuatayo. Kwanza Azimio hili limepitwa na wakati kidogo. Kwa sababu utafiti uliofanyika ni katika miaka ya themanini na tisini na tumechelewa zaidi ya miaka sasa kumi na mbili tangu Azimio hili ambalo lilitakiwa tumekwisha lipata lakini sasa ndiyo limetufikia. Nadhani tumechelewa na mapendekezo ya kemikali 12 ambazo walikuwa wameorodhesha. Nadhani kwa hivi sasa yatakuwa yameongezeka. Sasa suala zima ni vizuri kuangalia ni hayo hayo kumi na mbili au yapo mengine ambayo ni vizuri tukayazingatia.

Nasema hilo kwa sababu Mheshimiwa Spika, matumizi ya Kemikali kwa dunia ya leo ni katika jitihada ya kupambana na ongezeko la watu na mahitaji yake. Kemikali zote hizo zinafanyika kwa makusudi mengi. Lakini mimi nitazungumzia kwa nini kemikali upande wa mazao wa mimea zinatumika. Zimekuwa zikitumika kwa makusudi mazima ili uzalishaji wa mazao uweze kuongezeka haraka iwezekanavyo. Ndiyo maana kuanzia kilimo, kuanzia kutumia mbolea, kutumia dawa za kuua wadudu, kutumia dawa za kutunza mazao, zote ni kemikali hizo. Na ukianza kusindika mazao unatumia pia kemikali. Mafuta kuyafanya yawe meupe lazima utatumia kemikali. Ukitaka sukari iwe nyeupe utatumia kemikali na mlaji atakula kemikali, tutake tusitake. Hilo ni upande wa chakula. Lakini tunakwenda baya zaidi kwa mazao kwa mfano ya vyakula, chukua vyakula vya viwandani, hilo sitaki kulizungumza. Lakini tuzungumzie nyama, nyama ya ng’ombe, nyama ya kuku. Nyama ya kuku wote mnafahamu, wote mnaelewa hasa kuku wanaita wa kizungu, wa kisasa. Nyama yake haina ladha. Kwa sababu kemikali zimezidi katika nyama. *(Makofi)*

Lakini nyama pia za kizungu, ng’ombe wa kizungu wanatumia kemikali kubwa sana. Ndiyo maana hata magonjwa yameongezeka. Ukiangalia kichaa cha ng’ombe, ukiangalia kuku siku hizi wana mafua ambayo wanasababisha hata binadamu wanakufa. Yote ni makemikali ambayo wanapewa hawa wanyama ili kuweza uzalishaji. Lakiniu athari zake kwa watu wote mnafahamu. Vijana wetu mnawaona wanavyokuwa haraka. Wanakua haraka kuliko hata umri tunaowaona. Utaona vijana wengine wanaota hata maziwa, au matiti. Wakati mwingine wakina mama wanaota ndevu. Yote ni madawa yanayotokana na vyakula. Ni vizuri tukaliangalia suala hili wasizungumzie juu ya kemikali 12 tu tuzungumzie suala zima la kemikali ambalo linaweza kuleta athari kwa maendeleo ya afya zetu.

Upande wa mavazi. Wote tunaelewa ya kwamba mavazi karibuni yote tuliovaa hapa ni kemikali, waliovaa hapa pamba tunaweza kuwahesabu ni wachache, labda Mheshimiwa Spika nguo yake ile. Lakini wengine hapa ni kemikali tupu. Kwa sababu ni *petroleum products* zinaandaliwa kwa sababu ya kuweza kukidhi mahitaji ya watu katika ulimwengu huu. Pamba haitoshi. Hata pamba yenyewe ambayo tunazalisha bado inatumia kemikali kuizalisha. Bado athari zake tunaambiwa na wataalam ya kwamba katika nchi za joto athari za nguo za kemikali zina maisha mabaya kwa maisha ya binadamu kwa miaka 12, 13 na hii inatokana kwa sababu unapovaa nguo ambayo ina kemikali unatoka jasho. Jasho linaingia mwilini na likishaingia mwilini athari zake hutazipata siku hiyo hiyo, utakuja kuzipata baada ya muda mrefu.

Unasikia mtu anakohoa, huelewi anakohowa nini. Hizo ni athari. Lakini sitaki kuwakataza watu wasivae nguo. Lakini ni kwa uwangalifu mkubwa. Ndiyo maana unapoangalia nguo angalia kiasi gani kimewekwa cha cotton, pamba na kiasi gani kimewekwa kwa nguo ya kemikali. Wanaweza kusema pamba ni asili mia 40, 60 ni asilimia ya mazao ya petroleum wanakuambia hawakufichi. Sasa hiyo ni vizuri ukachagua. Unajua mazao ya pamba bei zake nguo yake ni kubwa sana kuliko hizi nyingine. Sasa nini athari nyingine ambazo tunazipata. Ni kwenye vifaa vya ujenzi. Zamani afadhali nashukuru, tulikuwa tunatumia mabati ya *asbestos.* Mabati ya *asbestos* ni mabati ambayo yanatokana na *products* za viwandani, viwanda vya petroli na ni hatari kwa afya. Naona baadhi ya nchi wamepiga marufuku mabati ya *asbestos* yasitumike kwa sababu yanaleta athari hasa katika nchi ambazo zina joto kali ya kwamba joto linapoingia pale linaathiri sana afya ya watu wanaokaa katika nyumba hiyo na baada ya muda mrefu ndiyo maana wanapata magonjwa mbalimbali yakiwepo kifua. Sasa ni vizuru tukazingatia ya kwamba ingawa azimio hili linakuja lakini kwetu sisi tuliangalia kwamba siyo azimio tu ambalo linashughulikia na hizi kemikali 12 lakini ni vizuri tukatumia baraza letu la mazingira kwenda kwa undani

kutambua baadhi ya kemikali ambazo sasa zinaanza kukubaliwa kuingia ndani ya nchi hii kama *DDT* ziendelee kutumika, basi tuangalie athari zake katika maisha ya binadamu kwa sababu usipofanya hivyo tutaingia katika mtindo ya kwamba tumeletewa ambayo hayastahili kutusaidia kutuletea mabadilika ya afya zetu.

Mwisho Mheshimiwa Spika, ningependa kuomba ya kwamba azimio hili liangaliwe katika upana wake. Na nimwombe Mheshimiwa Waziri afanye kazi kwa kushirikiana na wataalam ili sasa kemikali zote zinazokuja kuanzia mbolea, tuanze sasa kuangalia athari zake tufanye utafiti wa kutosha ili tujue kama kuna athari kiasi gani ili kuanza kutafuta kemikali mbadala ambazo zinaweza kutusaidia kupunguza matatizo ambayo tuna katika nchi yetu. Mimi nina imani kabisa tukianza kwa kushirikiana na wataalam mbalimbali ambao wapo katika vyuo vikuu tunaweza kufikia mahali Tanzania isiwe ni mahali pa kutupa kemikali ambazo ni chafu, kemikali ambazo hazitusaidii, lakini kemikali ambazo hazina athari kwa afya za watu wetu.

Baada ya kusema hayo, naunga mkono Azimo hili. Nina imani kabisa litatusaidia kufikia hatua ya kuweza kuleta maendeleo katika nchi yetu. Ahsante sana. *(Makofi)*

**MHE. DR. LUCY S. NKYA:** Mheshimiwa Spika, nashukuru sana kwa kunipa nafasi hii ya kuchangia katika Mkataba huu. Awali ya kwanza ningependa kuchukua nafasi hii kukutakia wewe kheri ya mwaka mpya pamoja na Waheshimiwa Wabunge wenzangu. Ningependa kusema kwamba tunamwomba Mwenyezi Mungu atupe afya njema pamoja na baraka nyingi kwa mwaka 2004 ili tuweze tukatekeleza majukumu yetu kwa wapiga kura wetu.

Ningependa pia kuchukua nafasi hii kumpongeza Ndugu Charles Makongoro kwa kuteuliwa na Mheshimiwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kuwa Mbunge mwenzetu. Namtakia afya njema na Mwenyezi Mungu amsaidie kufanya hii kazi ambayo amepewa kwa muda mfupi uliobakia.

Mheshimiwa Spika, ningependa kusema tu kwamba Mkataba huu umefika wakati muafaka ingawaje umechelewa tangu 2001, wakati ambapo sisi Watanzania tumeona na tumeendelea kupata madhara mengi yatokanayo na hizi pest side ambazo tunatumia.

Mheshimiwa Spika, ni jambo la faraja kuona ya kwamba Serikali sasa inaanza kujali afya zetu na afya za wananchi wake kwa kuhakikisha kwamba nao wanaungana na jamii ya ulimwengu kuthibiti madhara na matumizi yatokanayo na hizi *persistent organic pest side.*

Mheshimiwa Spika, ningependa kusema kwamba naunga mkono asilimia kwa mia azimio hili. Lakini ningependa kushauri Ofisi ya Makamu wa Rais yafuatayo ili tuweze kweli kufaidi na kuhakikisha kwamba azma ya hili azimio linatekelezeka kwa faida ya wananchi wetu ya kwanza ni kwamba pamoja na kuridhia mkataba huu, ningependa basi kuwepo na mipango mahususi ya kutoa elimu ya afya kwa umma inayoeleza vizuri kwamba ni kemikali gani ambazo zinatumika katika maeneo gani na madhara yake ni yepi.

Kwa sababu mpaka sasa hivi kuna maeneo wananchi wanatumia hizi kemikali bila kujua kwamba kuna madhara gani. Wanatumia pia hata kwa matumizi ambayo hayakukusudiwa. Kwa mfano, tukienda kwenye maeneo ambako wanapanda zao la kahawa pamoja na pamba. Zao la kahawa linaota Moshi, Mbeya pamoja na Mkoa wa Kagera. Zile dawa wanapokoroga na kuanza kuzitumia mashambani, unakuta kwamba wanakoroga kwenye maeneo ya mifereji na dawa inayomwagwa kule mferejeni unakuta wanakoroga zile dawa bila hata kuvaa gloves.

Wanaingia mashambani wana-spray bila hata kufunika pua zao na midomo yao na matokeo yake ni kwamba kwa sasa hivi kwa miaka hii matatizo ya kansa yamekithiri sana katika maeneo ya Mkoa wa Kilimanjaro, yamekithiri sana kule Kagera na yamekithiri sana kwenye maeneo mengine kama Mkoa wa Mbeya na sehemu za Mbinga ambako wananchi wanatumia hizi pesticide pamoja na maeneo ambayo wananchi wamepanda zao la pamba. Kuna matumizi makubwa sana ya pesticide. Jambo lingine ambalo ningependa tuchue tahadhari. Katika maeneo ambayo kuna mradi wa kuthibiti mbu hasa katika maeneo ya pwani. Matumizi ya *DDT* ni makubwa sana, lakini yale matumizi yake hayana *control.* Nasema hayana

control kwa sababu wale wana ambao tunaita kwamba ni *Mosquito Control Officers* wanadiriki kuwauzia walima mboga za majani kule Dar es Salaam na maeneo mengine haya madawa kusudi watumie wanapootesha zile mboga zao zisiliwe na wadudu.

Mheshimiwa Spika, mimi ningependa kushauri Serikali ilishauri Baraza la Mazingira kuhakikisha kwamba wanafanya utafiti wa hizi mboga katika haya maeneo. Wanafanya utafiti wa maziwa ya ng'ombe wanaolishwa na majani yanayotoka kwenye haya maeneo ili kuhakikiasha kwamba kuangalia kiwango cha *pollution* ya haya madawa katika hizi bidhaa mbili muhimu ni kiasi gani. Ili hatua mahususi ziweze zikachukuliwa.

Mheshimiwa Spika, nimefurahi kusikia kwamba sasa hivi vile *liquids* zinazotumika katika *transformer* zitabadilishwa. Au kutakuwepo na *liquid* mbadala au *pesticide.* Nasema *chemical* mbadala kwa sababu wasichana wetu wengi wameanza kutumia yale mafuta ya *transformer* wanatengeneza mkorogo kwa ajili ya urembo. Sijui kama Baraza la Mazingira linaelewa haya, hiyo ndiyo sababu kubwa sana ya kuibiwa mafuta ya *transformer,* wanatengenezea mkorogo. Sasa *you can imagine* wanaotumia mikorogo ni wasichana wadogo, hao ndiyo wasichana ambao wanazaa watoto na ile dawa ina-*concentrate* kwenye maziwa ya akina mama.

Mama atapata maradhi na mtoto atapata maradhi na tusishangae kwa nini watoto wadogo siku hizi wanapata lukinia, tusishangae kwa nini watoto wadogo siku hizi wanapata kansa na wasichana wadogo wadogo wanaanza kupata kansa nyingi za ngozi, kansa za maziwa, pamoja na kansa ya damu.

Tunasingizia kwamba kansa ya damu imeongezeka kwa sababu ya ukimwi. Ni kweli. Lakini hii mikorogo ambayo wasichana wetu wanatumia kutokana na *ignorance* ndiyo sababu nasema elimu kwa uma ni *very important* pamoja na kuridhia mkataba lakini basi ku-*sign is one thing* na kutekeleza kuhakikisha kwamba na sisi sasa tunakuwa *serious* kuhakikisha kwamba yale ambayo tunaona kwamba ni madhara kweli tunachukulia hatua zinazokubalika ambazo zitaweza zikazuia zile athari basi ninaomba hilo liangaliwe.

Mheshimiwa Spika, pamoja na kwamba tunasema kwamba hizi *DDT* zinasaidia kuua mbu, lakini nakumbuka ilikuwa ni mwaka juzi nilipita kwenye banda la Utafiti pale Nane Nane la *SUA* wakawa wamekuwa wametengeneza bidhaa nyingi tu ambazo zinaweza zikatumika kutokana na Mwarobaini katika kudhibiti hizi *pests* ambazo tunasema zinaharibu.

Kwa mfano, panya, mbu, Mwarobaini ukitengeza vizuri unadhibiti mbu, Mwarobaini ukitengenezwa vizuri hata bustani. Mimi naomba niseme kwamba bustanini mwangu ambako nalima mboga, sinunui dawa yoyote ya ku-*spray.* Ninatengeneza kutokana na majani ya mwarobaini. Nafikiri ni wakati muafaka kwamba tuangalie sasa huu mwarobani ambao unaota kila mahali katika nchi hii tunaweza tukautumia kwa namna gani ku-*control pests.*

Mwarobaini ukipandwa katika misitu yetu unadhibiti kukua kwa mbung'o. Mbung'o wanaozaliana mle wanakuwa sterilized mayai yake hayatoi tena watoto. Mimi *I don't see,* kwa nini kuanza kuchukua sasa mizigo kutoka kwa wenzetu kwa kisingizio kwamba *we need to use this you know, pesticide* kwa sababu tuna mbu au tuna mbung'o. Lakini mwarobaini upo. Hiyo ni teknolojia mbadala. *We need to be a bit serious,* tuangalie vitu ambavyo sisi tutavitumia havitatuletea maradhi.

Mheshimiwa Spika, kwa maeneo ambayo unakuta watu wanapata funza. Mimi natoa *experience,* nilipokuwa mtoto mdogo kule Moshi, wale watoto wenzetu walipokuwa wanapata funza unakuta kwamba wazazi wao wanachukua ile miguu wanaloweka kwenye *DDT* au ile dawa ya kahawa eti ni tiba ya kuondoa funza. Na kwa nini wanafanya vile. Wanafanya vile kwa sababu hawajui. Anaelewa kwamba kama hii dawa inatumika kuua wadudu kwenye kahawa *why not* kuua funza wanaoharibu miguu ya mtoto wao.

Mheshimiwa Spika, pia unakuta siku hizi dawa kwa kutibu magonjwa ya ngozi ambayo yamekuwa sugu, watu ambao wanakuwa na fangasi katika vidole vyao vya miguu au miguuni. Nasikitika kusema kwamba wanaambiwa eti wachukue ile dawa wanaotumia hawa, *you know, mosquito controllers,* wailoweke kwenye ndoo waloweke miguu yao mle ndani. Kwa nia njema tu wanatumia.

Mheshimiwa Spika, mimi na-*emphasize* kwenye kutoa elimu kwa uma lakini hiyo elimu ieleze madhara yake na kwamba kama kuna sababu ya kutotumia hizi *pesticide* basi zitumike kwa njia ile ambayo imekusudiwa. Kama ni ku-*strike* hawa na hawa wananchi wapewe elimu, mimi wala sijui *Extension Officers* ambao wanaishi kwenye hayo maeneo ambayo hizi dawa zinatumika kwa nini hawawapi watu elimu namna ya kukoroga ile dawa, namna ya ku-*spray* na namna ya ku-*disposal* zile ambazo zinabaki. *They don't it.* Lakini tunawalipa mishahara, tunawalipa mishahara kwa kodi inayotokana na mauzo ya kahawa na kodi inayotokana na huyu huyu ambaye anaumia kwa kutumia ile dawa ili azalishe alipe kodi.

Mheshimiwa Spika, mimi ningependa hilo tufanye ni *emphasize.* Lakini pia na utafiti. Hatuwezi tukasema kwamba tuna-*control,* na tukazungumza tu kwamba hizo mboga zinaweza zikawa na kiasi fulani *cha pollution, what is the level of pollution?* Tunaweza tukasema kwamba nyama ya ng'ombe wanaokula majani yanayotoka kule kwenye mashamba ya kahawa. Ng'ombe ambao wanalishwa na majani kule Dar es Salaam ambako tumesikia sisi kusudi tuue mbu hawa maziwa yake yana *pollution* kiasi gani. *What do we do tu-control that?* Nyama yake ina *pollution* kiasi gani? Hiyo ni *very important.*

Mheshimiwa Spika, baada ya kuzungumza hayo, mimi ningependa tu kusema kwamba ninaunga mkono hii hoja asilimia kwa mia. Ahsante.

**MHE. DR. SULEIMAN JUMA OMAR:** Mheshimiwa Spika, nakushukuru sana kunipa nafasi hii. Kwanza kheri ya mwaka mpya na pili ni kwamba nampongeza sana Mheshimiwa Makongoro kuwa Mbunge pamoja na sisi namtakia kheri katika kazi yake.

Kwanza niunge mkono hili azimio, kwa sababu ni azimio zuri ingawa kama wenzangu walivyosema kwamba limechelewa kidogo lakini hata hivyo limeletwa. Kwa hiyo, lazima tuliinge mkono.

Mheshimiwa Spika, kwanza ni kwamba mimi nakwenda kwa ufupi tu, Kwanza hapa kwetu kama walivyosema wenzangu kwamba ile mifuko ya plastiki hasa ile laini inatumika sana. Kwa kweli Zanzibar sisi nadhani kama miaka mitatu au minne nyuma tumeshapiga marufuku na Serikali iliikusanya yote. Ilikuwa kwenye *stock* na mimi nikainunua na hivi sasa haipo kabisa. Kwa hivyo hili nadhani suala hili na huku lingeweza kufanyika kwamba ile mifuko yote isitumike na ambayo iko kwenye *stock* bado haijapelekwa madukani ingenunuliwa ili isiweze kutumika kabisa kabisa. Kwa hiyo, nadhani hiyo kwanza ingeweza kusaidia kupunguza athari hiyo.

Mheshimiwa Spika, pili ni dawa za kuulia wadudu. Ni kweli kuna dawa ambazo kwa kweli hazistahili kutumiwa kama *DDT* ulivyosema, ingawa imeruhusiwa kidogo. Lakini Zanzibar zamani kulikuwa na mradi wa malaria na ikitumika sana hii *DDT* ikitumika ku-*spray* vichakani, kwenye maji majumbani. Baada ya mradi huu kumalizika kwa muda mrefu kidogo sisi watu wa kilimo tulikuwa tuna kokoa tulikuwa tunapeleka Uingereza na tulikuwa tunaianika chini kwenye majamvi lakini chini.

Hata hivyo Uingereza walituambia kwamba nyinyi kakao yenu inaonekana ina athari ndani kuna *element* ya *DDT* na *imegine* kwamba baada ya mradi kumalizika inafikia kama miaka 8, 10 au 12 lakini bado tulipoanika kakao kwenye majamvi, ilionyesha athari ya *DDT.*

Sasa unaweza kuona kwamba kiasi gani *DDT* inaweza kuwa *persistence* katika ardhi mpaka kuonyesha kwamba katika kakao pia imeleta athari ya *DDT.* Kwa hiyo, mimi nahisi kwamba *DDT* hata kama imeruhusiwa kidogo lakini athari yake ni ndefu sana na inafaa kabisa isitumike.

Mheshimiwa Spika, lingine ningeshauri kwamba dawa zinazoagiziwa, ziagizwe kwa wakati na kwa kiwango ambacho kitaweza kutumika na kikamalizika na pia makopo yanayoletwa au matanki yanayoletewa yasiwe na *likage*, yawe hayavuji na wale watu wanaotumia dawa hizi kwa ku-*spray* ni kwamba lazima wawe na *gloves* na pia zile za kuzibia puani kama alivyosema Dr. Nkya hapa. Mara nyingi kuna dawa ambazo zinakuwa *sprayed* kwa ndege zile zikiwa *sprayed* zinakuwa zinakumbwa kidogo na upepo, watu ambao wako nje au majumbani wanaweza kuvuta hewa ambayo ina dawa zile.

Nadhani Wizara *in collaboration* na Wizara ya Kilimo na Chakula na pengine Wizara ya Afya, wangeweza kutafuta *modalities* kwamba wafanya nini ili *drift* hii dawa inayo-*be sprayed* kwa ndege

isiweze kuleta athari kwa wananchi kwa sababu zinakuwa *accumulated,* leo wananusa zinakuwa mwilini na mwaka mwingine vile vile zinaingia zinakuwa zimekusanyika baadaye zinaleta athari kwa afya ya wananchi. Kwa hiyo, nadhani pale lazima Wizara iangalie pamoja na Wizara ya Kilimo na Chakula, Wizara ya Afya waweze kutafuta *modalities* za nini wafanye ili isilete athari kwa wananchi.

Mheshimiwa Spika, lingine ni kwamba tuna vitu vya plastiki ambazo tunavitupa katika majaa na vile vile hata hizi betri ndogo za redio hizi zinatupwa. Sasa nchi nyingine vitu kama vile vinatupwa katika mifuko mbalimbali, ni betri hizi ndogo ndogo zilizokwisha hazitupwi ardhini, zinatiwa kwenye mfuko, pengine mifuko mingine *glasses,* nyingine vitu vya plastiki zinawekwa mbali ili wale wachukua takataka wanaochukua vile wanavichukua mbali na taka za kawaida wanavichukua mbali. Vile ina maana kwamba hawataki zile kemikali ziingie kwenye ardhi, wanakwenda kuzifanyia *process* zao katika viwanda mbalimbali ili zisiingie kwenye ardhi.

Nadhani sisi ni mfano nzuri wa kuiga kwamba dawa za betri hizi labda tuwajulishe wananchi wetu kwamba wasizitupe na kwenye ardhi zikipata maji kemikali hizo zinakwenda mpaka kwenye visima vya maji na watu wakinywa maji yale wanapata magonjwa ya kansa na kadhalika kwa hiyo utupaji wa vitu kama hivyo, nao lazima tuwaelimishe wananchi wetu watupe kwa uangalifu na *collection* yake iwe mbali ili ziwe tofauti na takataka zingine.

Mheshimiwa Spika, viwanda vinavyotoa maji au maji ya kemikali zinazokwenda kwenye mito au baharini. Ni kwamba nilipokuwa Japan ilikuwa wakati kwamba samaki wa Japan wote na ndio maana meli za Japan zinakuja kuvua katika bahari zetu za Afya kwa sababu bahari yao imekuwa *polluted* na maji ambayo yanatoka viwandani ambayo ni maji yenye kemikali. Kwa kweli samaki wa Japan wanakuwa hawaliwi kwa sababu ndani walijaa *mercury* na *it is true* tumejaribu kuangalia samaki ni kweli wana *mercury* ndani.

Kwa hivyo ilikuwa Wajapan wanakuja kuvua huku kwa sababu bahari yao yote imekuwa *polluted* kwa maji ya viwandani. Sasa baadaye wakaanza kufanya mpango kwamba viwanda vyote lazima vijenge mitambo ya kusafisha maji yale ili maji yanayokwenda baharini yanayotelemka yawe *clean* yaani *chemicals* zote ziwe *expected* katika maji yale machafu ili bahari ipate kuwa safi. Nadhani na sisi tungeweza kwa mfumo huo kama viwanda vyote sasa vijenge viwanda vidogo vya kusafisha maji yale ambayo yana kemikali yakienda kwenye mto au bahari yale maji yako clean. Nadhani hiyo ingeweza kutusaidia zaidi.

Mheshimiwa Spika, ni kwamba juzi juzi nadhani kulikuwa na mgongano mrefu baina ya Marekani na Uingereza. Marekani wameleta meli ambayo yenye kemikali ambayo hawawezi ku-*process* kuangamiza na walete Marekani ili ziangamizwe pale Uingereza. Lakini Waingereza wakaona na wao watu hawataki kabisa meli zile zisiruhusiwe kabisa. Sijui ugomvi ule ulikwisha vipi. Lakini sasa nataka kusema kwamba kuna baadhi ya meli za nje zinakuja kwenye bahari yetu na wakatupa kemikali hizo. Sasa sijui Wizara inaweza kufanya mpango gani ili kuzuia meli hizo zinazokuja kwenye bahari yetu na kutupa kemikali hizo, jambo hilo linafanyika kwenye nchi nyingi za Ulaya zinatupa kemikali hizo baharini ambazo huleta athari kwenye bahari, samaki na watu wetu. Hilo nataka lichukuliwe hatua.

Vyakula vya kwenye vibati kama alivyosema Mheshimiwa Kimiti. Ni kweli kuna vingine vinaleta athari kutokana na kemikali zake na kwa muda ambao zinakaa nalo liangaliwe vizuri, moshi wa magari na kadhalika. Magari mengine hutoa moshi, petroli au dizeli hutoa moshi na watu wanavuta tu, na hivyo lazima kuwe na sheria, gari ambazo hutoa moshi lazima ziwekewe sheria kwamba gari kama ile izuiliwe au ipigwe faini.

Lakini watu wanaathirika tu, kwa hilo nalo litazamwe na la mwisho ninaomba niseme kwamba kuwe na *collaboration* na Wizara ya Kilimo na Chakula ni kwamba kuna baadhi ya wakulima wanapiga dawa mazao kwa mfano mboga au matunda na inavyotakiwa *at least* wa-*spray* wiki mbili au zaidi kabla ya uvunaji wa matunda yale au mboga mboga zile lakini chini ya hapo inakuwa ile dawa inabaki kwenye mboga mboga na inaliwa.

Kwa hivyo, nadhani nayo hii kama nilivyosema, ushirikiano wa Wizara ya Kilimo na Chakula waweze kuambiwa wakulima waweze kufundishwa na vile vile watu wanaonunua mboga mboga, vitunguu, watie kwenye ndoo ya maji mboga zao *at least* kwa *few hours* ili ile *cabbage* ipate maji iweze ku-*dilute* ile dawa kama imebakia. Nadhani watu pia wafundishwe suala hili.

Kwa hayo machache Mheshimiwa Spika, mimi nasema tena naunga mkono hoja na nakushukuru sana kwa kunipa nafasi. Ahsante sana. *(Makofi)*

**MHE. JACKSON M. MAKWETTA:** Mheshimiwa Spika, nimesimama kwanza kabisa kukutakia kheri kwa mwaka mpya na pili kuunga mkono Azimio hili la kudhibiti kemikali. Tatu, ningependa kumpongeza Ndugu Makongoro Nyerere kwa kuteuliwa kwake kuwa Mbunge wa Bunge letu Tukufu na kumwomba sisi wenzake tunamtazama Hayati Nyerere kupitia yeye. Kwa hiyo, atunze heshima hii.

Baada ya utangulizi huo ningependa kusema Mheshimiwa Spika kwamba adui mkubwa wa mazingira ya binadamu ni binadamu mwenyewe. Kwa lengo la kutaka ajiendeleze au ajihami na njaa au na matatizo ya kimaendeleo anajikuta anajiharibu mwenyewe. Kwa hiyo, malipo ya maendeleo yetu ni kujitahadhari wakati wote. Kwa sababu kwa wapenzi wa mazingira kila kitendo cha kimaendeleo kwa upande mmoja ni kitendo cha kuharibu mazingira. Na kwa aina fulani ya watu ili usiharibu mazingira basi ungebaki tu uishi bila kufanya kitendo cha maendeleo. Labda Adam na Hawa au wale wenzetu katika Misahafu kwamba walikuwa wanaishi kwa kula mana kutoka mbinguni, hawakuwa wanatifua ardhi, au kuharibu mazingira kwa njia ya maendeleo kwa sababu maendeleo ni *constraction through distraction.*

Kwa hiyo, tunachopambana hapa ni digrii ya kiwango cha uharibifu. Lakini kila maendeleo ni kitendo cha uharibifu wa aina yake. Na ndiyo maana tunazungumzia maendeleo endelevu kiasi gani unaweza ukadumisha maendeleo endelevu ndiyo tatizo kubwa linalomkabili binadamu na wanasayansi katika dunia ya sasa.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo nilikuwa napendekeza kwamba katika kufanya maendeleo wajibu wetu Wabunge, Viongozi, Wanasayansi ni kujua ile digrii kiwango cha uharibifu kinachofanywa na vitendo vyetu. Lakini kimsingi vinginevyo kwa mfano kila dawa au kemikali hata *asprine* ina madhara katika mwili wa binadamu.

Tatizo, tofauti ni kiwango tu kwamba kiwango fulani cha madhara kinavumiliwa hata katika madawa tunayotumia, tunayopata kutoka Hospitali. Kikipita kiwango fulani inakuwa hairuhusiwi. Kwa hiyo, ni vizuri tukajua tunazungumzua *agenda* ya aina hiyo kwamba *there is no development without distraction* na *development* ni *constraction through distraction.* Katika kulitazama hilo kwa mfano hili tatizo la *global warming,* Waamerika inasemekana inachangia asilimia 40 ya madhara ya *global warming.*

Lakini amekataa kuhudhuria kikao cha Kyoto kwa sababu wakubwa waliomuweka wanamwambia ukienda huko sisi tutakuondoa, kwa hiyo ilibidi ashike adabu na kutii matakwa ya wakubwa. Lakini *debate* ni maendeleo kwamba ukizuia hivyo tutaendelea vipi! Hilo ni moja.

*Pollution* inayotokea sasa hivi, haya ma-*plastic* kila ukiingia dukani unapewa mfuko wa plastic wa kuwekea bidhaa unazozinunua, na ukiangalia nchi yetu sasa hivi ni kama imepambwa na mifuko ya *plastic* tu kila mji na kila barabara nchi nzima imejaa mifuko ya *plastic.* Kwa baadhi ya magari ya abiria unavyopanda mle ndani wanakugawia chupa ya maji na zile chupa za *plastic* unatupa tu nje. Kwa hiyo, ukipita barabara ya kutoka Dar es salaam mpaka Arusha angalia kwenye barabara pembeni mle Dar es salaam mpaka Mbeya angalia barabara ilivyochafuka kwa mifuko ya *plastic* na Dar es Salaam mpaka Dodoma.

Mheshimiwa Spika, nilikuwa napendekeza kwamba labda badala ya kuwa na njia tu ya kufyeka nyasi kwenye barabara hizi vilevile kuwe na siku ya *operation* ya kuondoa mifuko ya *plastic* kusudi kutunza barabara zetu hizi. Kwa sababu hii mifuko ya *plastic* inapokuwa juu ya nyasi inazuia hewa na

mwanga usiingie chini ya ardhi. Kwa hiyo, ardhi vilevile inazidi kuharibika. Hilo lilikuwa ni pendekezo ikiwa ni sehemu mojawapo ya kusema tufanye nini.

Lingine ambalo nataka kutoa hapa kama caution ni kwamba tatizo la nchi maskini kama Tanzania ni kwamba katika baadhi ya mambo huwezi ukachagua, kwa mfano, mbolea ya chumvi chumvi. Uwiano wa mbolea ya chumvi chumvi na ile mbolea ya asili organic au samadi ni 30 kwa moja yaani unahitaji mifuko 30 ya samadi ili ilingane na mfuko mmoja wa chumvi chumvi. Sasa kwa nchi maskini kwanza hiyo mbolea ya samadi mifuko 30 ukiipata kutoka kwa ng'ombe ni shida. Lakini vilevile unataka uzalishe chakula kingi ili kutatua tatizo la njaa la watu wetu kama mnavyoona. Ukitumia samadi mazao utakayoyapata ni kidogo ukilinganisha na mfuko wa samadi.

Sasa katika mazingira ya namna hiyo licha ya madhara kwamba *chemical fertilizers* inaharibu ardhi. Lakini kwa sababu kuna tatizo la chakula kwa watu wako unalazimika kutumia mbolea ya chumvi chumvi ili upate chakula kingi kwa ajili ya kuokoa watu wasife njaa ingawa ni kwa muda. Maana kitendo hicho vilevile unaharibu ardhi. Kwa hiyo, ni jibu la muda mfupi lakini binadamu hawezi kukubali kufa kwa uzembe lazima aahirishe kifo kwa maana ya kusukuma siku ili aje afe baadaye. Urusi sasa hivi wamepata zaidi eka milioni 400 zimeharibika haziwezi kustawisha mazao kwa sababu ya kutumia mbolea hii ya chumvi chumvi.

La tatu, ambalo nataka nitoe kama *caution* katika kuchangia hapa mwenzangu aliyenitangulia amelisema. Lakini nataka niseme hivi kwa mfano, mchicha ukitumia mbolea kwenye mchicha inasababisha mchicha kukomaa kwa siku 20. Kwa hiyo, wataalam wanasema kwamba ile mbolea uliyotumia kwenye mchicha inakuwa bado iko hai ndani ya mmea wenyewe na unapochuma mchicha unakula na mbolea yenyewe. Kwa sababu kwa siku zile 20 bado inakuwa hajaharibika. Licha ya lile wazo la kusema unanyunyizia dawa kwa nje, lakini ile je, unayoweka chini ya mizizi unafanyaje? Ni *dilemma* kwa nchi maskini kama sisi kwamba unataka mazao kwa wingi na unataka mazao kwa haraka, utatue tatizo inabidi uli-solve kwenye njia hizi ambazo ni za haraka lakini zina madhara yake. Hata kama tungeamua watumie *organic manure* kwanza wataipata wapi. Lakini la pili, una idadi kubwa ya watu wako *Third World Countries* na ndiyo kwenye uhaba na matatizo ya chakula kila mwaka unafanyaje. Nadhani ni moja ya matatizo.

Mwisho, nilikuwa najadili na kupendekeza kwamba ugumu wa kuharibu madawa unatokana na kwamba njia halali ya kutumia *asprin* ni kumeza siyo kutupa nje popote pale, kumeza ndiyo njia halali. Sasa kama humezi ukitupa tu hivi hivi unaweza ukaharibu hali ya hewa, ukaharibu ardhi, ukitupa kwenye bahari unaharibu viumbe walioko kwenye bahari. Kwa hiyo, kiasi gani cha dawa duniani kitengenezwe kukidhi mahitaji halisi ya watu ndiyo tatizo. Ndiyo maana wakubwa siku hizi ni wajanja wanavyoona dawa walizozitengeneza ni nyingi na karibu muda wake wa kupungua nguvu umefika wanatoa misaada. Niliwahi kuwa Waziri wa Kilimo nikaletewa dawa kutoka Italy dawa ya mbolea siyo madawa ya ng'ombe, yale madawa karibu yalikuwa yana *expiry* baada ya miezi 6, kabla ya kujibizana bwana usiyalete amekwishaleta, yaliletwa *tons and tons* na huwezi ukayamaliza kuyatumia kwa muda ule mfupi, tukayapeleka Vikugi, pale Vikugi mvua zinanyesha zinayasomba kwa maji na yale maji yanakwenda kwenye mmea yanaleta madhara, hakuna njia nyingine yoyote ile. Ukiyachoma yanaharibu hewa, ukiyaacha yaende baharini yanaharibu samaki na ukiyaacha yabaki pale pale yanaharibu ardhi.

Mheshimiwa Spika, kwa hiyo *the best way* ya ku-*destroyed* madawa kwa sisi maskini ni *big problem.* Wenzetu wakubwa wanayapeleka Jangwa la Sahara wanarusha ndege wanakwenda kutupa kule. Sisi hapa ni *problem* na tunahitaji mabilioni. Kwa mfano, pale Mlologo wanasema wanahitaji bilioni 40 ku-*destroy* makemikali yaliyopo pale Mlologo. Sasa kama fedha yenyewe ya maendeleo ni shida sembuse upate fedha za kwenda ku-*destroy* madawa yale na usipoya-*destroy* yatakwenda kuua karibu watu wote wanaokaa Dar es Salaam unayafanyaje? Nasema *Poverty* ina matatizo na ndiyo maana baadhi vitu tunavyopokea kama misaada, haya magari kule Ulaya mahali pa kuyaweka ni tatizo, wakiona linakaribika kuharibu wanapeleka *dampo,* kwa hiyo kwa kuweka ndiyo Tanzania yanaletwa kama hapa *dampo second hand vehicles* yakishaharibika wanatupa kila mahali yanamejaa magari tu, kwao hii ni *solution* wanakubali kulitengeneza gari waliweke na magurudumu litembee lije lifie Njombe hapo maadam kwao wametatua tatizo.

Kwa hiyo nasema haya ni baadhi ya matatizo ya nchi maskini *you have no choice, choice* ni *very limited.*

Mheshimiwa Spika, baada ya kusema hayo, ningependa kusema kwamba umaskini ndiyo tatizo kubwa. Umaskini ni tatizo kubwa hata uamuzi wa lipi ulifanye kwa sababu ya maskini unajikuta uko kwenye matatizo. Kwa mfano, hivi sasa viazi mviringo kutoka katika nchi yetu baadhi ya mahoteli yanavikataa, nyanya wanazikataa, wanasema lazima zitoke nchi fulani na matunda yanakataliwa, maziwa yanakataliwa, mboga za mchicha zinakataliwa, na wakubwa ndiyo wenyewe uwezo wa kupima kiasi gani cha madawa kiko ndani ya mazao yetu haya. Kwa upande wa nyanda za juu kwa mfano, hivi sasa wanasema mito yote ile inayotoka nyanda za juu imejaa madawa kutokana na matumizi makubwa ya mbolea ya chumvi chumvi, kwa hiyo na maji nayo yana madhara yake. Wanaokunywa maji wanapata madhara hayo.

Mheshimiwa Spika, nadhani nimechangia kwa kuongeza tatizo zaidi. Ahsante sana. *(Makofi)*

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA MAKAMU WA RAIS (MHE. ARCADO D. NTAGAZWA):** Mheshimiwa Spika, kwanza nakushukuru kwa kunipa nafasi hii ili nitoe maelezo kuhusiana na michango ya Waheshimiwa Wabunge ambayo wote wameunga mkono hoja ya Azimio hili. *(Makofi)*

Lakini kabla sijaenda mbali na mimi nijiunge na Waheshimiwa Wabunge kumpongeza Charles Makongoro Nyerere, kwa kujiunga na sisi Waheshimiwa Wabunge wa Bunge la Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, tunaokubali dhana ya kiongozi mtumishi tuko hapa kuwatumikia watu wetu.

Mheshimiwa Spika, kwanza katika kuwashukuru wale waliochangia niruhusu niwataje kwa majina na wote kwa kweli wamesema hapa Bungeni hatakupata mchango kwa maandishi. Na wa kwanza kabisa ni Mheshimiwa William Kusila kwa niaba ya Mwenyekiti wa Kamati, alifuatiwa na Mheshimiwa Waziri Kivuli Karim Said Othman na Mheshimiwa Omar Mjaka Ali, Mheshimiwa Semindu Pawa, Mheshimiwa Paul Kimiti, Mheshimiwa Dr. Lucy Nkya, Mheshimiwa Dr. Suleiman Juma Omar, Mheshimiwa Jackson Makwetta ambaye amechangia mwishoni kabisa kwa kutia hofu zaidi kuliko kujenga, hapana. Ni mchango mzuri na inathibitisha tu kile tunachosema katika suala la mazingira unapozungumzia suala la mazingira na ukahusisha na maendeleo chochote utakachokifanya mwanadamu uwe mtu mmoja au kikundi kutafuta riziki au kutafuta maendeleo kina athari kwa mazingira. Jambo la msingi ni kuweka katika mizani athari hizi. Manufaa yanatokana na shughuli ile pamoja na kuwa ina athari isizidi faida inatokana na shughuli ile kwetu sisi kizazi cha sasa na vizazi vijavyo ndiyo changamoto tuliyonayo binadamu. Sasa nianze tu kwa yale ambayo Mheshimiwa William Kusila katika maoni ya Kamati ilikuwa ni kama ama pendekezo. Kwa kweli ya msingi ni kwamba liko hili la mifuko ya *plastic* limezungumziwa na Waheshimiwa Wabunge karibu wote waliochangia.

Mheshimiwa Spika, nilikuwa naangalia kanuni ya 51 ambayo inasema ni marufuku kuahirisha shughuli za Bunge lakini ni kwenye *Order Paper.* Sasa niruhusu tu niseme liko swali tutakalolijibu baadaye katika Mkutano huu kuhusiana na nini Serikali imefanya kuhusiana na suala la mifuko ya *plastic.* Tulikwishaanza kwa kuweka kodi kwenye mifuko ya *plastic.* Lakini kwa kweli inaonekana kodi peke yake haitoshi. Kwa hiyo, tunatarajia sasa kushirikisha sekta binafsi kwa ajili ya kufanya kitu wanaita *re-cycling,* Kiswahili nasikia wanasema kurejeleza sina hakika kama ni Kiswahili cha Kibondo au Kiswahili sanifu. Lakini tuna mipango hiyo na kwa kweli tutaeleza hivyo baadaye katika swali tutakalolijibu.

Kwa hiyo, kuhusu mifuko ya *plastic* yote yanayosemwa ni kweli na inabidi hatua zichukuliwe na tumeanza.

Mheshimiwa Spika, lingine ambalo ni la msingi kabisa ni suala la elimu kwa umma. Ni kweli mimi nakumbuka kuna Mheshimiwa Mbunge mmoja tena nadhani alikuwa ni Mheshimiwa William Kusila mwenyewe kwenye Kamati tulipopewa taarifa kwamba katika kuwasha moto hasa kwenye majiko ya mkaa inatangulizwa ile mifuko ya plastic halafu mkaa unawekwa juu, halafu mfuko wa *plastic* unapigwa kiberiti ili kuwasha mkaa jambo ambalo ni la hatari kabisa, moshi ule unachafua hewa na ni chanzo cha

kuweza kupata madhara ya kansa na aina mbalimbali tulizozitaja. Sasa Mheshimiwa alisema mimi nashukuru nilikuwa sijui. Kwa hiyo suala la elimu kwa umma ni la lazima.

Mheshimiwa Spika, niseme tena lingine linalofanana na hilo tutapofika hapa Ofisi ya Makamu wa Rais na Muswada wa Sheria Mama ya Mazingira mmoja ya kitu ambacho tumesema na kitakuwa katika sehemu ya Sheria ni kwamba sheria ile itabidi itafsiriwe kwa Kiswahili ili kila mwananchi anayejua kusoma na kuandika aweze kuisoma na kuielewa tunalenga kufanya nini? Kwa hiyo, elimu kwa umma ni kitu cha muhimu sana sana na tunalikubali hili.

Kuhusu taka za hospitali ni kweli taka za hospitali nazo kwanza tunajua zinakotoka kule hospitali ndiyo tunakwenda kutafuta ukarabati wa afya zetu. Sasa taka zinazotoka huko tuliokwishakupatwa maradhi zisiposhughulikiwa ipasavyo nadhani ni hatari zaidi. Lakini katika swali hilo ambalo tunatarajia kulijibu katika Mkutano huu na tutaeleza tunafanya nini katika kushughulikia suala hili.

Nadhani mwisho Mheshimiwa William Kusila alisema suala la mbolea na madawa ya kilimo au pembejeo tunayopata kutoka kwa Wahisani na kutoka kwa marafiki zetu wanaotutakiwa mema yaletwe kwa wakati ni kweli. Lakini kama alivyosema Mheshimiwa Jackson Makwetta ukiwa maskini mara nyingi sana huna uchaguzi, chaguo lako linakuwa si kama ambavyo ungependa.

Mheshimiwa Spika, lakini pia niseme katika nchi yetu hivi sasa nadhani uongozi wetu wa Taifa umetujengea heshima, Tanzania tunaheshimika tukijenga hoja kwa wale ambao ni Wahisani *Development Partners* wetu tukijenga hoja na tukawafikisha mahali wakaelewa. Bandari iko Dar es Salaam mbolea inahitajiwa Karagwe au Tarime ukamfikisha mahali Mhisani akaelewa tatizo mlilonalo la ukubwa wa nchi na hali ya barabara zenu bila shaka kwa heshima ambayo nchi yetu tumejenga na tunakubalika sasa, sidhani kama watatuletea mbolea au madawa ya kilimo ambayo yatachukua muda miezi 3 halafu yanakuwa ni sumu badala ya kuwa ni kitu cha kutusaidia. Kwa hiyo, wale tunaokwenda kufanya majadiliano hata kama ni katika suala la kupewa msaada tusione aibu kusema ukweli wa hali halisi ya nchi yetu tunajijengea heshima zaidi kwa kufanya hivyo kuliko kukubali.

Kama anavyosema Mheshimiwa Waziri wa Sheria na Mambo ya Katiba mara nyingine usema tunakubali mambo kichwa kichwa utadhurika. Kwa hiyo, nilitaka niliseme hili kwa kweli katika kugusia yale aliyoyasema Mheshimiwa William Kusila kwa niaba ya Kamati iliyochambua Azimio hili.

Mheshimiwa Spika, namshukuru sana Mheshimiwa Waziri Kivuli, Mheshimiwa Karim Said Othman kwamba yeye amegusia suala la uchafuzi wa mazingira katika maji na shughuli nyingine za maendeleo. Kama kwa mfano, wachimbaji wadogo wadogo wanaochimba dhahabu kutumia Zebaki, mercury kwa Kiingereza. Sasa kwa wanataaluma wa kemikali kama Mheshimiwa Semindu Pawa ni kweli Zebaki si suala la Azimio lililo mbele ya Bunge lako. Zebaki ni chuma *is the mental* lakini haya makemikali mengine ni vitu ambavyo si chuma ni *organic.*

Mheshimiwa Spika, lakini kwa faida ya Bunge lako Tukufu kwa sababu Serikali ya Tanzania, Serikali ya Chama chetu cha Mapinduzi inawajali watu wake, tunafanya nini katika eneo la wachimbaji wadogo wadogo, uko mpango ambao unafanya kazi hivi sasa si kwamba ni mpango kwenye karatasi. Kuna chombo kinaitwa Kiriba ambacho kinatumika kukamatisha dhahabu na unapotumia ile Zebaki inafanya kunyenyuka ili kupunguza athari ya Zebaki ile kuingia kwenye mkondo wa maji na kuchafua mazingira ya maji, na kwa maana hiyo samaki katika pengine Ziwa Victoria kule au hata katika mimea na mazao ya kilimo. Kwa hiyo liko jambo linafanyika nilitaka niligusie tu hili isije ikaonekana hatukulisikia au hatulifanyii kazi. Lakini uko mpango unaondelea na unafanya kazi kwa sababu ni kuhusiana na chuma ya Zebaki inayotumika kwa wachimbaji wadogo wadogo.

Mheshimiwa Spika, ninamshukuru pia katika kuzungumzia suala la yale mabwawa yanayowekwa maji kutoka Viwandani kabla ya kuyaachia kwenda katika mkondo wa maji yenyewe. Kwa lugha ya kiingereza wanaita *erection ponds* kwamba viwanda nina hakika katika sheria ya mama ya Mazingira hili nalo linazungumziwa. Viwanda vinatakiwa kuwaelekeza wanaotaka kujenga na kuendesha viwanda vya namna mbalimbali kwamba maji yanayotoka katika viwanda lazima wawe na mabwawa ya ukubwa kiasi fulani, yakae pale kwa muda gani ili yanapoondoka katika bwawa lile kwa kweli maji yale yawe hayana

madhara kwa afya ya binadamu na kwa mazingira. Kwa hiyo, namshukuru sana sana katika mchango wake kuyagusia hayo.

Mheshimiwa Omar Mjaka Ali namshukuru amezungumzia suala la utafiti ni kweli kuna haja kubwa sana. Lakini suala hili la matumizi ya *DDT* na kama lilivyozungumzwa katika Azimio hili ni kwa ajili ya mbu wanaoleta malaria. Sasa Waheshimiwa Wabunge wameeleza kwamba ni kweli unaitumia katika kudhibiti malaria *DDT as a chemical to combat factors of diseases* kuzuia wadudu wanaoeneza maradhi huwezi ukaweka mpaka utakapokuwa unatumia dawa ile ni kweli. Hili tunalikubali na tumeeleza Mheshimiwa Dr. Suleiman Juma Omar pale kwamba alikuwa anaitumia katika shughuli hiyo lakini baadaye ikaja ikaonekana katika zao la *Cocoa,* na kwa maana hiyo soko la kuuza *Cocoa* kule nje likawa limeathirika kwa matumizi hayo.

Mheshimiwa Spika, tunachokisema na katika Azimio tumetaja kemikali mbadala badala ya *DDT* imekwishapatikana, tatizo lake inamfanya huyu mbu sasa awe sugu. Ndiyo ile tunasema hata katika msemo wa kawaida mbuzi wa maskini hazai, akizaa sijui dume, akija mgeni yule dume anachinjwa. Kemikali mbadala imepatikana unatumia kumdhibiti mbu na mbu anakuwa sugu.

Mheshimiwa Spika, kuna wengine wametoa rai kwamba tusiishie kwenye hizi kemikali 12 tu tuangalie mfumo mzima wa matumizi ya kemikali mbalimbali. Lakini mahali pa kuanzia ni katika hili Azimio ili kwa ushirikiano wa Kimataifa kama tulivyosema Tanzania tutapata kujenga uwezo wa Kitaasisi kwa maana ya wataalam wetu na katika kushirikiana hivyo ndiyo tutakuwa tunapata fursa ya kusema kemikali tulizoanzia na hata ukisoma Mkataba wenyewe wa Stockholm.

Mheshimiwa Spika, maana wengine wamesema kwamba kwanza tumechelewa kwamba huu ni Mkataba wa 2001 na umeletwa leo hii katika Bunge lako Tukufu. Lakini katika Mikataba ya Kimataifa mnaanza na majadiliano. Majadiliano yameanza zamani sana mwaka 1995/1996 mpaka ilipofikia uamuzi sasa kwamba uwekwe Mkataba wa Kimataifa utakaosimamia masuala haya kuanzia kemikali hizi 12. Wanazungumzia juu ya initial 12 chemicals ni za mwanzo. Sasa itakapokuwa Mkataba umeanza kufanya kazi ndiyo tutakuja kujumuisha nadhani tahadhari na maoni ya Waheshimiwa Wabunge kwamba tusiishie kwenye Kemikali hizo tu. Lakini mahali pa kuanzia ni katika Mkataba wenyewe ukishaanza kufanya kazi. Kwa sababu tutakuwa tumejenga uwezo na tunapata fursa ya kujadiliana na watu mbalimbali.

Mheshimiwa Spika, na pengine hapa hapa nilihusishe suala lile kwamba tumechelewa kuleta Mkataba hapa kuridhiwa. Pengine ningependa niwatoe hofu Waheshimiwa Wabunge katika Mikataba ambayo imekwenda haraka kufikia hatua ni huu Mkataba wa Stockholm. Kwa niaba ya nchi yangu nilisaini Mkataba huu tarehe 23 Mei, 2001, mwaka 2002 tulikwishaanza kutekeleza matakwa ya Mkataba huu. Kwa sababu katika Mkataba wenyewe kiliwekwa kifungu kwamba kwa sababu mambo haya ni hatari na tulipokuwa pale Stockholm walikuja watu kutoka Greenland kule hakuna viwanda vya kemikali, hatumii hizi pembejeo na madawa ya kuua wadudu wanaoharibu mazao. Lakini walikuja watu pale wanatwambia sisi sasa hivi tuna matatizo haya makemikali yako katika miili yetu tumepimwa yakaonekana kuonyesha kwamba madawa haya hayana mipaka.

Kwa hiyo katika kujadiliana tukafika mahali tukasema Mkataba huu kwa jinsi ulivyo muhimu kwa afya ya binadamu tusingoje utekelezaji wa baadhi ya vipengele vyake mpaka zitapokuwa nchi 50 zimeridhia kama tunavyofanya sisi katika Bunge hili Tukufu. Kwa hiyo, tulishaanza kutekeleza Mkataba wa Stockholm kuanzia mwaka 2002 na ndiyo tulianza na ule mradi wa *African Stock Piles Programme* kupata takwimu na wingi wa madawa chakavu ya kilimo. Kama tusingekuwa na kipengele hicho mpaka leo hii tusingekuwa tunazungumzia suala hilo kwamba tunayo tani kama 1,000 za madawa chakavu.

Kwa hiyo, ni kweli tunaweza tukasema kwa hali ilivyo Azimio ili lingekuja hata mwaka 2000, sasa mwaka 2000 ulikuwa haujawekwa saini. Lakini kwa kweli kwa maana ya Mkataba kuwekwa saini mwaka 2001, mwaka 2002 tukaanza kutekeleza baadhi ya vipengele na mwaka 2003 kama tungepata muda hoja hii ilikuwa ije kwenye *Order Paper* lakini hatukupata muda, na inatuthibitishia kwamba muda kwa kweli ni raslimali adimu ni vizuri kuutumia ipasavyo. Kwa hiyo, ningependa tu niwatoe hofu kwamba hatujachelewa.

Mheshimiwa Spika, nije kwa Mheshimiwa Semindu Pawa ambaye namshukuru sana kwa mchango wake na kama Mkemia aliyebobea namshukuru kwanza kwa kutofautisha kati ya *Oganic pollutants* ambazo si vyuma si *mentals* na Zebaki ya Uzigi.

Lakini pia kuna kitu amekisema kizuri sana kwamba wakati mwingine linafanyika jambo la biashara na biashara wakati mwingine *money has not conscious,* fedha haina dhamiri. Ukitaka kupata fedha utakwenda kichwa kichwa mpaka upate fedha ile na ni kweli hata baadhi hasa ya Makampuni makubwa wakiona pengine makemikali waliotengeneza ni pembejeo za kilimo na karibu soko linalengalenga kidogo na muda utakwisha na yatakuwa ni tatizo kwao wanaweza wakasema tunayatoa msaada mahali fulani.

Sasa Mheshimiwa Semindu Pawa ametupa tahadhari kwamba kuna suala la biashara tusije tukabweteka, lakini tutumie bongo zetu kuona masuala haya. Na vilevile kuna kitu kimoja amesema wakati mwingine yanabadilishwa majina linatumika jina la biashara badala ya jina la kikemikali ili kujaribu kuficha mambo fulani fulani, kwa sababu jina la kemikali linasema mambo mengi zaidi.

Kwa hiyo, ningependa nimshukuru kwa mchango wake na kwa kweli kile Kiwanda cha Twiga ambacho walifanya kazi ya kuteketeza baadhi ya yale madawa chakavu tunawashukuru kwa hilo na ndiyo hata katika hilo swali tutakalolijibu baadaye tunaelezea mambo ya namna hii. Kwa sababu Waheshimiwa Wabunge hasa kwenye Kamati walitwambia na kutushauri. Kwamba badala ya Wahisani kutupa fedha za kukusanya na kusafirisha haya madawa chakavu. Hivi kwa nini hawataki kutupa uwezo wa kuwa na kiwanda chetu!

Mheshimiwa Spika, maana tulichokieleza kwamba baadhi ya madawa haya ili uweze kuyateketeza na yasikuletee madhara kwa afya ya binadamu na mimea inakubidi lile tanuri uweze kupata kiwango cha joto nyuzi joto 3,000.

Sasa nyuzi joto 3,000 mwili wa binadamu nyuzi joto 37.5 joto la kawaida. Nenda kwenye 3,000 kwa kweli pale ni kwamba kitu kinakuwa *nothingness* hakipo tena kitu cha namna ile kwa nyuzi joto hizo. Sasa katika Afrika yetu yote mpaka hivi sasa hatuna kiwanda cha namna hiyo wala hatuna ujuzi.

Lakini walichotushauri ni kwamba hawa wanaotaka kushirikiana na sisi na wanaotutakia mema kwa nini wasitujengee uwezo. Kama Wachina wanavyosema kama unapenda kunisaidia nifundishe kuvua samaki usinipe samaki, nikishamla yule samaki si nitataka mwingine, ndicho walichotushauri Waheshimiwa Wabunge kwenye Kamati na mimi nakubaliana nao kabisa.

Mheshimiwa Spika, nikija kwa Mheshimiwa Paul Kimiti, ninamshukuru sana na yeye kwa kweli alikuwa anazungumzia athari hizi kwa mfano, nguo ambazo si za pamba, zina *Petro Chemicals* zina pia matumizi ya *DDT* nimekwisha kuzungumzia na aligusia pia kwa nini ni kemikali 12 tu na si zaidi nimekwisha kulisema hili.

Lakini la msingi ni kwamba ushirikiano wa Kimataifa kupitia Azimio hili utatupa uwezo wa kujua ni kemikali gani mbadala na hata nyingine mpya ambazo pengine zitagunduliwa baada ya Mkataba huu kuanza kufanya kazi ndizo zitatupa uwezo na fursa ya kusema twende vipi. Lengo ni kuthamini afya ya binadamu na kuzuia athari kwa mazingira ili tuweze kupambana na umaskini ipasavyo.

Mheshimiwa Spika, najua Mheshimiwa Jackson Makwetta anasema jamani umaskini ndiyo tatizo, ni kweli umaskini ni tatizo na ni mzigo tu, na tena tatizo la umaskini hata huwezi ukampa yule tuliyemsema katika majibu ya maswali ya Mheshimiwa Waziri wa Elimu na Utamaduni. Tatizo la umaskini si mzigo wa kumbebesha Mnyamwezi.

Mheshimiwa Spika, Dr. Lucy Nkya na yeye aliligusia lakini yote nimekwishakuyagusia. Mkataba umechelewa na kadhalika. Lakini yeye amezungumzia kwa mfano, utafiti. Utafiti kuona hivi mboga na maziwa kwa wakazi kama wa maeneo yanayotumia *DDT* kupambana na mbu ni kiwango gani cha kemikali hii kinabaki katika mboga hizo. Ametoa ushauri na tunauzingatia kwa sababu lengo la

kupitisha Azimio ni kujijengea uwezo wa kupata hata namna ya kufanya utafiti hadi ngazi ya Kimataifa na kwa wataalam wa ndani ya nchi na wale wa nje ya nchi yetu.

Yeye ametumia mfano mmoja tu nalirudia kwenye elimu ya umma na akatumia mfano ambao zamani nilikuwa nasikia kwamba mtu akiambiwa unahamishiwa Mkoa wa Kigoma na hasa Wilaya za Kasulu na Kibondo anasema aah kule kuna funza, mimi namshukuru hata Moshi kulikuwa na funza.

Pengine alikuwa anataka kutuambia ukitumia kemikali hizi bila kupata elimu hasa utumie vipi unaweza ukapata madhara hata kama kwa muda mfupi unaona kwamba unapata manufaa kutokana na kemikali ile. Ninamshukuru kwa taarifa hizi maana huyo mdudu funza nadhani si tatizo wala si mzigo wa kusema haubebeki.

Lakini pia amezungumzia suala ambalo ni muhimu na tulikuwa tunazungumzia ndani hapa asubuhi liliulizwa hapa suala la ushirikiano. Sisi katika Ofisi ya Makamu wa Rais tunafanya uratibu *(Coordination).* Alizungumzia kwa mfano *extension officers* katika maeneo wanakolima kahawa na pamba, madawa yale ya kilimo ya kuulia wadudu yana madhara yake kama kemikali. Hapa akanikumbusha kwamba katika eneo moja alilolisema katika Wilaya ya Mbinga wakulima wa kahawa wanatengeneza dawa ya asili, wanatumia pilipili au majani ya mpapai na mimea ya asili mingine kutengeneza dawa ya kuua wadudu wanaoshambulia majani ya kahawa na hata pembejeo.

Nilipopata fursa ya kutembelea kule nilisema suala hili nadhani ni muhimu likatiliwa mkazo ili dawa hizi zinatokana na mimea ya asili, ziweze kupatikana kwa msingi iwe ni mbadala wa haya makemikali tunayotumia ya viwandani. Kwa kuridhia Azimio kama hili sisi Watanzania tunaweza hata tukajenga hoja katika Mkutano wa Kimataifa kwamba twendeni mkaona mimea yetu ile ina sifa zipi au *characteristics* zipi ili iweze kuilima kwa wingi na tupate dawa zile kwa wingi kama hizi za kiwandani.

Namshukuru sana Mheshimiwa Dr. Omar katika yale aliyozungumzia yanashabiiana na yale ya wengine. Isipokuwa kuna moja amelisema linalohusiana na meli za kigeni kutupa taka katika maeneo ya bahari yetu. Ni kweli mpaka hivi sasa hatuna chombo au utaratibu wa kufuatilia hizi meli zinazopita, wengine wakifikisha mafuta wanaposafirisha yale mameli makubwa ya mafuta uchafu ule unamwagwa wapi? Maana wako huko baharini, hatuna vyombo, hatuna nini. Kwa hiyo ni kitu ambacho anatutahadharisha kwamba inabidi tuliangalie hili na tuwe na chombo kama hicho.

Sasa sina hakika nadhani katika Muswada ule wa *(Deep Sea Fishing)* Uvuvi wa Bahari Kuu kulikuwa na kitu kama hicho nacho kingeweza kutusaidia kuona kwamba kwanza raslimali yetu samaki na viumbe vingine vya baharini haiibiwi katika eneo lile la bahari kuu. Sasa fursa ile ingetusaidia kuona meli ambazo zinachafua bahari yetu. Kwa hiyo, nadhani anatukumbusha kwamba pengine ni kuwa makini kutekeleza baadhi ya sheria zetu wenyewe.

Mheshimiwa Spika, suala la moshi wa magari *(exhaust fumes).* Ni kweli kabisa hili ni tatizo kubwa katika maeneo hasa ya mijini kwenye msongamano wa magari. Bahati nzuri katika sheria mama ya mazingira hili limepewa nafasi ili liweze kudhibitiwa na najua pengine wananchi wale wanaotumia magari haya watasema sasa Serikali mnasemaje, lakini sisi hoja yetu ni kwamba endesha gari lako lakini usimwue mkazi wa mjini kwa kutumia na kutumia gari linaloharibu mazingira. Fanya mapendo ya jirani tumia gari lako lakini mruhusu mwananchi mwingine hata mwende kwa miguu na mkazi wa mahali yanapopita barabara kusiwe na athari ya kuweza kumdhuru afya yake.

Mwisho nigusie alilolisema Mheshimiwa Makwetta kwamba kama nilivyoanza mwanzo kiwango cha uharibifu kwa maana unataka kupiga hatua ya maendeleo. Ndiyo maana katika mazingira kwa ujumla wake kila tunalotaka kufanya hasa katika mambo haya ya maendeleo kuna kitu tunaita ni athari kwa mazingira *(Environmental Impact Assessment)* katika kila mradi ili tunapoanza kutekeleza mradi ijulikane mradi ule utaathiri mazingira kwa kiwango gani. Hilo ni jambo la msingi kabisa na katika sheria mama ya mazingira hili litajitokeza wazi wazi na tunatarajia Waheshimiwa Wabunge watatupa mchango wakati wa kuwa Muswada huo umefikishwa Bungeni.

Lakini hatutoishia hapo kwa sababu pia limezungumziwa suala la *(monitoring)* ufuatiliaji. Hata kama umekwishasema nitachukua hatua hizi kuzuia athari kwa mazingira, lakini inawezekana wakati wa utekelezaji hili lisifanyike, sasa lazima kujipa uwezo na kuwa katika nafasi ya kufuatilia kama kweli hicho kilichotamkwa kinafanyika.

Mheshimiwa Spika, haya ndiyo kwa ujumla yaliyokuwa yametajwa labda nisahihishe moja tu alipozungumzia juu ya kiwango cha emission inayochangia mabadiliko ya tabia ya nchi global warming na climate change kwa nchi ya Marekani si asilimia 40 ni asilimia 25.

Lakini sasa hivi katika majadiliano ya namna ya kuridhia itifaki ya kyoto ambayo sisi tumesharidhia kinachojitokeza ni kwamba ni mjadala kuhusu soko huria. Kwa sababu hapa tunakwenda kwenye *carbon trading* unatoa *carbon* kiasi gani na unafanya nini mahali pengine kuiondosha hiyo *carbon* katika hewa na unalipwa kwa kufanya kazi hiyo. Kwa hiyo, hata kupanda miti huko tuendako itakuwa ni kazi nzuri inayolipwa. Ukipanda miti vile vile unatekeleza mkataba wa kuzuia nchi kugeuka jangwa, kwa hiyo, tunaua ndege wawili kwa jiwe moja.

Mheshimiwa Spika, nilitaka niseme hili katika kujaribu kutoa maelezo mafupi tu kwa Waheshimiwa Wabunge waliochangia hoja ya Azimio hili ambalo nawashukuru kwa kusema wengine wamesema limeletwa limechelewa ni kwa maana ya umuhimu wake na ushirikiano wa nchi yetu na Jumuiya ya Kimataifa katika suala hili lenye maslahi kwa watu wetu wote.

Mheshimiwa Spika, baada ya kusema hayo naomba kutoa hoja. *(Makofi)*

**WAZIRI WA ELIMU NA UTAMADUNI:** Mheshimiwa Spika, Naafiki.

*(Hoja ilitolewa iamuliwe)*
*(Hoja iliamuliwa na Kuafikiwa)*

*(Azimio la Kuridhia Mkataba wa Kimataifa wa Stockholm wa Mwaka 2001 liliridhiwa na Bunge)*

*(Saa 06.36 Bunge liliahirishwa Mpaka Siku ya Jumatano Tarehe 4 Februari, 2004 Saa Tatu Asubuhi)*